# Neno Lililonenwa Ndiyo Mbegu Ya Asili

Jeffersonville, Indiana, Amerika
Machi 18, 1962

1 Habari za asubuhi marafiki. Ninayo furaha kuwa hapa. Asubuhi hii tunawahi kidogo kuanza. Mara nyingi tunakosa nafasi ya kuwatosha watu kukaa, na ninajua inawawia vigumu kusimama. Nilikuwa nimepanga kuwa asubuhi hii iwe ndio ule wakati ningekuwa na muda mwingi. Nafikiri ingekuwa vema zaidi kama wakati ibada inapoendelea, wengine wakati na wengine wamesimama na kisha walioketi wawaachie nafasi waliosimama nao waketi, na kama kuna atakayetaka kutoka nje kidogo au atembee kidogo, kumbuka kwa kuwa ibada ni ndefu, hilo litakuwa sawa kabisa. Ndipo tutaweza kubadilishana nafasi hivyo.

2 Na sasa wapo … Tunajua wapo katika mpango wa ujenzi hapa hekaluni liwe kanisa kubwa na pana lenye nafasi ya kuketi ya kuwatosha watu. Nafikiri nafasi ya kuketi hapa kanisani ni kama watu 250 au 300 hivi, na inaelekea kuwa watu zaidi ya mia moja zaidi waliomo humu leo. Sasa itakuwa … Na nilipowasili niliona watu wakiendesha magari kwenda nyuma na mbelehawapati nafasi ya kuegesha magari na isitoshe, wanapofika mlangoni na kukuta ukumbi umejaa kabisa na watu wamesimama kuzunguka kuta zote na kadhalika; basi wanaondoka na kwenda zao. Na tunataka kila mmoja asikie Ujumbe wa Bwana tunapojitahidi kuuleta.

3 Nataka nitangaze hilo mara moja, nitajitahidi kuhubiri hadi saa sita adhuhuri na kisha baadaye … Tutamaliza ibada saa sita. Hiyo itampa muda kila mmoja aende kupata chochote ale. Wakati huo huo mchungaji Ndugu Neville hapa atakuwa na ibada ya ubatizo. Na ninyi watu mnaochomoka ili mkapate chochote mle, na ndipo tutarudi hapa na nitajitahidi kuwa mimbarani saa nane na kuendelea alasiri hii.

4 Nimekuwa katika maombi wiki hii, na nisingeweza kumaliza somo hili kama sikupunguza robo au theluthi hivi ya yale niliyotaka kuwaambia watu. Sasa tunawashukuru kwa ushirikiano wenu mzuri katika kuja mikutanoni na yale mliyotutendea na kutusaidia na kutuombea.

5 Kitambo kidogo kilichopita nilitunukiwa kuongea na mzee mmoja na mwanamke ambaye … tunawafahamu Ndugu na Dada Kidd ambao wamekuwa waaminifu miaka hii yote. Walinifikia muda mfupi uliopita. Niliwaambia wapitie; nilitaka kuonana nao kidogo na ni tunu kuongea na wazee ambao walikuwa tayari wanahubiri Injili nilipokuwa nikingali … mtoto.

Na ile Injili tukufu inaendelea kuwa bora zaidi kadiri tunavyokaribia mwisha wa njia.

6 Na sasa kuna vitambaa vya kuombewa vipo hapa na ninataka kuviombea punde kidogo. Na sasa tuinamishe vichwa vyetu kidogo ili tuombe.

7 Baba yetu wa mbinguni, Ulisema katika Neno Lako “Kama Nikiinuliwa juu kutoka duniani Nitawavuta watu wote waje kwangu”. Na hilo ndilo kusudio letu katika maisha, ni kukuinua Wewe juu ya kizazi hiki cha watu walio kufani kuwa Yesu Kristo bado ni Mwana wa Mungu, Mwokozi wa ulimwengu. Nami nafurahia kujua kwamba ninaishi mahali penye watu wanaoamini hilo, pamoja na maelfu waliomkubali Yeye awe Mwokozi wao.

8

Na tukijua kuwa baada ya maisha haya kwisha kutakuwepo na maisha ng'ambo ya pili yatakayokuwa ya utukufu mno kiasi kwamba masumbufu na masaa haya machache tunayopita kwenye vivuli vya maisha hapa kwenye uwanja wa majaribio, kwamba tunaingia tu kwenye mkondo sasa tukingojea hesabu za kinyumenyume, kwani punde si punde wakati wa Mungu utatimia. Ule mkono mkuu ambao umezuia wakati kwa muda mrefu mno, hatimaye utaachilia na Kanisa Lake litanyanyuka kutoka duniani kwenda angani hadi nchi ambayo hakutakuweko magonjwa, huzuni, uzee, kifo. Ndiyo sababu tumekusanyika hapa leo. Bwana, ni ili kudhihirisha tunavyojisikia kuhusu mambo haya.

8 Tunafurahi kwamba hii si kuwaleta watu pamoja bure, ila imethibitishwa ni uhalisi mkuu kupita yote iliyowahi kufahamika hapa duniani, kwamba Mwana wa Mungu si mfu,

Yeye aliyetoa hizo ahadi, bali yu hai miongoni mwetu daima. Na tunayo furaha mno asubuhi hii Bwana, juu ya yote, hata ijapo dunia ni mali yetu, na tungeweza kubaki vijana kwa miaka mamia na kuufurahia, lakini bado ingekuwa tu ni kwa kipindi fulani, ukilinganisha na wakati waliowekewa wale wampendao Yeye. Hivyo tunajaribu kumwelekeza ndugu yetu na dada yetu kwenye saa hii kuu inayotukaribia. Na tunapoiona saa hiyo ikiwadia, Bwana, mioyo yetu inawaka moto. Tunataka kujiandaa.

9 Mmoja baada ya mwingine tunatelemka njia ya kwenda chini. Ni kitambo kidogo kilichopita tumemzika mmoja miongoni mwetu, Dada yetu Bell, aliyekwenda haraka (kufuatana na ombi lake), ghafla mno hata hatukuweza kumfikia na kumwombea, lakini ndivyo alivyoomba kuondoka - tunaona jinsi Ulivyo mwema hata Unatupa yote tunayotamani mioyoni. Hakuna lolote usilotupa. Uliahidi hivyo.

Sasa tunakuomba uipe mioyo yetu kukuelewa leo - wale wasiokufahamu. Wasaidie wenye dhambi watubu; wasaidie wagonjwa wapate ufahamu wa uponyaji wa Mungu. Ee Mungu uwabariki watakatifu wako na uifunge mioyo yao pamoja. Na kanda hizi za mahubiri zitakapopelekwa katika miji mbalimbali katika mataifa yote duniani, nawaombea ndugu wahudumu ambao labda hapo awali walikuwa wameelewa vibaya, sasa waelewe vema, ili Kanisa Lako lipate kuwa tayari.

10 Na sasa Ee Bwana, Wewe uliyenitoa mimi kwa mama yangu, Wewe uliyenitunza siku zote za maisha yangu, na umenileta hadi saa hii, kwa neema yako; Hali najisikia kuwa ni mapenzi Yako niwaeleze watu ni kwa nini nimefanya mambo haya ambayo nimeyafanya. Naomba hili liwasaidie watu kupata ufahamu bora zaidi, Bwana, kuhusu upekee wa mtumishi Wako.

Utujalie haya, Baba, na haya Maandiko Matakatifu na somo hili na maelezo ambayo tumeandika hapa wiki hii pamoja na kuomba na kujifunza. Naomba yaanguke kwenye udongo mzuri popote yatakaposikika - Udongo utakayoyatunza na kuyalisha na sifa zote zije Kwako, kwani tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

11 Kwa watu waliokaa kwenye magari huko nje ambao hawawezi kuingia kanisani, ninaweka chombo hiki kidogo hapa, na funguweni radio zenu mita 1150 - 1150 na utapata Ujumbe huu katika radio garini mwako. [Ndugu Branham aeleza kidogo kuhusu matumizi ya chombo hicho - Mh.]

12 Sasa, kwa marafiki zangu ambako kanda hizi za mahubiri zitafika, najisikia kuwa nawiwa kuwaelezea watu sababu za mengi ambayo nimeshasema na kutenda. Mara nyingi watu wamenijia na kusema, "Kwa nini unafanya hivyo ndugu Branham? Kwa nini ulisema hivi? Na ni kitu gani kinachokufanya ufanye hivi? Sasa, kwa moyo wangu wote, yote ambayo nimeyafanya, nimefanya kwa nia njema sana jinsi nifahamuvyo. Na kila ambacho nimekwishakisema, nimekisema kutoka moyoni mwangu. Na nimefanya hivyo kwa makusudi; na nitajitahidi asubuhi hii kwa msaada wa Mungu kueleza kutoka kwenye Biblia makusudi na kwa nini nikafanya hivyo.

13 Na sasa labda, katika kundi, katika kundi la watu kiasi kama hiki, huenda pakawepo wahudumu kadhaa walioketi hapa, na ni wengi watakaosikia hili, na ningefurahi kama ningekuwa na muda wa kutosha ili ni … niyalete yale niliyowaza yaliyomo katika Maandiko … niyalete Maandiko pia, bila shaka kwa watu. Lakini kwa ndugu zangu: Hata kama hujakubaliana nami - sasa ninazungumza nanyi hapa na pia kwa wale watakaonisikia kwa njia ya kanda - huenda hukubaliani nami zaidi hasa kutokana na msimamo wangu kuhusu yale ninayofikiria kuwa ni sahihi. Na unayo haki ya kutokukubaliana nami unapoona mambo tofauti na ninavyoona; lakini natumaini kwa msaada wa Mungu asubuhi hii, nitaweza kuwaonyesha kwa nini nimechukua msimamo huu.

14 Na sijawahi … imetokea mara nyingi nimeyakemea makanisa, madhehebu, uvaaji nguo wa wanawake, mienendo ya wanaume. Nafikiri nimeyathibitisha hayo kwa Maandiko. Na haijawahi tokea wakati wowote, Mungu anaujua moyo wangu sijawahi kuwa na nia mbaya kumhusu yeyote. Hata kama hawakukubaliana nami kiasi cha jinsi mashariki ilivyo mbali na magharibi, bado nimewapenda. Na wakati wote niwapo na Roho wa Mungu ndani yangu daima nitalipenda Kanisa Lake- watu Wake. Hata wafanye nini, hiyo haidhuru chochote. Bado nawapenda.

15 Nakumbuka wakati mmoja mtu mmoja aliyeitwa Musa. Watu hao daima (tungeita tunavyozoea huku kusini) walimsumbua - walimfanya daima akose utulivu. Kila kitu walinung'unika au kulalamika na kadhalika. Lakini Musa, ilipofikia makabiliano, Mungu

aliposema, "Jitenge nao kwa sababu ninakwenda kukuondoa miongoni mwao na kukufanya wewe uwe taifa, Musa alijitupa katika mkondo wa ghadhabu ya Mungu. Akasema, nichukue mimi na wala usiwaangamize hawa watu," kwamba hatimaye angewaita hao watu waasi, (waliomwasi Mungu na kumwasi yeye), na hata hivyo aliwapenda mno hao watu hata aseme, " Niondoe mimi na uwaachilie wao". Hivyo alikuwa Kristo ndani ya Musa.

Na kama mtu, hata ijapo mwingine hatokubaliana naye, iwapo hatokuwa na tabia hiyo, basi naamini amepungukiwa na Kristo - kama kutoka moyoni mwake sio mdomoni mwake, lakini moyoni mwake, kama hana huruma ya namna hiyo kuhusu wanadamu …

16 Nilishangazwa wakati fulani (sio tu kwa ajili ya kuwa na huruma wakati huu), bali kulikuwako na mkutano Chicago na mtu mmoja mweusi aliendelea kusema, "Nataka nimwone daktari Branham". Alikuwa amevaa kofia kubwa na misalaba mikubwa urefu na upana wa inchi nane au kumi hivi kifuani pake na joho alikuwa amevaa kipekee sana na vipuli vya kiajabu na shanga na kadhalika. Na nikamwambia Ndugu Baxter aliyekuwa msaidizi wangu, " Mlete chumbani nionane naye:. Ndipo akaketi karibu nami na kusema, "Nikuchukulie kama Baba au Mchungaji au 'Mzee" au unataka nikuchukulie kama nani?".

21

Nikasema, "Kama unanipenda niite 'ndugu'". Na yeye kwa heshima alifanya hivyo, naye basi akanielezea cheo chake ambacho, loo, ningetumia mistari kadhaa kuandika kwenye karatasi jina la kanisa na cheo chake

kanisani.

17 Lakini aliniambia kitu kimoja ambacho daima kimebaki moyoni mwangu. Alisema, "Navutiwa na hili Ndugu Branham. Nina … Aliniambia kitu kilichomvutia kanisani mwake na mambo yake. Alisema, "Navutiwa na jumuia moja ya watu, alisema " na hiyo ni jumuia ya wanadamu".

Nikamwambia, "Hapo tutashikana mikono." Jumuia ya wanadamu, kila mtu, kila ungamo, kila rangi, kwa kila mtu aliyefiwa na Kristo, ndicho kivutio changu asubuhi hii. Na nimejitahidi daima kufanya hicho kiwe kivutio changu.

18 Sasa nataka kusoma … Ndipo … Sikusudii kuhubiri kwa sababu huenda ikawa - Niliyo nayo hapa ya kusema yaweza kunichukua masaa manne au matano; kwa hiyo baada ya masaa mawili hivi tutafumukana tukale chakula cha mchana na kurudi hapa kama saa nane … uwe hapa kabla ya saa nane kwani napenda kuanza saa nane kamili. Uwe hapa kama saa saba na nusu ukiweza. Ndipo tutaweza kutoka ibadani muda mzuri jioni hii.

Jioni hii itabidi niondoke kwenda Tifton, Georgia ambako tutakuwa na ibada kesho jioni katika jumba la mikutano la shule ya sekondari pale - ibada ya mahubiri tu. Na kutoka hapo sijui. Basi ni kokote Atakakoniongoza kutoka hapo . Mahali pengi - Ndugu Arganbright na wengine wameita kutoka ng'ambo, tuanzie moja kwa moja kutoka huko, kukatisha hadi magharibi hadi Canada kuzunguka ulimwengu. Lakini nita … mtajua … aminini … Naamini utaelewa vizuri baada ya mimi kumalizia, kama Mungu atanisaidia niwapitie katika jinsi ile ile niliyopewa, basi baada ya ibada mtaelewa, natumaini.

19 Na kama kuna maswali yoyote ambayo hamjaelewa, nawaomba mlete vitabu vyenu, ndipo ninyi wenye vinasa sauti (tepu rekoda) mnaweza mkapata kanda mkaziweka nyumbani kwenu mkaketi na mioyo iliyo wazi-mioyo iliyo wazi tu. Basi jiachilie na kusema, "Bwana sasa nimetulia, ninakwenda kusikiliza", na upatapo kitu fulani, zima kinasa sauti na uyaendee Maandiko. Biblia inasema, Yesu alisema "Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi". Mnaona? Pitia katika Maandiko na uone kama hivyo si sahihi.

20 Sasa napenda tufungue … (samahani, hapa huyu ananionyesha vipasa sauti nitakavyotumia. Hapa vipo vingi asubuhi hii na sijui nianzie na kipi). Sasa tufungue Maandiko … Ninakwenda kuanza na Mwanzo niishie Ufunuo jioni hii. Naliamini Neno. Na sasa kama mtu angetaka mwingine achukue … chukua kalamu na karatasi na kadhalika kwani nina Maandiko mengi. Nitapenda kusoma Maandiko wakati wote.

Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji. Roho wa Mungu akatulia juu ya uso wa maji.

Mungu akasema, Iwe nuru, ikawa nuru.

Mungu akaiona nuru ya kwamba ni njema, Mungu akaitenga nuru na giza. Mungu akaiita nuru Mchana na giza akaliita usiku. Ikawa jioni ikawa asubuhi siku moja.

Mungu akasema, Na liwe anga katikati ya maji likayatenge maji na maji. Mungu akalifanya anga akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga ikawa hivyo. Mungu akaliita lile anga Mbingu. Ikawa jioni ikawa asubuhi siku ya pili.

Mungu akasema, maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, ili pakavu paonekane, ikawa hivyo. Mungu akapaita pale pakavu Nchi, na makusanyiko ya maji akayaita Bahari, Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Mungu akasema, nchi na itoe majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake ambao mbegu zake zimo ndani yake juu ya nchi, ikawa hivyo. Nchi ikatoa majani mche utoao mbegu kwa jinsi yake. na mti uzaao matunda ambao mbegu zake zimo ndani yake. Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tatu.

21 Sasa ninataka nianze nianze somo langu asubuhi hii nililoliita "Neno lililonenwa ndiyo mbegu ya asili". Sasa hapo ndipo ninapotaka kuweka msingi wa somo lenyewe - " Neno lililonenwa Ndiyo Mbegu ya Asili". Sasa kama utaona Mungu alisema "Kila kimoja kizae kwa jinsi yake". Chochote kilichokuwako kilizaa kwa jinsi yake.

Sasa hili Neno la Mungu ni la milele. Mungu, ambaye adumu milele hawezi kusema jambomoja na kisha abadilishe kuwa kitu kingine baadaye, au afanye uamuzi ulio bora kuliko aliofanya awali, kwani uamuzi wa Mungu ni mkamilifu. Yeye hawezi … pindi Neno Lake linaponenwa, kamwe halitakufa. Ladumu daima, na haliwezi kufa kwa sababu Lenyewe ni Mungu. Kwa kuwa Yeye Mwenyewe hafi Neno Lake pia halifi. Ndiyo sababu tunasoma katika 1 Yohana … au Yohana Mtakatifu sura ya kwanza, kuwa "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu. Naye Neno Alifanyika mwili". Neno Yule Yule aliyenenwa pale mwanzoni akiwa na kusudi Lake la milele alikuja na akafanyika mwili na akakaa miongoni mwetu - Neno la Mungu.

22 Miaka kadhaa iliyopita nilisikia kuwa mwanamke mmoja (sasa hili haliwezi kuthibitishwa) aliramba kwa ulimi madini yenye nguvu ya moto wakati akijaribu kuchanganya ili kutengeneza ndimi za saa za ukutani na mikononi - ilimwua huyo mwanamke. Na miaka mingi baadaye, kwa kuwa walihifadhi fuvu lake la kichwa ili kuendelea kulifanyia utafiti kuhusu kisa cha kifo chake, walisema ungeweza kuweka juu ya fuvu hilo, vifaa vya uchunguzi na ukinguruma pale, bado ungesikia miendo ya sauti za nguvu iliyokuwa katika ile madini yenye moto wa kujiendesha, ikiendelea katika fuvu la kichwa hicho hata baada ya mwanamke huyo kufa tangu miaka mingi. Nguvu katika madini hiyo daima zikiendelea kujiendesha.

23 Neno la Mungu daima linaendelea. Huwa ninawaambia kuwa kama tungekuwa na chombo cha kuweza kudaka sauti ya mtu, sauti yangu ninayonena leo miaka kumi ijayo bado ingeweza kudakwa hewani. Ni kama kudondosha changarawe katikati ya dimbwi. Yale mawimbi madogo yanaendelea kiasi kisichoweza kuonekana kwa macho lakini huendelea hadi kuishia ukingoni. Na mawimbi ya sauti zetu husafiri daima kuzunguka dunia; kwa hiyo sauti zetu, yale tusemayo yatajakuwa hukumu yetu. Ushuhuda wetu utasimama dhidi yetu. Sauti zetu wenyewe zitagonga masikioni mwetu wakati tukisimama hukumuni pale kile chombo kikuu cha Mungu kilichonasa kila sauti iliyonenwa kila neno lililotamkwa.

24 Sasa kuna njia moja tu ya kufuta sauti hiyo yenye makosa, ni toba. Ni Mungu pekee awezaye kufuta. La sivyo itaendelea tu hadi ikutane nawe katika umilele. Hivyo basi, Mungu alivyo mkamilifu na sauti Yake ya Milele, Sauti Yake Mwenyewe itapasa ije kusikika tena. Kwa hiyo lazima awe mkamilifu katika kila uamuzi anaoufanya. Kwani pindi asemapo jambo, itapasa lisafiri na lirejee hadi mwisho lifikie ile siku ya hukumu.

25 Sasa kama wewe utakuwa wa kuelewa kihalisi, au ujaribuye kuelewa, utaweza kuona sababu ya mimi kuchukua msimamo huu nilio nao juu ya Neno la Mungu, kwani vitu vingine vyote lazima vitaangamia, Mungu ni wa Milele na Neno Lake ni la Milele. Sasa unapojifunza, na nitajaribu kuelezea kwa kirefu kadiri niwezavyo, ili mweze kuyapata maneno hayo; nami nafanya hivyo kwa ajili ya kurekodi kanda pia - ili mpate kujua Biblia ni Neno la Munngu.

26 Sasa tunajua kuwa tunaifikia hukumu, kwamba Sauti ya Mungu inakwenda

kutukamatia mahali fulani, kwani ilisema ili kila mwenye mwili asikie. Wahudumu wanawajibika kuichukua, na kama Sauti hii ya Mungu inapasa imkabili kila mtu, basi tuna … unalazimika kuisikia ama hapa ama hukumuni. Kwa hiyo kama kanisa lina sauti ya Mungu, basi itabidi uisikie sauti ya Kanisa kama wenzetu Katoliki ya Kirumi wanavyotuambia. Na wakati wao wenyewe wamechanganyikiwa vibaya katika mafundisho yao (Katoliki ya Kirumi, ya Ugiriki na aina nyinginezo), basi hakuna popote unapoweza kupaamini, kwani ni lipi ndilo Kanisa?

27 Je, ni kanisa la Kirumi lililo sahihi au ni la Kigiriki lililo sahihi, au ni lipi miongoni mwa hayo mengine lililo sahihi? Je, Lutheran iko sahihi? Wababtisti? Wamethodist ni sahihi? Wapresibitariani wako sahihi? Au ni lipi lililo sahihi wakati yote yametofautiana kiasi hicho? Moja liko mbali na mwenzake kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, bali kwa maoni yangu, Neno la Mungu ndiyo Jaji. Kwa hiyo sauti ya Mungu ni kamilifu mno, na inapasa itokee katika chanzo kilicho kikamilifu, na kama mtu akilileta katika njia moja na mwingine nyingine wakiwa na tofauti za madhehebu, basi hatuna njia ya kusimamisha imani zetu kwa uhakika katika hayo wanayoyasema.

28 Natumaini hayo yamekuwa dhahiri, unaona, kwa sababu kama mmoja anasema ni hivi, … Mmoja anasema ni lazima ujiunge na kanisa hili. Ni hili tu lenye wokovu. Huo ni mtindo wa Katoliki. Walutheri nao wanakuja na kudai kuwa wao ndio njia. Hapa wanakuja Wamethodisti wakiwa na kitu kingine, Wababtisti wakiwa na kitu kingine, Wapentekoste na kitu kingine, ndipo panaonekana mkusanyiko wa machafuko namna hii. Basi uchukuapo Neno hili lililoandikwa ukawapelekea ndugu zetu, wengi wao husema, " Vema, hizi sio zile siku". Mwingine anasema, " hii ni historia tu." Yule mwingine anasema, "Hiki ni kitabu cha mashariki tu". Mwingine anasema, "Kanisa lina haki ya kulifanyia mabadiliko". Sasa tunasimama wapi? Ni mahali gani imani itakapotia nanga?

29 Wakati Mungu aliye wa milele … Naamini kama itapasa tuhukumiwe (na daima tutapasa) … Kama tutapasa kuhukumiwa na chochote, itapasa kiwe ni Neno la Mungu ndilo lililoagizwa; Na kama itapasa tuhukumiwe na lile Neno, basi Mungu angelikuwa na hatia kwa kuweka machafuko makubwa namna hii duniani, na akili za mwanadamu zilizo ndogo hivi kukabiliwa na fumbo gumu namna hii, na hajui cha kufanya; mwingine atajiunga na hili, na lile.. Basi jamaa anajitahidi akifikiri kuwa anajaribu kupata mahali palipo sahihi, atalisikiliza dhehebu lingine, na hili linaelekea kuwa bora kuliko lile; atakwenda huko na hatimaye atajikuta amerudia lile la kwanza tena. Basi hajui tu la kufanya. Lakini kama kuna kitu Mungu atakachohukumia ulimwengu, kitakuwa ni Neno Lake. Mimi ninaamini hivyo.

30 Na sasa, ndugu zangu - sasa nisemapo hivyo, ninamaanisha sio tu hili kundi dogo hapa asubuhi hii, bali namaanisha kote ambako kanda hizi zitafika kote duniani - ningependelea mnivumilie kidogo mkiliwazia hilo, kuwa patakuwapo mahali fulani tutakapopaendea ili kuhukumiwa. Ndipo wengine wanasema, "Ni Biblia chapa ya King James" au chapa nyingine, na sasa wanatengeneza chapa ya standadi au kitu kingine.

31 Ninaamini kama Mungu ndiye Mungu mwenye uwezo (na ndivyi Alivyo) Yeye aliye wa Milele, ni sharti alishughulikie hilo, ni juu Yake. Kama ninataka kwenda mbinguni Makaoni Mwake, ni juu Yake Yeye anipe pahali ambapo mimi nitajua la kufanya - pahali ambapo nitaweka mkono wangu na kusema, "Hapa ndipo penyewe". Unakubalina na hilo? Panapasa kuwapo … Ni juu yake. La sivyo angalikuwa na hatia.

32 Kama ningesema, "Bwana, mimi nilikuwa Mlutheri" na mwingine aseme, "Vema mimi nilikuwa Mkatoliki", vyema, hapo wapo wawili wanaopingana. Sasa huyu jamaa atafanya nini? Na kama kanisa Katoliki likiwa ndiyo sahihi? - Ndipo Walutheri wote watakuwa wamepotea. Na kama Walutheri wako sahihi? Basi Wakatoliki wote watakuwa wamepotea.

40

Unaona, lazima pawepo mahali imani itajituliza. Na kwangu mimi - sijui wewe utajisikiaje juu ya hilo, lakini kwangu mimi Biblia ndilo Neno la Mungu lisilo na dosari. Na ninaamini Mungu amelisimamia Neno Lake kuhakikisha hakuna hata yodi moja yenye hitilafu.

33 Binti yangu pale nyuma, Rebeka alikuwa anasema, Baba, kule shuleni tulithibitisha kuwa ulimwengu huu umekuwepo miaka mamilioni na mamilioni, je hiyo haipingani na Biblia?

"Hapana bwana", nikasema, haipingani

"Vyema", nikasema, kama utafiti kuhusu miamba, maumbile ya uso wa nchi na mapango makuu yanayoendelea kuumbika kwa kudondosha chokaa na kadhalika ikithibitika kuwa chokaa imeendelea kudondoka miaka mamilioni, na Mungu alisema Aliumba mbingu na nchi kwa masaa ishirini na manne, je hiyo haikosoi Biblia?

Nikamwambia, "Hapana". Kama ukiona Mungu anavyomwambia Musa juu ya Biblia, Alisema, "Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi" - Kipindi. Kwamba ilichukua muda gani, hapo sisi hatuhusiki. Ndipo anaendelea na kuanza kuelezea wakati wa kupanda mbegu ardhini. Lakini hapo mwanzo - inawezekana ikawa mamia ya mabilioni ya matrilioni ya miaka, karne za miaka isiyoweza kuhesabika, lakini Mungu aliumba mbingu na nchi, kipindi! Hapo tatizo linakwisha. Hilo ndilo la kwanza. Unaona? Yeye hakosei. Paulo yule mhubiri mkuu alisema … alimwambia Timotheo "ajifunze kujithibitisha mwenyewe akilitumia ipasavyo Neno la Mungu". Jifunze Neno kwa moyo mweupe ulio wazi, na ndicho ninachojitahidi kukifanya.

34 Sasa, nilivyo na imani ndani ya Neno hivyo, siwezi kuchukuliana na fasii fulani waliojifanyia, kwani Biblia inasema kuwa Biblia haifasiriwi kama apendavyo mtu fulani. Sasa ni Roho aliyetudhihirishia hilo kitambo kidogo kilichopita. Najua Andiko hilo, lakini sikumbuki sasa hivi mahali lilipoandikwa katika Maandiko, lakini ninyi mnaoandika haya mtakwenda kutafuta na kupata. Natumaini ni katika 2Petro 1:20 kwamba Biblia haifasiriwi kama apendavyo mtu fulani tu.

Kwa hiyo kama mwandishi aliyevuviwa na Roho Mtakatifu alisema … na kama hilo ni kosa, basi ni kwa kiasi gani sehemu nyingine zake zilivyo makosa? Kama ni hivyo, basi ama Maandiko yote ni makosa ama yote ni sahihi. Haiwezekani iwe vinginevyo. Kwa hiyo u … "Vyema kuhusu Kanisa" … "unasema, vyema basi Kanisa, sasa ni kanisa gani lililo sahihi? Ni kanisa gani lililo sahihi? Unaona, inapasa urejee tena mahali ambapo imani itajituliza, na kwangu mimi ni katika Neno la Mungu nikiamini kuwa Biblia ndio mpango wa Mungu kwa watu - ndivyo imekuwa siku zote.

35 Yesu alisema Maandiko sharti yatimie. Hiyo ni kwamba, kama yote yaliyoandikwa katika Maandiko - (sasa mzingatie hili kwani ninyi mnaopata hizi kanda sasa, mwishoni mwa kanda hizi mtaona kuwa nitayarudia tena haya) kwamba yote yaliyo katika Maandiko sharti yatimie. Sasa hebu - hebu ninyi darasa, hilo lizame kidogo. Unaona? Yote yaliyo katika Maandiko sharti yatimie. Sasa kama Mungu alisema chochote - zingatia sasa! Sharti litimie. La sivyo halikuwa Neno la Mungu. Na kama si Neno la Mungu, sasa tupo wapi? Hebu tupate kitu kinachofanana na Mungu au chochote tunachotaka kufanya. Kama Biblia ilivyosema, "Tule, tunywe na tufurahi kwani kesho tunakufa". Unaona?

36 Sasa kama hilo si Neno la Mungu, basi sote tumepotea, na kama ni Neno la Mungu, Mungu ni sharti apewe heshima. Yule Mungu wa … Yeye aliye chemchemi ya heshima yote, Yeye aliye Mwanzo wa heshima yote, Yeye aliye chanzo cha Kweli yote, sharti asimamie lile alilolisema! Na kama hili si Neno la Mungu, sasa Mungu ni nani? Mungu yuko wapi? Au hata kuna Mungu?

37 Lo useme, "Ndugu Branham , najisikia:. Lo, hata makafiri wataweza kukuambia hivyo hivyo kuhusu ibada zao za sanamu.

Kusafiri kunatusaidia, wakati unapojionea mambo haya mwenyewe.

Kwa hiyo ni … Naamini ningeweza kutazama na kuona haya. Ndiyo.

Naamini kama ni … Naamini kwa sababu nilibadilishwa namna hii, kwa sababu …

Ninafanya hivyo pia, lakini kumbuka makafiri hufanya hivyo hivyo. Kwa nini maadili ya Afrika ni mengi … Baadhi ya makabila kule yatawafanya Wamarekani wanaojiita Wakristo wajionee aibu - maadili na usafi ulioko miongoni mwa watu wanaoabudu sanamu za kipagani. Labda hiyo ndiyo Mungu. Unaona ninachomaanisha? Unaona, unapoyaangalia mambo usoni, unapaswa kuufunika mviringo mkubwa, unapaswa uwe na pahali utakapoparudia na kuweka mikono yako.

38 Sasa hebu tuyazungumzie madai ya Walutheri, yanashindwa! Tuyachukue madai ya Wakatoliki, yanashindwa! Tuyachukue madai ya Wabaptisti, Wapentekoste, yanashindwa! Kwani huwezi ukayawekea matumaini. Lakini hakunachochote kilichoandikwa katika Biblia hii ambacho Mungu hajakithibitisha kwa kumtumia mtu

fulani, kuwa ni cha Kweli. Hiyo ni Kweli.

Kama ambavyo nimesema mara kwa mara, “labda imani yangu haitaweza kupanda juu kufikia Henoko alipofikia, lakini sipendi kuwa kikwazo kwa mtu yeyote ambaye angeweza kupanda kiwango hicho”. Imani kuu. Sasa baada ya kupata msingi huu yaani kwa nini ninaamini Biblia, na ndipo ninapochukua somo langu.

39 Sasa kitu kingine nataka kusema ni kwamba Biblia haijipingi yenyewe, na nimetoa changamoto duniani kote anayeona Biblia inapopingana aje kwangu anithibitishie. Njoo unithibitishie. Biblia haijipingi. Ni wewe unayeipinga Biblia. Mungu hawezi kujipinga Mwenyewe. Kama akijipinga Mwenyewe, basi Yeye si Mungu. Na kama Neno hili ni Mungu basi … na linajipinga, basi unamfanya Mungu anajipinga Mwenyewe, sasa Mungu wako yuko wapi? Hapo jambo hili linavimba, au sivyo? - ni gumu.

40 Kama Mungu alijipinga Mwenyewe Yeye anakuwa kama mimi tu au kama wewe tu, kwani hawezi kujipinga Mwenyewe. Neno lipo pale, lakini limefichwa machoni pa wenye hekima na busara.

Ndiyo sababu mmoja alisema Mathayo 28:19 pale, “Enendeni mkawafundishe mataifa mkiwabatiza kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu”, Matendo 2:38 Tubuni mkabatizwe kwa jina lake Yesu‟ - ”Kuna kupishana‟. Hakuna kupishana!

41 Kila mtu aliyebatizwa yapasa abatizwe katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Na kama hujabatizwa ukitumia jina lake Yesu Kristo, hujabatizwa katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Umebatizwa katika sifa za jina. Kama hiyo ni … Kama huo si ufunuo wa kweli, basi Biblia ingekuwa na makosa kwa kuendeleza hilo na kila mtu akabatizwa katika jina lake Yesu Kristo. Lakini kama Biblia ilibatiza … Kila mmoja miongoni mwa mitume moja kwa moja katika kizazi chote walibatiza katika jina lake Yesu Kristo baada ya Yesu kuwaamuru wabatize katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, basi Biblia ingekuwa inajipinga. Lakini kama ukiliangalia utaona haijipingi. Wao walifanya kila tu alichosema. Si vyeo bali jina. Kwa hiyo hakuna kujipinga.

42 Sijui ni mambo mangapi nitaweza kuyavuta juu hapa kwenye somo ambayo niliyaandika ili nilete kwenu, ambayo watu husema kuna kujipinga katika Biblia. Kwa miaka ishirini na tano (karibu thelathini sasa) nimeita ajitokeze mtu atakayenionyesha Biblia inapojipinga. Sijaona. Hapana bwana! Kweli ipo pale, Kweli yote, Kweli tu na wala si kingine, na imani yetu imetia nanga hapo hapo - hapo penye kile alichokisema Mungu. Usijaribu kukifasiri, soma tu kilivyosemwa. Usiweke fasii yako upendavyo wewe, na naamini hakuna kitu kingine zaidi.

43 Sasa natumaini kama hili linaumiza huyo hakuwa mimi; ninajaribu kusema kwa nini naamini hiki ninachoamini, na jinsi nilivyotenda - juu ya mambo yale niliyotenda. Ninajaribu kujionyesha kwa ulimwengu, kwamba nimefanya haya kwa kuwa ndivyo nilivyoshawishika.

Ninaamini kwamba neno lolote linaloongezwa katika Biblia hii, na yeyote aliye na hatia ya kuongeza, sehemu yake itaondolewa katika Kitabu cha Uzima - Ufunuo 21. “Yeyote atakayeongeza au kupunguza kutoka katika Hii” … Siamini kuwa mapokeo yeyote, mafundisho ya dini, chochote kile, isipokuwa Neno la Mungu lenyewe, ndilo tu mpango wa Mungu. Kinginecho chote ni dhambi, kitashughulikiwa na kitapotea milele - mtu yeyote, mapokeo yoyote, dhehebu lolote na chochote kitakachoongeza au kupunguza kutoka katika tamshi lolote la Neno hili. Mungu ambaye si Mungu wa jana ambaye aliandika kitabu na kukikabidhi mikononi mwa kundi fulani la watu na kuwaachia wavuruge na kufanya lolote lile halafu akahukumu tena ulimwengu na kitabu hicho! Lakini Mungu aliyekiandika Yu hai. - Anaishi ndani Yake na kuthibitisha Neno Lake. (Sasa ninyi mnaojifunza kwa kanda, nataka mjifunze kwa makini sana hapo - hicho nilichosema sasa hivi, unaona?)

44 Sasa nimeanza Mwanzo na nimefika hadi Ufunuo sasa nikiyaleta yote pamoja kuwa hili ni Neno la Mungu. Ufunuo inasema kuwa yeyote atakayetpunguza au kuongeza, yeye sehemu yake itaondolewa kutoka Kitabu cha Uzima. Baada ya muda nitalifikia na kulinukuu hilo Andiko. Ufunuo mlango wa mwisho.

Hiyo ndiyo sura ya kwanza inayoonsyesha sasa, nini? Neno ni nini? - Sasa ni la Milele. Halipasi kuvurugwa - Mungu amesimamia hilo. Halipaswi kuongezwa - chochote juu yake. Chochote hakiondolewi kwalo maana ni la Milele. Unaona? Sasa kujenga

msingi juu yake ili kukuonyesha hilo, yaani kile ninachojaribu kusema kiko kati ya (Mwanzo na Ufunuo haitachanganyika na chochote kingine).

45 Sasa hapo ndipo tunakwenda kutofautisha - toka hapa hadi saa kumi na moja mchana huu. Unaona? Hapa ndipo tutatofautiana. Ni wangapi wanaokubali hichi ndicho Kitabu cha Mungu cha Hukumu, kuwa tutahukumiwa kufuatana na Neno la Mungu? Halitaongezwa wala kupunguzwa. Sasa ni kwa nini imefanyika hivi? Sasa tunakaribia kuliona hilo. Ni kwa nini hili limetendwa kikatili hivi? Sasa tunakwenda kulipata hili kati ya Mwanzo na Ufunuo, lilipitia nyakati nyingine hadi kufikia wakati wetu.

46 Sasa ninapenda kulielezea liwe wazi kwa ajili ya kanda. Sasa baada ya kuwaeleza kwa nini ninaamini Neno, na jinsi lisivyoweza kuongezwa au kupunguzwa, nataka kuingia katika kina chake kupata maelezo ya somo hili refu ambalo nimeshalichora ubaoni ili niwaeleze na kuwaonyesha mambo yalivyotokea, ndipo utaweza kuona sababu nikaamini jinsi ninavyoamini.

Unaona?

47 Sasa haliwezi kuchanganywa, na haliwezi kuchanganya mbegu na chochote kile. Halitachanganya mbegu. Siku ya leo ni maarufu kwa uchanganyaji mbegu za wanyama, mahindi, ngano, ili kufanya mazao yawe mazuri zaidi. Lakini haifai. Imeoza, haina uzima ndani yake - hufa, haiwezi kuzaa uzao wa jinsi yake, imekufa - kwani kila kitu tulicho nacho duniani leo kilicho katika maumbile yake ya asili ni Neno la Mungu lililonenwa!

48 Ndiyo sababu nyumbu ambaye ni haramu aliyetokana na mbegu mchanganyiko hawezi kuendeleza uzao wake tena. Mungu alimfanya farasi na akamfanya nyumbu, au alimfanya punda. Unapochanganya mbegu zao unampata nyumbu. Huo ni uzao mchanganyiko, kwa hiyo hawezi kuendeleza uzao wake. (Tunakwenda kugonga swala la uzao wa nyoka punde si punde sasa). Hawezi kundeleza uzao wake.

49 Sasa somo langu ni nini? -Neno lililonenwa ndiyo mbegu ya asili. Sasa ninapenda kuthibitisha hilo. Tufungue sasa Mathayo 24:35 mara moja na tunapoendelea kuchambua Maandiko haya kwa kitambo kidogo (Na nitaangalia kama tuna muda kiasi gani), ndipo nitapenda kusoma hapa neno ambalo Yesu alisema. Mathayo 24 na mstari 35 - sura ya 24, aya ya 35 kuonyesha jinsi Neno hili lilivyo la Milele (haya ambayo tumekuwa tukiongea habari zake).

Amini (34) amini nawaambia, Kizazi hiki hakitapita, hata haya yote yatakapotimia. Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.

50 Sasa, je ungeweza kuchanganya chochote na hilo basi! Sasa katika Kitabu cha Ufunuo mlango wa 22 na aya ya 19, ningependa kupasoma. Ufunuo mlango wa 22 aya ya 19 na tuone Anachosema. Tuanzie aya ya 18.

Namshuhudia kila mtu (sasa kumbuka kutoka Mwanzo ambapo Alisema Neno, unaona!) Namshuhudia kila mtu …(hapo ni padri, papa, askofu, kasisi mkuu au yeyote) … ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu yeyote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki.

Je vipi kuhusu kanuni zenu za imani mlizojitungia? Je vipi kuhusu maungamo yenu ya imani ambayo hayana msingi katika Maandiko, ambayo mnayasikiliza? Maungamo ya madhehebu yote, hakuna hata moja lisilohusika na haya.

Na mtu yeyote akiondoa lolote katika maneno … (akisema si sawa, unajua, unaona?) ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika mji ule mtakatifu ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.

51 Hata kama akiwa mhubiri (unaona) hata kama akiwa ni mshirika wa kanisa maisha yake yote, hata awe askofu au papa, yeyote atakayeondoa neno moja katika hili - neno moja tu! Unafahamu kuwa ni neno moja ambalo Hawa alilionea mashaka ndicho kilichosababisha matatizo yote haya? Neno moja la Mungu lililonenwa, Hawa alilionea mashaka kama ndiyo ile Kweli, na ikasababisha kila kuugua, kila ugonjwa, kila kuumwa kwa mtoto, ikasababisha kujengwa kwa kila hospitali, kila upasuaji wa hospitalini uliowahi kufanywa, kila kifo kilichowahi kutokea - kwa mtu mmoja kuamini moja - kutokuamini neno moja. Hilo ni lako sasa.

52 Hawa alijaribu kufanya nini? - alichanganya mbegu, alichanganya na kitu fulani. Inakupasa kulichukulia jinsi ile ile Alivyonena Mungu. Neno halichanganywi na chochote. Hapana bwana. Wakati mmoja Yesu alisema, "Kama ungekuwa na imani kama mbegu

ya haradali … nimeambiwa kuwa mbegu ya haradali haiwezekaniki kuchanganywa na mbegu nyingine. Huwezi kuichanganya na chochote. Utaweza kuchanganya nafaka nyingine, lakini huwezi kuichanganyisha mbegu ya haradali, unaona, kwa sababu haichanganyiki. Na kama unayo imani ya namna hiyo, yaani hiyo … ukichukua neno moja la Mungu … hapo ndipo wainjilisti wengi sana wanapopumbazika (tutaliendea hilo baadaye), jinsi wanavyosema ″Aa tunaamini hili‟, na watalichukua lile na wataamini lile neno moja na kuhakikisha linafanya kazi, lakini je, mbona wanalipuuzia neno linalofuata hapo hapo baada ya hilo waliloliamini? ″Ni heri yule atendaye yote anayopaswa‟. (Unaona?) Atakuwa na haki ya kuingia katika Mti wa Uzima, kwani huko nje wako wachawi, mbwa, wazinzi na kadhalika.

53 Sasa hapa nina darasa la watu mchanganyiko, lakini nina maelezo mazito hapa ambayo si kawaida kuyaeleza katika kundi kama hili, kwa hiyo nawahitaji akina dada mwelewe vizuri, unaona, hakikisheni mnaelewa.

Sasa ndiyo sababu tunaliamini - kwamba ni Neno la Mungu, hivyo Neno la Mungu lililonenwa ndilo asili. Na kila kitu kilichoumbwa na Mungu (Mungu alichokitamka kiwepo) ni asili. Na huwezi ukachanganyisha hatimaye baadhi ya maumbile aliyoumba. Ndiyo sababu Hawa alifanya vile alivyofanya juu ya mbegu yake mwenyewe —kwa sababu hakuwepo katika uumbaji wa asili. Yeye ni tunda lililotoka kwa mtu - hakuwa katika ule uumbaji wa mwanzo alioumba Mungu. Mungu ndiye aliyeumba mtu mkamilifu na ndipo akatoa sehemu ya kiumbe chake na kumfanyiza msaidizi.

Ndiyo sababu unaweza kuchanganyisha mbegu ya farasi na punda, lakini huwezi ukaendeleza uzao huo kwa kiumbe hicho cha mchanganyiko. Ni kifo. Lakini kile kiumbe cha asili kina uzima. Kinajizaa tena. Natumaini unaweza kuliona hilo sasa. Kile kiumbe cha asili kina uzima; ndiyo sababu vikundi vya dini, na madhehebu na mashirika ya dini huwa yanakufa. Historia inathibitisha kuwa yote yamekufa. Hayakuwahi kuamka kamwe, na kamwe hayataamka. Hayawezi yakajizaa upya tena. Hayana kitu cha kushirikiana nacho ili kupata uzao, wao ni tasa. Ndiyo sababu watoto wa Hawa wanakufa.

54 Sasa natumia muda wa kutosha kuelezea ili kanda … niwape watu muda wa kujifunza. Sitaki kuwa na haraka yoyote. Nataka niwe na muda wa kutosha. Sijui nini kitatokea kuanzia sasa, lakini nataka watu walipate hili, kuwa hata ijapo siku moja Mungu ataniondoa kutoka ulimwenguni kama sitaishi hadi Arudipo, Ujumbe utaendelea kuwepo. Ni kweli. Dumu katika Neno.

55 Sasa kumbuka, kila Neno la Mungu lililonenwa ndiyo mbegu ya asili. Mungu alipandikiza kila kitu duniani kwa njia ya Neno Lake; na kadiri unavyodumu na mbegu ya asili, ndivyo itakavyojizalisha yenyewe tena na kujiongeza yenyewe tena. Ukichanganyisha mbegu yake na mbegu nyingine, itakufa. Na Hawa, yule mwanamke, ndiye aliyekuwa mchanganyisha mbegu wa kwanza kabisa kabla ya wengine.

Sasa natumaini hamtazima kanda zenu, hadi tuende na somo hili hadi chini kabisa tuyathibitishe haya muda mfupi ujao, unaona? Niwaonyesheni sababu ya haya.

56 Yeye alikuwa mchanganyishaji mbegu, bibi arusi. Tazama, kwa kupitia hayo kukatokea kifo - katika kujaribu kulichukua Neno la Mungu na kuchanganya na hekima fulani. Unaona? Hupaswi kufanya hivyo. Kama unaamini … una hekima ya kulieleza, sema tu. Ni Mungu aliyesema hilo, na hapo umemaliza kazi - kwamba Mungu alisema hivyo, na hakuna kitu kingine zaidi ya hicho. Kama huwezi kueleza hilo, liache lilivyo, lakini useme liko hivyo kwa sababu Mungu alisema hivyo. Unaona? Ndivyo ilivyo, Mungu alisema hivyo.

57 Sasa angalia. Sasa haitachangamana. Mbegu ya Neno inapasa iachwe ilivyo bila kuguswa. Mungu atamwadhibu yule atakayejaribu kuiharibu, na wala haitachangamana na chochote kingine. Hilo ni Neno la Mungu pekee. Mungu hahitaji neno lako lijiunge na Lake. Hatupaswi kunena maneno yetu wenyewe, tunapaswa kuhubiri Neno Lake - Neno la Mungu.

58 Sasa, hivyo basi, uzima wa kweli utaweza kuja au kujizalisha wenyewe kwa njia ya ile mbegu ya asili. Unaona? Uzima … Sasa uwazie … sasa jifunze hilo, sasa, wakati unapojifunza kwa kusikiliza kanda, na ujifunze sasa. Uzima U-zi-m-a utaweza tu kuzalishwa kwa njia ya mbegu ya asili, jinsi ilivyoanza pale mwanzo, ndipo ikajizalisha yenyewe. Kama ikifanyika hivyo, ikiwa mbegu mchanganyiko huwa inatokomea hatimaye. Baadhi yake inaishia katika kizazi cha kwanza, unaona, wakati uo huo. Punde si punde inajikuta imerejea pale pale ilipoanzia bila ya kujiendeleza. Haiwezi kuleta

uzima sahihi kwa kuwa ni mbegu mchanganyiko.

59 Mwanzo 1:11 Biblia ilisema (Mungu alisema), kila mbegu izae kwa jinsi yake". Sasa wakati Mungu aliposema, hiyo ilitosha. "Kila mbegu izae kwa jinsi yake. Kama ukichanganyisha mbegu utapata mazao mengi. Ni zao la hali ya juu la nini? Sikiliza kwa makini sasa. Hebu tuzingatie swala hili kwa mtiririko. Kuchanganya … Ninajitahidi kuwaweka wasikilize, somo kama hili ningeweza kulihubiri. Lakini ninajitahidi kujizuia nisifanye hivyo). Kuchanganya kutasababisha lije zao la hali ya juu kama ambavyo imekwishathibitishwa. Lakini ni zao la aina gani? - zao lisilo halisi, kifo.

Changanyisha mbegu ya mahindi, itakuletea mahindi makubwa zaidi, mazao bora zaidi, yanayopendeza zaidi, lakini yaliyokufa. Hebu pandikiza tena, haiwezi kujizalisha yenyewe tena. Mambo yake yamemalizika, yenyewe imekwisha. Kama Hawa, unaona? Yeye alizaa zao la mbegu mchanganyiko. Hebu tutazame sisi leo. Utaweza kuangalia huko na huko na utathibitisha kuwa hilo ni kweli. Kweli ndivyo ilivyo. Haikuwa kusudi la Mungu, hapana bwana. Hebu tu ujizatiti kwa jambo ambalo nalifikiria sasa hivi, unaona.

60 Kuchanganya kunaleta zao la mbegu mchanganyiko, na zao la mbegu mchanganyiko ni zao lililokufa - kufuatana na mwendelezo wa uzalishaji. Haiwezi ikajizalisha tena, haiwezi kwa sababu Mungu alisema hivyo. Inapaswa izae kwa jinsi yake, lakini wewe umekwishaichanganyisha.

Sasa unaweza ukaliona Kanisa papo hapo, mahali litakapoishia. Linafia pale kwani haliwezi kuzaa kwa jinsi yake. Kwa nini. Lina mbegu mchanganyiko. Huwezi ukafanya lolote na kanisa. Limekufa, limekwisha. Sawa. Ndiyo sababu kila kizazi kina uamsho wake wenyewe - nafasi yake maalum ya kukutana na Neno. Ah Mwenyenzi Mungu pale hukumuni - Kikundi cha John Wesley kitaamka na kusimama, ndipo hawa Wamethodisti wa leo waliozubaa kiroho wataaibika mbele yao. Luther atainuka. Wakatoliki watainuka. Na nyuma ya Irenia, Martin, Polycarp watakuwepo wafuasi watakaohukumiwa kwa kuchanganyisha mbegu ya Neno na kanuni za imani za kidhehebu. Kikundi hiki cha Walutheri kilichofuata uamsho wa Luther nao watahukumiwa kwa ajili ya hayo vile vile. Kikundi cha Wabaptisti waliofuata uamsho wa John Smith nao watahukumiwa vivyo hivyo. Wale wa Alexander Campbell watahukumiwa hivyo vile vile. Na wapentekoste nao watahukumiwa hivyo hivyo. Ule uamsho wa mwanzo wakati Roho Mtakatifu aliposhuka aliwaita watu wa Mungu akijaribu kuwaingizia Neno Lake, na wakatunga taratibu za kidini na kuunda dhehebu na wakafa pale pale.

Utasema, "Lakini angalia kile wanachokifanya.

Tutaliongelea hilo baadaye kidogo Leo. Tunaenda nalo moja kwa moja … Ninajaribu kusia mbegu sasa. Ndipo tutaenda kuwaonyesha punde si punde yale yaliyotokea.

61 Sasa, hiyo ndiyo sababu kila uamsho una uamsho wake wenyewe - kila kizazi kina uamsho wake, na Mungu anajiinulia Mwenyewe mtu, anamtuma na Neno Lake na anamtumikisha aupeleke ujumbe kwa ajili ya kizazi hicho. Na pindi tu yule mtu atakapoondolewa baada ya kipindi chake kwisha, mtu mwingine anaudaka huo ujumbe na kuuchanganyisha mbegu na inaangukia nyuma kwenye kila kitu … kikamilifu … inaweza …

Ningeweza kusimama hapa kwa dakika. Hatuko katika haraka, rejea, hivyo ndivyo kabisa mambo yalivyoanza kule Mwanzo. Mungu alianzisha zao Lake la taifa la wanadamu na Hawa akalichanganyisha mbegu. Unaona kilichotendeka? Hivyo, hiyo ndiyo hukumu ya Hawa.

62 Luther aliweka - wengine wote - Kristo aliweka. Mitume waliweka manabii waliweka. Je, Yesu hakusema, "Ni yupi katika manabii Mungu aliowatuma kwenu ambaye baba zenu hawakumtesa?"

Je Yesu hakufundisha kuwa mfalme mmoja wakati fulani alimtuma mtumwa wake, na hatimaye akamtuma mwingine, na akamtuma mtumwa mwingine, na kadhalika na hatimaye akamtuma mwanaye, unaona? Kila kizazi kikipokea … kwa sababu ni yale ya Adamu na Hawa yanayojirudia tena - zao lile la kwanza katika Bustani ya Edeni. Nusu yao walipotea - wanawali wenye busara, wanawali waliolala, nusu yao … Mmoja alitunza Neno, mwingine alilichanganyisha mbegu. Ukienda mbele na nyuma haraka uwezavyo, moja kwa moja, ndivyo ambavyo imekuwa katika vizazi vyote. Tutathibitisha hayo kwa kutumia Neno la Mungu na kwa kutumia historia hapa. Hiyo ni sawa - uchanganyishaji mbegu.

63 Uchanganyishaji mbegu ulianzia kwanza Edeni, katika Kitabu cha Mwanzo. Ni ule Mwanzo. Ndipo pale … na inaishia hapa katika Ufunuo. Hiyo ndiyo kurudi mara ya pili kwa Kristo. Sasa kumbukeni kwa usahihi. Ndiyo sababu kila kizazi kina uamsho wake chenyewe; kinapata nafasi yake katika Neno. Ndipo wanachanganyisha mbegu - badala ya kulichukua na kuendelea nalo, wanakwenda mahali pengine.

64 Utume wangu, na ninaamini Mungu ameniitia hilo … Itanipasa leo niseme mambo fulani ya kibinafsi leo, kwa sababu ndivyo nilivyowaambia ningefanya, unaona? Na kuuambia ulimwengu. Utume wangu kwa dunia, naamini, ni nini? Ni kuandaa njia mbele ya Neno Ajaye, unaona? Neno Ajaye ambaye ni Kristo. Na Kristo ndani Yake anao Utawala wa miaka elfu moja na anacho kila kitu pale pale kwa sababu Yeye Ndiye Neno. Unaona?

65 Sawa Yesu alisema katika Yohana 3:5. Tunalifahamu hapa hapa. Nitafungua, mtu fulani asikilizaye kanda ange … labda asingeweza kufungua na kupapata wakati uo huo, na nitasoma hapa Mtakatifu Yohana sura ya 3 na aya ya 5, na tutaona kile Yesu alichosema. Tungeweza kuanzia nyuma kidogo kabla ya hapo - mstari wa tatu.

Yesu akajibu akamwambia, Amin amin, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.

Nikodemo akamwambia, awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?

Yesu akajibu, Amin Amin nakuambia mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu.

66 Je hiyo ni mbegu? Kila Neno la Mungu lililonenwa ni Mbegu. Hiyo ni sawa. Ninakwenda kuthibitisha hilo katika muda mfupi - mahali Yesu aliposema hivyo. Kila Neno la Mungu lililonenwa ni Mbegu. Ndipo utarajie mtu azaliwe tena - kwa nini azaliwe tena? Yeye yu mfu akiwa katika huo mwili. Yeye ni mbegu mchanganyiko. Inapasa azaliwe mara ya pili. Kwa nini? Alizaliwa dhambini kutokana na dhambi ya Hawa, akatungwa mimba hatiani, akaja duniani akisema uongo. Yeye ni mwongo kimsingi.

Hata kama awe ni mwerevu namna gani, msomi namna gani, au chochote kile alicho, bado yeye ni mwongo - Biblia inasema ndivyo alivyo - wazazi wake wawe watakatifu kiasi gani au lolote linalohusu hayo, bado kimsingi ni mwongo. Na njia pekee ya yeye kusema ile Kweli, ni kusema Kweli ni nini kwa midomo yake mwenyewe. Ndiyo njia peke yake ambayo Kweli yaweza kupitia. Chochote kilicho kinyume cha lile Neno, bado yeye ni mwongo.

Hilo ni uwazi mno, lakini ndicho Mungu alichosema, "Neno la mwanadamu liwe uongo na Langu liwe kweli". Unaona? Chochote kilicho kinyume au kinachokataa Neno hili au kulisukumia taifa fulani au kizazi kingine, au chochote kile, yeye ni mwongo. Hilo ni sawa kabisa. Inapasa azaliwe mara ya pili ndipo aweze kuliona kila Neno. Njia pekee awezayo kuzaliwa mara ya pili ni kwa Ule Uzima wa Mungu ndani yake ujizalishe ule - Uzima.

67 Mbegu sharti iwe na maji ndipo iote. Sasa uweke mbegu ardhini na kama hakuna unyevunyevu ardhini, ni vumbi. Haiwezi kuota vumbini. Haiwezi. Inapasa iwe na asilimia fulani ya unyevunyevu, la sivyo haitaota. Je, hilo ni sawa? Andiko huua, bali Roho hutupa Uzima. Unaona? Sasa lazima iwe na unyevunyevu ndipo iote.

Neno Lake ndilo mbegu. Sasa ili kuthibitisha hilo, hebu tufungue Luka mlango wa 11 … au mlango wa 8, samahani, na mstari wa 11. Sasa Anaendelea mbele na kuanza kueleza. Kuna mengi ya kusema kuhusu hilo. Hebu tuanze aya ya 4 tusome.

Mkutano mkuu ulipokutanika, na wale waliotoka kila mji wakimjia, alisema nao kwa mfano.

Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake; naye alipokuwa akizipanda, nyingine zilianguka karibu na njia, zikakanyagwa, ndege wa angani wakazila.

Nyingine zikaanguka penye mwamba, zilipoanza kumea zikakauka kwa kukosa rutuba.

68 Unyevunyevu - Wabaptisti, Wapresbiterian, Walutheri hawana maji. Na wakati anapookolewa mara ya kwanza, anamkazia Kristo macho, anaamini. Na unajua, jambo la kwanza dhehebu linamfungia mahali na unyevunyevu wa Roho unamtoka na anakuwa mdhehebu, mfu. Sio tu Wabaptisti, hata Wapentekoste pia. Hawaamini hilo - Najua

wengi kati yenu hawaamini hilo, lakini hebu ngoja kidogo tu. Tutaona kama Biblia inatamka hayo au la.

69 Vema, kukosekana kwa unyevunyevu - neno la mwisho katika mstari wa 6 mlango wa 8. Ukosefu wa unyevunyevu.

Nyingine zikaanguka kati ya miiba, na miiba ikamea pamoja nazo ikazisonga,

Unaona, hiyo ilikuwa nini? Anaendelea na kuwaambia kuwa baadhi punde baada ya kuwa … Leo sitatupa ngumi yoyote hewani. Kitu ninachofikiria tu hawa wafanya biashara wa Kikristo na wengine wote wa haya mashirika ya Kipentekoste na hawa watu wanojenga haya majengo makubwa yanayogharimu dola mamilioni ya vitu - utajiri wa ulimwengu umesonga hadi utukufu wa Roho wa Mungu ametoka nje yao. Wamekufa kwa sababu ya kusongwa. Ulimwengu, masumbufu ya ulimwengu yamesonga hadi utukufu wa Roho wa Mungu umetoka.

70 Wanawake wanataka kuwa kimbelembele na kupunguza nywele zao pembeni na kukata nywele kwa kupunguza utosini, wanavaa nguo fupi na kuonekana kama ulimwengu ulivyo. Wahubiri wanasimama mimbarani, wakiwa … wanajizoeza kusema amina na wakiogopa lile Neno la Mungu wasije wakapoteza tikiti ya mwaliko wa karamu za vyakula. Kama hawatakuwa na gari zuri kama Cadillac, basi wanaonekana kama si watu wa kiroho tena. Hiyo ni sawa. Kama hawatamudu kuvaa nguo nzuri sana na hata vitu vingine wanaonekana kama waliorudi nyuma kiroho. Wao si akina fulani na fulani.

100

Mzee mmoja nyuma huko, mzee Ndugu Kidd, aliniambia asubuhi hii kwamba hawamtaki tena, eti kwa sababu amezeeka na anasimama kwa usahii na Neno. Kuna nini? - Hawana unyevunyevu. Hiyo ni sawa.

Nyingine zikaanguka penye udongo mzuri, zikamea, zikazaa moja kwa mia. Na alipokuwa akinena hayo, alipaza sauti akisema, "Mwenye masikio ya kusikilia na asikie.

Aaa ni mfano mkuu hivi! Ningependa mno kulifanya liwe somo katika mahubiri yangu. "Wakati alipokuwa akinena hayo …" Mlango wa 8, aya ya 8 na mlango wa 8.

Nyingine zikaanguka kwenye udongo mzuri, zikamea, zikazaa moja kwa mia. Alipokuwa akinena hayo, alipaza sauti akisema … (alipaza sauti, jambo fulani labda kama hili aliposema, "Lete moja kwa mia. Yeye aliye na masikio na asikie". Kwa maneno mengine kama sikio lako limeelekezwa kwa Mungu, hebu na asikie, unaona).

Wanafunzi wake wakamwambia, Maana yake nini mfano huu?

Akasema, Ninyi mmepewa kuzijua siri za ufalme wa … (siri - unaona anachokiongelea hapa? Sasa tazama. Siri za ufalme ni nini? Tazama kwa dakika moja tu.) … siri za ufalme wa Mungu; bali wengine kwa mfano, ili wakiona wasione, na wakisikia wasielewe. (Unaona, lakini Neno la Mungu hushuka kwenye hukumu ili liwahukumu - kwa sababu waliliona! Lilikuwa pale).

Na huo mfano, maana yake ni hii; Mbegu ni Neno la Mungu.

71 Mbegu ya Uzima ni nini? - Neno la Mungu! Kwa hiyo, kwa ajili ya Uzima, huwezi kuja kwa kupitia ungamo la dini, huwezi kuja kwa kupitia dhehebu, yakupasa kurudi kwenye Neno! Sasa, ile mbegu ya Uzima!

Vema, Neno Lake ni Mbegu Yake, na Roho Wake ni yale Maji. Sasa ,turudi nyuma kwa Yohana 3:14 pale, unalipata tena, unaona. Unaona? Yule Roho ni Maji.

Sasa tazama, Yohana 3:14 , tunaelewa kile linachomaanisha kama unataka kulisoma.

Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa;

Unaona? Sasa ikiwa Musa alimwinua yule nyoka wa shaba, kwa kusudi lile lile Kristo aliinuliwa, sasa ni kitu gani? Musa alimwinua nyoka wa shaba ili kwamba wale watu waliokuwa wakiangamia waweze kupata maji kwa ajili ya uzima. Na tazama, Yesu … (Lo Mungu!) Yesu ni Neno la Mungu. Sasa tunakwenda kuligonga hilo lizame ndani mchana huu, unaona, kuhakikisha hilo.

72 Yesu ni Neno la Mungu, na Yeye kama mbegu Aliweza kupasuka kufungulia, ule Uzima, ule Uzima ulio ndani ya Mbegu, kwamba huu Uzima, ambao, ni Roho, Maji

yakitiririka juu ya … Roho juu ya Mbegu ya Mungu italeta uzima wa ile Mbegu. Na ikiwa utaleta kitu kingine, kuna aina nyingine ya mbegu pale basi! Amina! Unaelewa?

Ikiwa Roho wa Mungu atakuja kuimwagilia Mbegu maji, kama hiyo anayoimwagilia maji ni Mbegu, itazaa Uzima wa ile Mbegu. Imeeleweka? Itazaa Uzima wa ile Mbegu, kwani huo ndio iliyopewa.

73 Naamini Biblia ni Neno, Kweli yote, na Yesu ni Neno lililodhihirishwa; Yeye na Neno Lake ni Mmmoja na kitu kile kile. Yeye alikuwa nini? Sasa tazama. Yeye alikuwa ile Mbegu.

(Sasa, yanipasa niache jambo fulani ili niweze kulitoa hapa jioni hii, unaona. Ni vigumu.)

Yeye alikuwa ile Mbegu ambayo Hawa angezaa. Unalielewa! Yeye alikuwa ile Mbegu ambayo Hawa alikuwa aizae, lakini aliichanganya kwa kutokuamini Neno la Mungu. Kwa hiyo Yeye alikuwa ile Mbegu, na njia pekee ule Uzima ungekuwa, katika kuzaa Uzima, Uzima ingebidi uje kupitia ile Mbegu, na ingepasa ile Mbegu ife ili iweze kusambaza Uzima! Je, huwezi kuliona? Hiyo ndiyo sababu yale Maji yalitolewa - kunyeshea ile Mbegu!

74 Roho Mtakatifu aliyekuwa katika Bustani ya Edeni alikuwa ainyeshee ile Mbegu. Mwanadamu hakuumbwa ili afe; aliumbwa ili aishi, lakini kuchanganya mbegu kulileta uzima … au namaanisha kifo. Hawa alichanganya mbegu. Sasa unakataa uzao wa nyoka. Basi nitakuuliza, "Hizi ibada za mazishi ni kwa ajili gani?" Hawa alichanganya mbegu. Kila mmoja wetu ni mbegu mchanganyiko mbali na ile ya asili. Hiyo ndiyo sababu unakuwa katika hatua za kufa wakati wote. Lakini (Ee Mungu!) kuna chembechembe ya uzima itokayo kwenye Mbegu halisi, ambayo Mungu alihakikisha ilikuwa Mbegu Yake; Alimfufua Yeye tena! Unaona? Kuwa kwa njia ya ule Uzima uliokuwa unakuja juu ya ile Mbegu ya asili, kama alivyopewa Hawa, unakuja juu ya Kanisa Lake halisi, unaleta Uzima tena kwa njia ya uzao, kupitia tumbo la uzazi, la Bibi Arusi Wake. Unaona?

Ee, jambo hili ni tukufu na kina kirefu. Nitaendelea kwa muda kidogo zaidi ili lizame ndani.

Yeye ni ile Mbegu. Yeye ni ile Mbegu ambayo ilizaliwa na Neno la Mungu. "Na iwe kwangu kama ulivyosema." Hiyo ndiyo Mbegu. Unaona?

Kupokea Neno, unaona?

75 Sasa, Yesu ni Neno lililodhihirishwa. Yeye na Neno ni Mmoja na kitu kile kile, na hiyo ndiyo sababu lilikuwa hivyo … lilidhihirishwa ndani Yake kikamilifu. Hiyo ndiyo sababu Mungu alijidhihirisha Mwenyewe kikamilifu katika Yesu: kwa sababu Yeye alikuwa Neno Mbegu, uhai wa Neno Lenyewe (ule uhai ulio ndani ya mbegu, ambao ni uzima katika ile mbegu). Unalielewa? Unaona, ilikuwa … Yeye alikuwa Neno lenye uhai la Mungu. Uhai ni Roho; uhai ni Maji, na Yesu ilimpasa apasuliwe na kuwa wazi pale ili kwamba ile Mbegu itoe Uzima Wake na kunyeshea mbegu nyingine zilizokuwa zinakuja. Unaona? Hata akasema ,"Hata ninao kondoo wengine; ambao si wa zizi hili. Ninao. Wataliona hilo; watalipata lile Neno na kudumu kabisa nalo. Nami natuma Roho kulimwagilia maji, nalo litazaa kwa jinsi hiyo hiyo kikamilifu."" Litazaa miujiza, litazaa nguvu za Mungu, litazaa ... na halitakataa lolote, kwa sababu ni mbegu iliyo jamaa ya ile Mbegu. Haliwezi kusema, "Bwana mwiba, uje uishi nami." La, hapana , bwana; la, hapana. Haliwezi kufanya hivyo. Hata kidogo. Haliwezi kujichanganya. Huwezi kuchanganya kifo na uzima. Huwezi kuwa umekufa na uwe hai kwa wakati mmoja.

76 Hivyo, mmeona kile ninachomaanisha? Ni Uhai utokao kwenye Mbegu - Ndiye. Yeye ni Neno la Mungu lililodhihirishwa kikamilifu. Hiyo ndiyo sababu kwamba ndani Yake kulikuwa na nini? Hicho kilikuwa kitu ambacho Yeye kwa usahihi … yule mwana ambaye angetokea kwa Adamu wa kwanza ambaye ndiye mwana aliyeahidiwa apitiae kwa Adamu aliendelea kuja kwa hatua kupitia jamaa ya binadamu, na Hawa alichanganya mbegu na kwa ushirika na nyoka na kuleta kizazi cha watoto haramu waliozaliwa wawe wa mauti bila Uzima, na Yesu alikuja na alikuwa ile Mbegu. Yeye alilihakikisha hilo. Yote yale Adamu aliyopoteza, Yesu alikuwa hayo. Unaliona? Yeye ni yule sahihi … Hatimaye Hawa angelimleta yule mtoto, lakini yeye alichanganya mbegu, akamwingiza nyoka katika utaratibu wa uzazi, akisikiliza hekima, ufahamu, maarifa.

77 Sasa subiri hadi tutakapoingia kwenye Bibi Arusi na hilo. Hilo ndilo … hiyo ndiyo sababu naamini kile ninachoamini. Yapasa irudi kwenye hili Neno. Hiyo ndiyo sababu

nasema kama mtu anataka kujadili na mimi, kuongea nami kuhusu hili Neno, "Njoo." Hiyo ni sawa. Nimekaribisha hilo wakati wowote. Kama unadhani kuwa Jina la Yesu Kristo sio njia sahihi ya kubatizia, njoo zungumza nami kuhusu hilo. Kama huamini kuna kitu kama uzao wa nyoka, njoo unione. Hebu na tuchukue tu Neno. Ikiwa huamini kuwa wanawake wangepaswa kuwa na nywele ndefu na hizo ndizo kifuniko chao, njoo zungumza nami kuhusu hilo kwa Neno. Kama huamini kuwa wakati wa mwisho umewadia na haya mambo ninayosema ni … njoo tuzungumze kuhusu hayo, unaona. Twende. Ndugu Mbegu, njoo. Vema.

78 Huwezi kuwa mbegu na usikubaliane na Neno kwa sababu Neno ndilo Mbegu. Na kama wewe ni Neno, wawezaje kutokukubaliana Nalo? Ungekuwa unayejipinga mwenyewe. Ungekuwa unayetangua nia yako mwenyewe. Kama mtu fulani aliyesema, "Kwa nini unafuatana na watu kama wale?" Vema, kama sikufanya hivyo, ningetangua lile kusudi ambalo kwa ajili yake nilitumwa hapa. Yapasa kuwe na nuru.

Sasa tunaendelea ndani zaidi, tunakwenda kuingiza mambo Fulani na kuwaonyesha jinsi mambo haya yanavyojipanga katika utaratibu - kikamilifu kabisa kulingana na Neno.

79 Sasa, naam, bwana. Yeye ni … hiyo ndiyo sababu Mungu aliweza kutenda kazi Zake kwa kupitia ndani Yake Yeye. Naye alisema nini alipokuwa hapa duniani? - "Sitendi lolote mpaka Baba anionyeshe Mimi" - kamilifu. Na chochote Yeye alichofanya siku zote kilithibitishwa na Maandiko. Yeye alisema, "Chunguzeni Maandiko kwani yananishuhudia Mimi, na kama sifanyi yale waliyosema walifanya, basi mimi si ile Mbegu ya Asili. Lakini ikiwa natenda yale mambo, basi kwa nini hamniamini?" (Hiyo ni sahihi.) Ikiwa hamwezi hata kuniamini Mimi, jinsi nilivyosimama, basi aminini Neno nilisemalo, aminini kazi nizifanyazo, kwa sababu Mbegu Yangu yaweza tu kuzaa kile nilicho Mimi."

80 Mwiba waweza tu kuwa mwiba. Unaweza kuchanganya mbegu na kitu kingine chochote lakini bado ni mwiba. Hiyo nisahihi. Italikubali hilo.

Ndiyo sababu kitu chenye asili mbili zilizochanganyikana ni nafiki. Hiyo ni mbegu mchanganyiko. Mtu anayedai kuwa mtu wa Mungu na huku anakataa Neno, yeye ni mnafiki. Nyumbu anayedai kuwa yeye ni farasi, hawi farasi. Yeye alisema, "Mimi ni punda." Na yeye si punda wala farasi; wewe ni mnafiki, mwanaharamu kwa kuzaliwa, hiyo ni sahihi kabisa. Hilo nimeweka wazi kabisa, lakini hivyo ndivyo lilivyo. Mungu hakukusudia kufanya hivyo. Mwandamu ndiye aliyefanya hivyo kwa hekima yake. Hapo ndipo anapopata. Hapo ndipo hekima yote ya mwandamu inapoishia - kuzaliwa akiwa mwanaharamu. Vema.

81 Sasa, hiyo ndiyo sababu Yesu alidhihirishwa kikamilifu - Mungu alidhihirishwa kikamilifu ndani ya Yesu kwa sababu Yeye alikuwa Neno la Mungu. Yeye alikuwa Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sababu Yeye hangefanyika chochote - ila tu Mungu hasa. Na ikiwa Mungu yu ndani yako, waweza kuwa nini zaidi?

Je, Yesu hakunena juu ya manabii ambao Neno la Mungu liliwajia … Neno la Mungu lilikuja kwa nani? - manabii. Je, Yesu hakuwaita miungu? Kwa nini? - Mungu alidhihirishwa ndani yao. Ilikuwa nini? - Neno lililonenwa likidhihirishwa. Unaona? Ndilo hilo. Akasema, "Mwawezaje kukataa … akasema … Kama mngekuwa na hekima yeyote, mngeelewa." Akasema, "Mimi … mwawezaje kusema mna …tuliwaita … Mungu Mwenyewe aliwaita miungu." Na kusema, "Mwawezaje basi kusema mnawaamini na kunikataa

Mimi nisemapo Mimi ni Mwana wa Mungu?" Kwa nini hawakuliona hili basi?

82 Jambo lile lile leo: "Mimi Ndiye ile Mbegu iliyokuwa ije (uzao wa mwanamke)." "Nitakupa uzao - kwa nyoka. Nyoka alikuwa tayari amemchafua. Yeye akasema, "Lakini uzao wako nitakaokupa utamponda kichwa chake." Yeye atarudisha kile kitu tena! Amina! Natamani - Natamani tu kila mtu angeweza kuliona hilo. "Nimekuja kushinda na kurekebisha kile yeye alichofanya." Na njia pekee ambayo naweza kulifanya ni kupitia mwanamke aliyeiamini ile Mbegu pale ambapo mwanamke hakuiamini ile Mbegu. Mwanamke aliliamini Neno ambapo mwingine hakuliamini. "Mimi Ndiye yule mshindi. Mimi Ndiye yule ajaye kutoa Uzima kupitia kifo Changu, kulipa adhabu ya kile Hawa alichofanya, kwa ajili ya uzima Wangu mtapewa uzima na utatiririka juu yenu, nanyi mtakuwa wana wa Mungu na binti za Mungu" (unaona) - ili mradi ile Mbegu ipo pale.

Changaya mbegu juu ya hili na hupati chochote ila mtoto aliye mwanaharamu wa

kidhehebu. Ni hivyo tu. Chochote kinachokataa Neno. Samahani akina dada. Nawatakeni … Yanipasa nikiseme tu jinsi inavyosemeka hapa, unaona. Na hivyo ndivyo ilivyo.

83 Wana wote wa Mungu lazima wafanane. Naam, bwana. Kuzaliwa kwa Neno na Roho huturudisha kwenye Neno lililonenwa tena kama katika Yohana 3. Unaona? Kuzaliwa kwa Maji na kwa Roho, kunafanya nini? Ndipo kunakurudisha moja kwa moja nyuma tena pale ambapo ungepasa uwe pale mwanzo. Unaona? Hiyo ndiyo sababu ya kifo cha Kristo: huturudisha moja kwa moja wapi? - wana wa Mungu.

Kama Hawa angalikuwa amezaa yule mtoto … Hatimaye angekuwa amefanya hilo. Je, Mungu hakumwambia, "Mkaongezeke na kuijaza nchi?" Lakini aliweza kupita hapa na kutenda sehemu ya kahaba.

84 Unasema tu, "Hilo umeweka mno wazi, Ndugu Branham," lakini subiri tu kidogo; tutaingia katika hilo baadaye kidogo. Unaona? Unasema, "Haiwezekani." Vema, tutaona tu kama Neno linasema ndivyo lilivyo au la. Unaona? Basi ni sahihi. Halija - halikufichwa. Kama limefichwa, limefichwa kwa wale waliopotea. Unaona, hilo ni sahihi.

85 Sasa, hapo ni … hurejesha moja kwa moja kwenye Neno lililonenwa. Ndipo tunakuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa. Unaona? Yesu alisema jambo hili hili. "Yeye aniaminiye, mambo yale - Mimi ni nani, kile nilichojia na kusudi la kufanya - kumrejesha mwanadamu kwenye kuamini Neno la Mungu bila kuchukua chochote pamoja nalo, zile kazi nizifanyazo Mimi naye pia atazifanya." Ndivyo hivyo.

86 Kwa nini haifanyiki hivyo leo? - imechanganywa mbegu, watoto haramu, waliochanganyikana. Hai - ni nyumbu; hajui anaamini nini. Nyumbu hajui baba yake, hamjui mama yake. Yeye ha- … hana ukoo; hakuna chochote kwake. Yeye ni kiumbe haramu.

Hivyo ndivyo mtu yeyote anayedai kumwamini Mungu na haamini Neno Lake atachukua ungamo la dhehebu na kulichanganya na Neno. Unaona, wewe si wa Mungu; umekufa. Huwezi kuwa umekufa na kuwa hai kwa wakati mmoja. Kwa hiyo hata Neno la Mungu halikui. Unashika tu sehemu ya mnafiki. Hebu hilo liende kwa ajili ya askofu, padri, kadinali au yeyote yule. Hiyo ni sahihi. Yapasa liwe Neno au umekufa - mtoto haramu tu. Na Neno la Mungu … Sehemu ya Mungu haitakua. Utaweza kukulia katika shamba hili hili tunaloliendea moja kwa moja, lakini ukawa hakika haupo kwenye zizi. Haiwezi kukua.

87 Vema; vema, tunaona basi, unaona, lile Neno lililonenwa; basi sisi ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Hivyo ndivyo Mungu anavyolitaka Kanisa Lake - ni kujidhihirisha Mwenyewe. Atawezaje kujidhihirisha Mwenyewe bila Mbegu Yake Mwenyewe iwe ndani ya yule mtu? Unawezaje kutumia mawazo yako mwenyewe na Mungu ajidhihirishe Yeye Mwenyewe kupitia kwako? Unawezaje kuchukua imani yako mwenyewe na useme, "Vema, mchungaji wangu hufundisha … Kanuni yangu ya imani husema kuwa hili … siku za miujiza …" Utakwendaje kufanya hilo na uwe mwana wa Mungu aliyedhihirishwa? Utakwendaje kufanya hilo? Kifo cha Yesu hakikumaanisha kitu kwako! "Ee, ninampokea Yeye … Mwokozi wangu" Unasema unampokea, lakini humpokei! Matendo yako yanathibitisha kile ulicho. Yesu alisema kitu hicho hicho. "Kama mnadhani Mimi nimezaliwa haramu …"

Walisema, "Sisi ni wana wa Abrahamu, na hatuhitaji yeyote kutufundisha."

Alisema, "Kama mngekuwa watoto wa Abrahamu, mngenijua Mimi." Unaona? Akasema, "Ni nani miongoni mwenu anayenihukumu kuwa nina dhambi (kutokuamini)? Nionyeshe jambo hata moja, ambalo Mungu aliahidi kuhusu Mimi ambalo halijalitimia. Nionyesheni jambo hata moja ambalo Baba aliahidi ambalo Mimi sijalitimiza. Dhambi ni kutokuamini. Tuone mkilifanyiza basi." Hilo liliwang'oa pembe zao. Unaona? Hakika. Alisema, "Ni nani awezaye kunihukumu Mimi na dhambi na kutokuamini?" Unaona? "Kama siamini, kwa nini basi Baba anafanya kazi Zake kwa njia ya Mimi kama afanyavyo - kila Neno kama alivyoahidi? Sasa hebu nione mahali ulipo katika matendo yako."

88 Ni nani mwanaharamu basi? - ilikuwa wao. Watoto haramu wakidai kuwa wao ni wa Mungu. Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu , Ibilisi, na kazi zake mnazifanya." Shetani alifanya kazi za namna gani? - alijaribu kulichanganyisha Neno la Mungu kupitia Hawa!

Hicho ndicho kile kile hasa ambacho haya madhehebu makubwa yanachokifanya leo. Zile kazi za Shetani, baba yao, wanazifanya. Wanajaribu kuchukua ungamo la dhehebu, na kulichanganya na Neno la Mungu! Hicho ndicho kile alichofanya Shetani

hapo mwanzo - baba, Ibilisi.

Mungu awabariki ndugu. Tokeni ndani yake! Yesu alisema hivyo. Kama unao mkwaruzo mdogo wa Mungu ndani yako, ingekupasa kutazama na kuona hilo. Kuchanganya mbegu! Loo, jamani!

89 Zile kazi alizofanya Yesu - kama mtu anayo Mbegu ya Mungu ndani yake pamoja na Roho wa Mungu akimwagilia maji ile Mbegu, kazi zile zile ambazo Yesu … zilidhihirishwa katika Yesu, Yeye akiwa ile Mbegu ya asili ya Mungu, kifo Chake kinakurudisha kwenye Mbegu ya asili ya Mungu, na ikiwa Roho yule yule aliyekuwa ndani Yake yu ndani yako, basi kazi zile zile zitadhihirishwa. Huamini hilo? Vema, hebu tufungue kwenye Yohana 14:12.

Unasema, "Mimi ni mwamini, Ndugu Branham. Hakika nami ni mwamini." Vema, nitaona kama Yesu atasema wewe ni mwamini, tuone kama Neno la Mungu litakuita mwamini.

Amin, amin, … (kabisa, kabisa) … nawaambia, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atazifanya; kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.

90 Ni nini? - mbegu ile ile. Huwezi kuweka … wawezaje kupanda ngano na ngano hapa na useme, "Nitapata matango hapa na ngano hapa?" Huwezi kufanya hivyo. Njia pekee utakayopata matango ni kupanda matango. Kama ukilichanganya, basi halitakuwa tango. Litakuwa mnafiki. Je, hilo ni sahihi? Hilo litakuwa mnafiki, marafiki. Hili … Yakupasa uliseme. Siyo moja kati ya hizo. Siyo tango wala kile ulichochanganya nalo. Ni mbegu iliyochanganishwa, na ni zao baya, na limekufa ndani yake yenyewe, na haliwezi kujizalisha lenyewe tena kamwe. Limekufa pale pale - kule nyuma, haliwezi kujiendeleza zaidi tena. Hilo linalimaliza; hivyo tu. Lakini kama unataka tango, anza na tango. Kama unataka kanisa, anza na Neno la Mungu. Kama unataka Uzima wa Mungu, anza na Neno la Mungu. Kubali Neno la Mungu katika utimilifu wake, kila kiwango Chake. Na basi hilo ni … Na kama huo ni utimilifu wa Mungu ndani Yako, basi mvua inayonyesha sasa itazalisha kile hasa kilichoko katika bustani yako. Basi sasa, ile Mvua yako ya vuli nafasi yake iko wapi? Unaona kule inakokwenda baada ya kitambo kidogo, sivyo? Ni kwenda na vibuyu mwitu ambavyo Eliya alipata na akadhani havikuwa vibuyu au ile … shule ya manabii juu kule, lile dhehebu walilokuwa nalo. Walikusanya vibuyu mwitu na kudhani … yalikuwa njegere. Loo, vema.

91 Basi kazi zitakazodhihirishwa ndani Yake ni zile zile … kwani ni Mbegu ile ile ya Neno la Mungu. Mwana wa Mungu alikuwa mfano wa Mbegu Yake. Na kile Uzima Wake ulichokuwa Roho alipomwagwa juu Yake baada ya ubatizo Wake na Roho Mtakatifu akaja juu Yake, ule ule Uzima ambao Yeye aliufanyiza uta (ile ile Roho ya kumwagilia maji ya Roho Mtakatifu) - utaleta aina ile ile ya Uzima, akifanya kile kile Yeye alichokifanya; ikiwa ni Mbegu ile ile. Mbegu ya Mwana wa Mungu itazaa Mbegu ya Mwana wa Mungu. Sasa aibu kwenu ninyi wanawake mnaopunguza nywele. Aibu kwenu ninyi wahubiri mnaoikana ile Kweli. Mnasema, "Hiyo ni sahihi, haihusiani na nywele." Lakini Mungu alisema inahusiana.

92 Mnaona pale ilipo? Unaona?Hiyo ndiyo sababu naliamini Neno. Ni Mbegu. Na kama mvua ikinyesha juu ya Mbegu, itazaa jinsi yake. Sasa kuna tatizo gani na hii miamsho? Utafanya nini? - Kupata milioni moja zaidi katika arobaini na nne: Wabaptisti, Wapresibiterian, na kadhalika, Wapentekoste. Lakini uko wapi ule udhihirisho wa kazi zaYesu Kristo! "Sitendi lolote hadi Baba anionyeshe Mimi." Mbegu ya aina hiyo inatoka wapi?

Roho Mtakatifu ataimwagilia maji na kuizalisha ile Mbegu. Ni Maji kwa ajili ya ile Mbegu. Ikiwa Mbegu imekwishapandwa, maji yako hasa kwa ajili yake. Na kama Maji yakianguka juu yako, sema, "Mungu abarikiwe, hebu nikuambie jambo, mhubiri. Mimi ni fulani na siamini juu ya hayo." Wewe ni wa kidhehebu tu. Kwanza wewe ni mnafiki mkongwe. Hiyo ndiyo aina ya mbegu iliyopandwa.

93 Usi- … usi- … usi- … usinielewe vibaya. Nakupenda, Mpenzi. Najaribu kuleta hli kwako, unaona. Ni-Nitaliacha nitakapomaliza leo. Nitaliachia, lakini nataka mjue wakati mmoja kile kilicho sahihi na sababu ya mimi kuamini kile ninachokiamini. Na naamini Ibilisi amekudanganya. Kwa kweli, najua alikudanganya. Kufuatana na Neno la Mungu, haliwezi kushindwa. Ibilisi amekudanganya. Naam, bwana. Hiyo ndiyo sababu nahubiri hayo mambo hivyo: kwa sababu Neno la Mungu lilisema hayo.

"Loo," unasema, "Vema, Ndugu Branham, hii ni siku tofauti." Ni Neno lile lile hata hivyo. Walikuwa na ngano toka ghalani tangu nyuma kule iliyokuwepo katika wakati wa Yusufu na kuiweka na kupanda hapa miaka kadha wa kadha iliyopita (Mliona hilo katika gazeti?), na ikazaa zao la ngano.

Bado ilikuwa ngano; hiyo ndiyo sababu. Kitu ilichohitaji tu ilikuwa tu ni maji.

94 Neno la Mungu ni lile lile tu kama lilivyokuwa wakati Yeye alipolinena nyuma kule miaka maelfu iliyopita. Kitu pekee linachohitaji ni maji! Kwa nini hatupati mazao? Kwa sababu tulipanda namna ya mbegu isiyofaa.

"Wangapi wenu mngependa kubadili hati zenu?" - unakuwa mtoto wa kuzimu mara mbili kuliko ulivyokuwa ulipoanza!" Ni wangapi miongoni mwenu Wamethodisti mngependa kuwa Wabaptisti?" " … ninyi Wabaptisti mngependa kuwa Wapentekoste? Lete tu uanachama wao hapa." Ee, kwa nia njema! Uvundo! Takataka! Takataka za Ibilisi. Hakuna Uzima ndani yake hata kidogo. Ni mbegu mchanganyiko, ya kinafiki, imekufa maradufu, imeng'olewa tangu kwenye mizizi. Je, Yesu hakusema, "Kila pando asilolipanda Baba Yangu wa mbinguni litang'olewa?" Dhehebu au chochote kile, kitang'olewa! Neno la Mungu pekee litasimama! Vema. Hilo ndilo Yeye alilosema. Kila neno la mwanadamu ni uongo, lakini Langu ni Kweli.

95 Basi tutakwenda wapi? Bora urudi kwenye fahamui zako. Lakini huwezi kusikia ila uwe umechaguliwa tangu asili kulisikia. Tunaingia katika hilo. Si ajabu linaanguka kama maji mgongoni mwa bata. Ameumbwa kutawanya maji, sio kuyanyonya.

Safina ilitengenezwa kwa miti ya mvinje na mshita. Ni … si chochote ila ina nafasi ndani. Kila kitu kimetolewa ndani yake. Umekuwa jinsi hiyo - mti mwepesi kuliko miti yote, mwepesi kuliko utomvu wa miti. Kwa nini walifanya hilo? - Kwa hiyo wangeiloweka kwa lami. Kama ukilowekwa … unasema, "Je, mti Ulaya usingefaa pia?" Hapana, bwana, hauwezi kufyonza chochote; unakikataa. Unakataa na huu unafyonza. Na Mbegu halisi ya Mungu inamfyonza Roho! Udhehebu wote unatolewa nje. Kutokuamini kote kunatoka, na Roho Mtakatifu ajapo ndani ya chembechembe ya Uzima uliolala pala, unazaa Mbegu nyingine, iliyo hivyo hivyo. Mwana mwingine wa Mungu amezaliwa, mungu mdogo mwingine, mwana wa Mungu.

96 M-Branham kwa sababu nilizaliwa na Charles na Ella Branham kwa sababu mimi ni mbegu yao. Makubaliano yao wawili kwa maji ya uzazi ya mwili kwa pamoja yalifanya mbegu, na hilo kunifanya mimi.

Mungu na Neno Lake wanapokuwa Mmoja (Haleluya!) hiyo ni … wakati Roho wa Mungu anapoinyeshea Mbegu ya Mungu, Neno la Mungu, inazaa Mungu, na sio mtu binafsi, ni Mungu! Kwa ajili ya nini? - umekufa, wewe si mwenyewe tena. Unajihesabu mwenyewe kufa, uko tupu, ukisubiri chembechembe ya uzima ya Mbegu. Basi ni kitu gani? Si wewe tena, si mwanadamu; ni Mungu ndani ya mwanadamu. Ni uhai wa Mbegu kama Neno lililonenwa hapo mwanzo. Neno la Mungu lililodhihirishwa ndani ya mwanadamu; basi si yule mwanadamu, ni mwanadamu aliyekufa. Hawezi kuwa mbegu iliyochanganywa na awe mwana kwa wakati uo huo mmoja. Ama ni mwana wa kifo ama mwana wa Uzima. Kwa hiyo kama ni mwana wa kifo, apelekwe kwa Ibilisi naye amwue. Jitoe kwa Mungu kwa dakika moja na umwache amwue yule Ibilisi aliyeko ndani yako - amfukuze nje. Anakuweka mtupu. Basi mwache Mungu apande Uzima Wake Mwenyewe ndani yako, ndipo unakuwa si wewe tena; ni Uzima wa Mungu kwa sababu ni Neno la Mungu - lililonyeshewa na Roho Mtakatifu, litazaa tunda la kitu kile kile. Mnaliona hilo? Ningependa kuhubiri juu ya hilo kwa dakika chache, lakini nina kurasa kama thelathini au arobaini za Maandiko hapa … Na nimeshamaliza tatu tu hadi sasa.

97 Vema - lililodhihirishwa. Kazi zilidhihirisha kitu kile kile … nasi tutazitenda hizo hizo, kwani ni Neno lile lile. Sasa kama unataka kuzitenda kazi za Kristo fanya kitu kile kile alichokitenda. "Yeye aniaminiye atakuwa na matendo Yangu." Hiyo ni nini? Aaminiye nini? - kuwa Yeye ndiye uzima wa ile Mbegu ya Asili uliokuja. Mbegu iko wapi? Hapa, hebu nichukue hivi vitambaa vya mkononi. Yupo mtu hapa ambaye alipasa kuwepo hapa. Huyu ndiye yule mtu aliyepaswa kuwa hapa. Ni kitu gani kilichotokea? Hawa aliichanganya - alichanganya mbegu. Ilichokifanya … Ndiyo hiyo ilifanya nini? - iligeukia kifo, ikaendelea kufa, kufa.

Sasa kwa huyu mmoja ile ilitoka - sasa hapa anadumu akiwa Neno hivyo hivyo. Neno amekaa hapa hivyo hivyo. Sasa ni nini kilichotokea? Hili hapa ni Neno. Sasa lile Neno alilolinena Mungu kuwa likaongezeke na kuijaza nchi, halikupata mahali pa kutua.

Mwishowe Neno hili likadakwa ndani ya tumbo la bikira mmoja. (Tutaongea zaidi kuhusu hayo matumbo mawili ya uzazi alasiri leo). Na ni nini kilichotokea? Kutokana na Yeye ilitokea chembe ya Uzima - kile kitu kinachotoa, yale maji yanayofanya kile kiini cha mbegu kiote na kujizaa chenyewe. Yule Roho alitokea ndani Yake na akaenda juu.

98 Ndipo hapa tulipo. Tumetokea kote huko. Ni nini kilichotokea? Tunaamini Hilo, tunaamini hilo. Sasa Yesu alisema nini? - "Yeye aniaminiye Mimi (mnaona) … yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi - yale madhihirisho ambayo Roho Mtakatifu alikuja katika umbo la hua akaja juu yangu na akafanya hili, siyo kwa njia ya kuchanganya mbegu, lakini kwa njia ya kuzaliwa na bikira. Siyo ile … ule utaratibu wa kawaida wa uhai, kama uzazi wa mtoto, mume kwa mke, hapana, siyo hivyo, siyo kuchanganya mbegu, bali kuzaliwa na bikira. Sasa kwa kupitia hii, ninawapa Uzima huu ili ninyi kwa imani mpokee kile Baba, manabii wote, Neno lote la Mungu, nitamwaga Uzima huu ndani yenu, nanyi mta … hamtaweza kufanyiza kitu kingine chochote isipokuwa kile Mimi nilicho." Hivyo ndivyo.

99 "Zile kazi nizifanyazo, naye atazifanya pia." Na Yeye alifanya nini? - kama tu Baba alivyompa kufanya, yale aliyoyaona. Mtakatifu Yohana 5:19 - vile tu … "Sifanyi chochote mpaka Baba anionyeshe." Yeye alikuwa nani - Yeye alijifanya Yeye Mwenyewe kuwa mwanadamu. Mungu alifanyika mwili akakaa kwetu. Neno la Mungu lililonenwa kwa kupitia kwa bikira, lilifanyiza mwili ulioonekana, na katika mwili huo yakaja Maji na Roho, na akaoshwa kwa maji ya Neno, na ndipo yakaingia ndani Yake, yakakaa ndani Yake, na hapo Uzima wa Mungu ukamdhihirisha Yeye Mungu kwa njia ya Kristo, yule aliye Mtiwa Mafuta.

100 Kristo maana yake ni Yeye Aliyetiwa mafuta - Mwanadamu aliyetiwa mafuta. Na Mungu hali amekaa ndani Yake. Ilikuwa ni nini? Ile chembe ikiwa na mwili, Yule Mtiwa Mafuta, mwili ukiwa umetiwa mafuta na Roho wa Mungu ulifanyiza Neno la Mungu lililodhihirishwa. "Nasi tulimwona, mwana pekee wa Baba, amejaa neema." Mnaona? Alikuwa pale, mnaona. Alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Sasa Yeye alikufa ili kulipa deni la kutokana na sisi kuchanganya mbegu. Sasa! Jamani! Hilo hapo. Ni kitu gani? - kwamba ungeweza kufa nafsini mwako, hadi uwe wewe si wewe mwenyewe tena, na ujazwe na Neno Lake, ukiamini Neno Lake, na ndipo Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani Yake ashuke kulimwagilia maji lile Neno, kulifanya liote.

Mnaona? Na ndipo ni kitu gani? Mungu akidhihirisha, akiendeleza kazi ya Mwanawe wa kwanza, Mwanawe wa Pekee, mnaona, Yule aliyekufa kwa ajili ya maisha yetu yaliyochanganywa mbegu, ili aweze kutupatanisha Naye tuwe wana na binti wa Mungu ili kupitia kwa kanisa asimamishe Uzima ule ule kwa njia ya Neno likidhihirishwa kama ilivyokuwa katika Kristo. Kristo alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Na alikufa, akatoa maisha Yake, ili aweze kumtuma Roho - Akapeleka mwili Wake juu na kumtuma Roho arejee kumwagilia maji, alipe gharama ya ukombozi, kama tutaamini hilo. Hivyo ndivyo ilivyo hapo - kama utaamini hilo. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo …" Ndipo akaja Roho Mtakatifu juu ya Neno hilo hilo la Mungu

…

101 "Sasa", unasema, "Kwa nini, kwa nini unalitupa jambo hilo juu ya Biblia basi?" Biblia inapaswa kuwa ndani yako. Neno ni Mbegu, na wakati wote itakapokuwa imelala tu hapa, haitafanya kitu chochote. Lakini wakati itakapoingia ndani hapa, wakati itakapoingia moyoni, ndipo itakapoanza kujidhihirisha kwa njia ya Roho Mtakatifu, matendo ya Mungu. Ndipo maono yanakuja, nguvu zinakuja, unyenyekevu unakuja. Ujuaji wako wote unakuwa umeondoka. Unakuwa si chochote, Kristo anakuwa hai. Wewe unakufa, Yeye anaishi. Ndivyo hivyo. Kwa kuwa Yeye alikufa, mimi naishi. Nitakapokufa, Yeye ataishi tena. Na nitakapokufa, Yeye aliniahidi Uzima. Na nilikufa nafsini mwangu, ili niweze kuwa na Uzima wake, na nilifanyaje hilo? - kwa kulichukua Neno Lake, Mbegu Yake, nikaweka Mbegu Yake ndani hapa kwa imani, nikaamini, na ndipo ikafanyiza kitu kile kile Biblia ilichosema.

102 Sasa, ndugu zangu, chunguzeni katika nchi nzima. Tunakuta uigaji mwingi.

Hebu tuendelee kidogo zaidi.

Vema, kazi hizo hizo zinadhihirishwa katika Kanisa lililokusudiwa, ndizo zilizodhihirishwa katika Kristo. Yeye alisema hivyo - Mt. Yohana 14:12 - "Mbingu na nchi zitapita lakini Neno langu halitapita." Je, hiyo ni sahihi? Vema, waliochaguliwa tangu asili kama Yeye alivyo, hufanya Mbegu ya Neno kufanyika mwili … Ni bora niishie hapa sasa.

Labda isingekuwa hivyo kwako, lakini mtu Fulani anayesikiliza kanda yawezekana asielewe.

103 Kuchaguliwa tangu asili: wana na binti wa Mungu wote walichaguliwa tangu asili. Punde kidogo tutakwenda kwenye Maandiko, na nitayanukuu kwa ajili yako - Waefeso mlango wa kwanza, mstari wa 5. Vema. Tumechaguliwa tangu asili. Kwa nini? - Kristo ndiye Mbegu ya asili na hii Mbegu ya asili ilichaguliwa kimbele kwa njia ya ufahamu wa Mungu wa tangu asili, hali akijua kuwa anguko lingekuja, na akamchagua Yeye tangu asili kuchukua mahali petu. Je unalipata hilo? Wana na binti wote wa Mungu wamechaguliwa tangu asili. Lakini, ndipo ulisema, "Je, Yeye angehukumu kitu?" Hapana bwana. Wewe upo hapa ukiwa mwenye uhuru kiroho kuamua utakavyo, lakini sababu kwamba Yeye alijua, Yeye akiwa Mungu, Yeye Yule asiyepatikana na mauti (kaona nilivyowahi kuwahubiria kuhusu hilo), Yeye alijua kimbele kila kitu ambacho kingetukia, Yeye aliwajua walikuwa akina nani.

104 Sasa, Yeye hakumfanya Hawa atende hilo. Yeye hakumfanya Hawa atende hilo, lakini alijua kuwa Hawa angelilitenda.

Sasa, si ajabu ndiyo sababu naamini katika Mt. Luka 12 (naamini ndivyo ilivyo). Yeye alisema Ni … (usiandike hili nilikujaandika hili baadaye kidogo) kwa Yeye alisema, "Wanayo macho lakini hawaoni. Wanayo masikio lakini hawasikii. Isaya alisema vema kuhusu ninyi. Isaya aliwaona ninyi kimbele." Na pale wameketi pale wakiwa na macho, masikio na kila kitu kinginecho, lakini hawezi kuona. Kwa nini? - Wao wanalisukumia mbali Neno la Mungu. Ndipo Yesu alisema, "Ee ninyi wanafiki. Ninyi ni … ninyi ni wana wa Shetani na kazi zake ndizo mzifanyazo. Basi mnihukumu." Alisema - "kataeni huduma Yangu". Lini unionyeshe ambapo huduma yako inafanyiza Neno lote la Mungu, kama huduma Yake ilivyokuwa. Unaona? Unaona?

105 Sasa, waliochaguliwa tangu asili kama Yeye alivyokuwa - sasa unasema, kule kuchaguliwa tangu asili kunakujaje? Mungu ni wa utaratibu … Sasa kama kuna mtu yeyote asiyeelewa hili, nataka unyoshe mkono wako sasa wakati nitakapomaliza, unaona.

106 Mungu, hapo mwanzo aliwaagiza Adamu na Hawa wakaongezeke na kuijaza nchi. Hivyo ndivyo jinsia ilivyopatikana - sababu ya kuweko kwake. Lakini ni kitu gani kilichosababisha kuchanganya mbegu? - kikaleta kifo. Sasa tutalipata hilo alasiri leo katika yale matumbo mawili ya uzazi. Unaona?

Sasa tazama. Sasa katika hili Mungu alitangulia kuona na akachagua tangu asili ulimwengu wa wana na mabinti. Yeye aliwachagua tangu asili wao wawepo. Na kwa sababu ya kuchanganya mbegu, - kutokuamini Neno la Mungu, kulisababisha kuchanganya mbegu - Mungu alilirejesha tena ili wewe usiwe mbegu mchanganyiko tena; unaweza kurejea hadi nyuma kwenye Neno la asili na ukawa mwana wa Mungu kama tu ulivyopaswa kuwa pale mwanzoni. Mnaona?

107 Kristo asingeweza kutokuwa vile Yeye alivyokuwa. Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Ndiyo hivyo. Mnaona ninachomaanisha sasa? Angalia kama ulikususdiwa, unaona Neno la Mungu, unaliamini; kwa nini? - kuna kitu fulani kipya. Kwa nini? Umewahi kusikia juu ya mvuto wa mienendo katika familia? … mtoto wa kiume atamuiga baba yake, au mama, au babu, au bibi. Huo ni mvuto wa mienendo katika familia. Mmewahi kusikia hivyo? Vema, hilo ni jambo lile lile kwenye kuchaguliwa tangu asili. Ulipaswa kuwa hapa katika njia sahihi tangu mwanzo, lakini kwa kuja kama ulivyokuja, ililazimu uwemo katika anguko. Lakini ukiwa uliyechaguliwa tangu asili unasikia Neno na linakuleta moja kwa moja pale ulipokusudiwa tangu asili! Amina. Hukuwahi kuona hilo hapo mwanzo. Linakuleta moja kwa moja … Kitu gani kinakufanya uamini Neno la Mungu na uache haya mambo mengine? Ni kwa sababu ulikuwa … kuna kitu fulani ndani yako. Nyuma kule ulipaswa … je, ingekuwaje kama … umefanywa uishi hapa milele.

108 "Vema, Andiko juu ya hilo wahubiri."

Linakuja hapa: "Wote aliowajua tangu asili aliwaita, wote aliowaita aliwahesabia haki, na wote aliowahesabia haki, tayari amewatukuza!"

"Kuna haja gani ya kuhubiri Ndugu Branham?"

Kuna zao pale; kitu pekee unachokifanya ni kutupa wavu. Ninautupa tu nione utakakokwenda. Kama wakiukataa, mafuta ya takataka za ulimwengu, madhehebu yanautupilia mbali, siwezi kusaidia; lakini kama kuna mmoja kule ambaye anaweza

kulipokea, atageuka kuwa mwana na binti wa Mungu kama tu hakika ulivyo ulimwengu. Amina! Kwa sababu lilikusudiwa tangu asili.

109 Hiyo ndiyo sababu kwamba Mungu aliweza kufanya kazi Zake kupitia

Yesu; Yeye alikuwa Mwana aliyechaguliwa tangu asili. Yeye alikuwa MwanaKondoo aliyechinjwa kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu! Kabla ya miaka bilioni mia moja, trilioni iliyopita ile tunayosema Mwanzo 1:1 nilihubiri juu ya hilo kitambo kidogo kilichopita, Yeye alichaguliwa tangu asili huko achukue mahali Pake. Amina. Hiyo ndiyo sababu Yeye alifanya mapenzi ya Baba. Yeye alikuwa Neno lililodhihirishwa. Na kila mmoja wa wale wana wengine atakuwa na udhihirisho huo huo, ndio wale waliochaguliwa tangu asili.

110 Lile kundi dogo katika kila kizazi litakuja katika ufufuo kote toka mwanzo wa ulimwengu. Na sababu wakalishikilia … Hata Paulo alililinena katika Ufunuo … katika Waebrania sura ya 11, alisema walizungukazunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi na walikuwa wakiwa na wenye mateso na taabu; ambao ulimwengu huu haukustahili kuwa nao! Amina. Hawana chochote cha kula na kukimbia huku na huku na kukaa katika mashimo na kuteswa na kukatwa vipande kwa msumeno kama Isaya alivyokatwa na wengine wengi - Paulo akiongelea wale watu. Ambao walikuwa, yeye alisema, alinene juu ya kukatwa na vipande kwa msumeno? - Isaya, nabii aliyechaguliwa tangu asili hata kabla ya kuanza kwa ulimwengu. Ilimpasa aje kupitia tumbo la uzazi la Hawa. Lakini basi, alikuja kupitia tumbo la uzazi la mwanamke; roho yake ilipasa ije hapa kuwa shahidi.

Kwa hiyo Yesu alikuja pia kwa ajili ya ushuhuda wa kifo, kuzikwa, na ufufuo kwamba mtu atakufa, lakini ataishi tena kupitia Yeye! Kwani Yeye ni Mbegu ile itakayoinuka. Natumaini mnaliona.

111 Vema, Yeye akiwa amechaguliwa tangu asili, hufanya Mbegu ya Neno iwe mwili ndani yako, Kanisa Lake. Neno la Mungu … Unasema, "Hakika Ndugu Branham, kila Neno, naliamini." Basi usishikilie tena mila zako, unaona? Dumu kwa usahihi na lile Neno na ukae nalo; tazama kinachotokea. Sema, "Ee Mungu. Bwana, naliamini. Mtume Roho Mtakatifu." Ndipo utazame. Basi kama Yeye akiendelea kushuhudia, ndipo unajua unaye - si kwa msisimko fulani, mapepo hufanya hivyo; sio kwa maajabu, mapepo hufanya hayo; ila kwa kudumu kwako bila ya kutetereka ukiliamini Neno la Mungu na maisha yale unayoishi bila ya kukana lolote kamwe. Vema, hilo hufanya Neno kuwa mwili, unaona, mwili na maji yale yale ya Roho.

112 Sasa subiri kidogo. Siwezi kulipita hili. Unaona, Yesu alikuwa mbegu ya Abrahamu, kwa kunena kimwili. Je, hilo ni sawa? - mbegu ya Abrahamu iliyochaguliwa tangu asili. Na Roho aliposhuka juu Yake, Yeye alileta aina gani ya uzima? - Alileta uzima wa imani. Aina gani ya uzima?

"Unamaanisha alikuwa awe mgeni kama Abrahamu?"

Hapo ndipo watu huchanganyikiwa mno leo. Wanajaribu kuwaza kuwa mtu wa Mungu yampasa kufanya hili na kufuata hili na kufanya lile. Lo rehema, hapana! Nini kilikuwa - Kristo alikuwaje Mbegu ya Abrahamu? Si katika … si sana katika mwili Wake, kwa sababu Isaka, ile mbegu ya Isaka, hatimaye ilianguka na kufa. Ilirudi nyuma na kuchanganya mbegu pia. Tutaingia katika hilo moja kwa moja. Unaona? Lakini ile mbegu ya imani ya Abrahamu ambayo aliamini Neno la Mungu bila kujali hali ilivyokuwa … Hivyo ndivyo! Hu! Unajua, najisikia kama nipige kelele! Tazama, angalia, mbegu ya imani ya Abrahamu. Ilikuwa nini? - si mwili wa Abrahamu, ila imani ya Abrahamu. Imani ya Abrahamu katika nini? - Neno la Mungu. Haidhuru kitu gani kinakuja, aliita chochote kinyume Nalo kama vile hakikuwa pale. Ee mimi, je, hilo lisingerarua hayo madhehebu vipande vipande? Umph, umph, umph, umph! Hakika lingefanya hivyo.

113 Kama hata Kweli ya ndoa na talaka ililetwa tu katika Nuru yake kuwa ipo ndani hapa katika Biblia, ingevunja kila kanisa katika mji huu - mji mwingine wowote - wakijaribu kurudi katika hiyo. Pande zote mbili zimekosea. Naweza kuthibitisha hilo Neno. Wote wamekosea. Vema, iwapo mwanaume angefanya hili au lile, au mwanamke afanye hili au lile, sitalisema, kwa sababu kuna kuchanganyikiwa kutosha miongoni mwao. Unaona? Yesu alisema, "Waacheni. Kipofu huongoza kipofu." Kwa nini, wanalalamika tu juu ya hilo, wasingeweza kuamini hilo. Kama walizaliwa ili waupate Uzima wa Milele, wataamini Neno. Hiyo ni sahihi. Kama sivyo, Mungu atajidhihirisha Mwenyewe kwao. Kama hawaliamini, mbona, hawataliamini; hivyo tu.

114 Hebu tuliendee hili kwanza. Tutaweza kuliendea hilo wakati fulani baadaye, lakini hebu tushughulike na hili kwanza na tuone kwa nini ni lazima tuamini haya mambo - na tutayaaminije. Ni lazima uyaamini. Kama huyaamini, umepotea; umepotea. "Niamini nini, Ndugu Branham? - wewe?"

Hapana, bwana, siyo mimi. Uniamini mimi … Nasema Neno. Siweki chochote hapa. Nawaambia tu kile Biblia inachosema kuhusu kuamini hili Neno. Na nilichofanya ni kujaribu kuamini Neno lile kama Tu lilivyoandikwa. Siongezi chochote, sipunguzi chochote; naisoma tu jinsi ilivyo na kuiamini hivyo tu. Na kwa neema na msaada wa Mungu Mwenyenzi, ameithibitisha na naita mtu yeyote authubutu kukanusha. Sasa, ninyi kwenye kanda mjooni mlifanye. Niambieni wakati wowote niliowahi kuwaambia chochote cha makosa … ambacho hakikutokea. Niambieni chochote wakati wowote ambao Mungu hakuwahi kuthibitisha na kulitenda tu kulingana na jinsi lilivyosema.

115 Vema. Kwa kuchaguliwa kwake tangu asili, hufanya Mbegu ya Neno maji yale yale juu ya nini? Kanisa hili leo ni Bibi Arusi aliyechaguliwa tangu asili? Je, Mungu alisema Yeye angekuwa na Bibi Arusi asiye na ila wala kunyanzi? Basi limechaguliwa tangu asili, sivyo. Unaona? Vema, Kristo alichaguliwa tangu asili. Yeye alikuwa Mbegu ya Kifalme ya Abrahamu, nayo lifanya nini? Roho alipokuja juu ya Kristo, Yeye alishuhudia Neno la Mungu, na wakati yale Maji, Roho, yanapotiririka juu ya Mbegu ya Neno, Mbegu ya Kifalme ya imani ya Abrahamu katika Neno la Mungu itazaa zao la aina ile ile.

Unasema, "Siamini hilo." Vema, hebu tutafute. Hebu sasa tuende tuone; je, sisi tu mbegu ya Abrahamu? Mwanzo 17. Rudi kwenye Mwanzo na upate ile sura ya 17. Naacha mengi ya haya hapa, lakini ya-yanipasa nigonge baadhi yake ndani hapa kwa sababu baadhi ya wakosoaji wanaweza kuja na kusema, "Siamini hilo," kwa hiyo tutaweka kidogo ndani pale ili Yeye amzuie yeye kulisema, unaona. Vema, 17:7. Hebu tuanze kwenye aya ya 6.

Nitakufanya uwe na uzao mwingi sana … (mbegu ya Abrahamu) …nami nitakufanya kuwa mataifa (Mataifa na wote) … na wafalme watatoka kwako.

Agano langu nitalifanya … (sasa tazama) … imara kati ya mimi na wewe, na uzao wako baada yako, na vizazi vyao, kuwa agano la milele, kwamba nitakuwa Mungu kwako na kwa uzao wako baada yako.

116 Mbegu ya Abrahamu ni nini sasa? Siyo mwili wake. Paulo alisema Myahudi … kwamba Myahudi kwa nje sio Myahudi; ni Myahudi kwa ndani. Mnaona? Mbegu ya Abrahamu ni nini? - wale wanaoliamini Neno lote la Mungu bila kujali ni wa dhehebu gani au baba au mama au chochote anachokisema yeyote; wanaliamini Neno lote la Mungu. Mungu alisema, "Nitalifanya agano langu sasa hivi (kuchagua tangu asili) hili agano na wewe na uzao wako katika kila kizazi baada yako watakaoliamini." Ndivyo hivyo - mbegu ya Abrahamu. Sasa unasema … sasa tazama, Mungu alisema,

"Nitalifanya na uzao."

117 "Vema," unasema, "Ndugu Branham, hilo linampa kila mtu …" Subiri kidogo sasa. Hebu twende kwenye Waefeso sasa, pale kwenye Kitabu cha Waefeso, na tutaanza kwenye sura ya 1 ya Waefeso. Na ndipo tutasoma kidogo hapa na tuone tu kile Mungu anachosema juu ya hili somo. Sasa, sikiliza. Paulo - sasa, tazama jinsi anavyoliweka hili sasa. Sasa kila mtu kwenye … kwenye miguu yenu sasa. Tuna … make macho. Tuna, dakika chache sasa ndipo tuta- … kwenye dakika arobaini na tano, kitu fulani, halafu tutaondoka kwa ajili ya chakula cha mchana. Sasa tazama;

Paulo, mtume …(mtume ni nini? - aliyetumwa. "Paulo aliyetumwa na Yesu Kristo." Sawa hilo? "Kwa mapenzi ya Sanhedrin?" Nimesoma hilo vibaya, sivyo? "Kwa mapenzi ya Lutheran." Vema, vyovyote …)

Paulo, aliyetumwa na Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu, kwa watakatifu … (Ni akina nani? Kwa kila mtu? La, bwana. Sio kila mtu awezaye kulipokea. Hiyo ni sahihi.) … kwa watakatifu walioko Efeso, wanaomwamini Kristo Yesu.

118 Wale walioko ndani mle tayari. Hilo ndilo ndilo kundi ambalo natumaini naongea nalo katika hili kusanyiko asubuhi hii - wale ambao tayari wako katika Kristo Yesu. Sasa hilo ni wakati hili … Unaona, huwezi kuwaambia wale, wale watoto nje kule kuhusu hili. Hawawezi kula nyama; yawapasa wanywe maziwa. Wamedumaa, unaona. Kwa hiyo, kumbukeni, hawawezi kula nyama ngumu. Sasa:

… wanaomwamini Kristo Yesu:

Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo. (Vema.)

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki … (sasa, yeye anaongea juu ya kanisa sasa. Hii sio nje; kanisa tu) … kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho … (kama asubuhi hii - wale wanaolipenda; wanalila tu) … ulimwengu wa roho ndani ya Kristo:

119 Kama vile alivyotuchagua … (Je, sisi tulimchagua? Aha aha? "Ee Ndugu Branham, samahani, mimi nilimchagua." Hapana … Kufuatana na Neno, hukumchagua. Yesu alisema, "Hamkunichagua ninyi; niliwachagua Mimi." Ee naam. Je, Yeye alilichagua lini? Yesu alilichagua lini Kanisa? - kabla kuwekwa misingi ya dunia.

Kama vile alivyotuchagua katika yeye … (kwenye ule uamsho uliopita aliokuwa nao daktari Fulani. La, hapana. Lazima uwe umesoma hilo katika kanuni, kitabu, lakini sio katika Hiki)

Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, … (Tulichaguliwa lini? Kwenye uamsho uliopita? Usiku ule tulipookoka? Mbona, wakati hakukuwepo na ulimwengu, hakukuwepo na nyota, hakukuwepo na atomi, hakukuwepo na molekuli - ndipo tulipochaguliwa. Amina. Ee, msiniache nikaanza kuhubiri juu ya hilo. Najaribu tu kuelezea jambo fulani hapa. Vema.)

… kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe …(nini? - washiriki, "La, tuwe … ee, baada ya kuokoka unatenda tu upendavyo" - hapana.) … tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika … (ushirika? Ee, la. Ni upendo, sivyo? Hiyo ni sahihi. Vema. Katika upendo! Samahani, nadhani nakata tu sasa. Nisingefanya hivyo. Vema.) … katika pendo.

Kwa kuwa …(Nini? A-l- i - t - a - n - g - u - l -i-a k-u-t-u-c-h-a-g-u-a t-an-g-u a-s-i-l- i)

… alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe … (mbegu tangu asili, unaona) … wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake,

120 Nani alilifanya? - Mungu! Yeye alilifanya lini? - kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Basi kama tukija katika uzao wa haramu kupitia uchafu wa Hawa, ukitufanya sote watoto wake na tukabiliwe na kifo, basi Mungu Mwenyezi yapasa aweke njia kukomboa watoto Wake. "Na wote wale alionipa Baba watakuja kwangu. Na hakuna mtu atakayekuja ila avutwe na Baba Yangu." Loo, jamani! Sasa liko wapi jambo lako kubwa ulilolifanya? Hakuwahi kufanya lolote. Yakupasa uone aibu. Mungu, Yeye aliyefanya yote … Gurudumu linakwenda sawasawa.

Mtu fulani alikuja juzi na kusema mtu fulani alisema jambo fulani baya kunihusu na kunishutumu juu ya jambo fulani lililokuwa la makosa. Nikasema, "Ee, achana nalo."

Akasema, "Unawezaje kulichukua hivyo? Hilo linahusisha familia yako."

Nikasema, "Loo, jamani." Nikasema, "Hilo lilichaguliwa asili kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu kuniwia jaribu." Nikasema, "Jamani, jamani, jamani. Hakika, kwa hiyo hilo ni sahihi."

Akasema, "Unalifanyaje?"

Nikasema, "Ikiwa ningetazama chini moja kwa moja hivi, ningekuwa nikianguka wakati wote."

121 Hiyo ndiyo njia ya watu leo: "Kama nikipokea Kweli ya Neno la Mungu, Ndugu Branham, watanitupa nje." Vema, unatafuta nini hapa? Tazama hapa mwisho wa njia. Unaona, mtu anayetazama hivi, hajui anakokwenda. Yeye anatazama hivi. Lakini nikitazama kule, hujali kile kinachoendelea sasa, unajua kule unakokwenda. Unaona? Ndivyo hivyo. Tazama kule unakokwenda. Kaa kwenye mstari ukilingana Neno.

122 Vema, tumechaguliwa tangu asili ili tufanywe wana. Sasa mnaamini kuwa tulichaguliwa tangu asili? Sasa, je, Yesu alichaguliwa tangu asili? Yeye alikuwa Mwana-Kondoo wa Mungu aliyekwishachinjwa kabla hakujawepo na nuru, kabla hakujakuwepo na kimondo, kabla ya kuwepo molekuli, atomi - chochote. Yeye alikuwa Mwana wa Mungu aliyechinjwa. Loo, ukuu wa Mungu. Basi hizi akili ndogo sana zitokazo kwenye kiangulio kilichotengenezwa kiungu hapa zinajaribu kujadili hilo na kusema hilo sio

sahihi. Hiyo ni aibu.

Wewe ni nani? Hata baadhi yao husema hakuna kuzimu, na umekaa juu ya chungu chake siku zote - yenye unene wa maili elfu nane chini yako, volkeno, na ndipo unatazama juu na unampinga Mungu na Neno Lake. Unapopinga Neno, unampinga Mungu. Hiyo ni sahihi. Ee, jamani, jinsi ulivyo Mkuu, Bwana. Tungekuwa waaminifu jinsi gani.

123 Vema, kwa hiyo waamini wa Neno na Roho lazima wawe mmoja. Mnalielewa? Waamini, Neno, na Roho ni mmoja kabisa. Hutendi mawazo yako mwenyewe; hutumii akili yako mwenyewe. Je, hilo si la ajabu? Ile nia iliyoko ndani ya Kristo iko ndani yako, unaona. Nia iko ndani ya Kristo na utachukua Neno kama tu Yeye alivyofanya kwa sababu Yeye alikuwa lile Neno. Na kama nia ya Kristo iko ndani yako, wewe ni lile Neno. Wewe ni Neno la Mungu lililo Hai, wawakilishi Wake duniani - hiyo ni sahihi - mkiendeleza kazi. Kanisa lapasa liwe hivyo.

Na hivyo, Biblia inadhihirishwa tena kama zile siku za mwanzo za wanafunzi, kama wanafunzi tu. Biblia inaishi tena ndani yako.

124 Sasa hebu tuone, yanipasa nijaribu kupata angalau kama kurasa kumi natano hapa kwa haraka, na nachukia tu kufanya hilo, ila nitakwenda tu kupita juu yake kwa sababu kama sikufanya hivyo, basi nitafanya hivyo mchana huu na kuwa na mkutano kesho, na yanipasa niharakishe sasa. Vema, sasa tutajaribu kulifanya kwa haraka zaidi kama tutaweza; kuingia ndani yake. Mnaamini?

Vema.

125 Na hivyo, Biblia inadhihirishwa tena kama katika siku za mwanzo za Kristo. Unaona, kwa sababu wewe ni mbegu iliyochaguliwa tangu asili kama tu ilivyokuwa kwa Kristo; na mvua inaponyesha juu ya mbegu, uzima unajizalisha wenyewe. Wakati Roho Mtakatifu - anaposhuka - aliposhuka juu ya zile mbegu ambazo Yesu alisema alizichagua - lini? - kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu. Basi zilikuwa mbegu zilizochaguliwa tangu asili. Sawa hilo? Basi hapa walijikokota wenyewe hadi ndani ya chumba cha orofani, hizi mbegu, lile Neno, na Neno lilikuwa limelala pale bila Uhai ndani yake. Ghafla tu kukatokea uvumi kutoka Mbinguni kama maji yakitirirka kwa kasi. Na hakika ulijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi humo. Na mbegu zikaanza kuota. Nazo zikaanza kujidhihirisha zenyewe - Lile Neno la Mungu likidhihirishwa.

126 Vema, kwa nini basi mioto ya uamsho ikapngua ukali? Sasa, nina Maandiko kumi hapa (kama ungeweza kuyaona hapa) kwamba ilipasa niyaseme, lakini ninalazimika kuyaruka mengi katika hayo, na hivi … ili mpate muhtasari wake.

Vema, kwa nini basi mioto ya uamsho imepungua makali? Sasa, italazimu kutaja majina. Sitafanya hivi tena baada ya hili, mpaka Mungu aniambie nifanye. Lakini itabidi nitaje majina. Itabidi niseme mambo ambayo sitaki kusema, lakini ili kuweka jambo hili wazi … Unaweza kuona sasa ninakoelekea sababu ya mimi kufanya haya ambayo nimeyafanya. Ninnamini hili ndilo lile Neno. Na ninaamini kuwa Kristo analo Kanisa, na Kanisa ndilo shamba (tutalifikia hili punde kidogo) na yabidi ulifikishe Neno shambani kabla yule Roho hajafanya jambo lolote. Unaona?

127 Kwa nini basi ile mioto ya uamsho imepungua makali? Husikii zaidi sana tena kuhusu Billy Graham, kama wainjilisti wakuu. Oral Roberts hachomi nchi tena kama ilivyokuwa awali. Mikutano yangu wala haisikiki tena. Kuna watatu tu. Kuna jambo gani? Lakini tunakwenda kupata fundisho la kina sasa. Inabidi niende kulitumia hili sasa na kama hii kanda itaangukia mikononi mwa Billy Graham, Oral Roberts, ninataka mfahamu, ndugu zangu, si kwamba ninawapuuza ninyi, ninachukua nafasi yangu pale, kama ukiliona hilo, kama ndugu mjoli wenu katika Injili. Na baada ya hili nafikiri mtakuwa na ufahamu bora zaidi, ndugu, juu ya kwa nini nimefanya haya ambayo nimeyafanya. Na natumaini nimepata neema usoni pa Mungu, na mbele zenu, katika kuwa mwaminifu na mkweli kuwaeleza sababu ni kwa nini.

128 Billy Graham - kitambo kilichopita ulimwengu ulikuwa unawake na Billy Graham.. Ni mara chache utasikia juu ya hilo sasa. Yeye bado anaendelea, lakini ni jambo gani lililotokea? Oral Roberts - mbona, amekuwa tu akiiwasha dunia moto; anazimika. Tommy Osborn - wote hawa ni watu wema wacha Mungu. Ni jambo gani limetokea? Hali nikiamini kuwa Mungu aliniita kwa ajili ya huduma, ni jambo gani limetokea kuhusu huduma yangu? Sasa haya yanakwenda kujibu baadhi ya maswali. Ni jambo gani

limetokea?

Unasema, "Ndugu Branham, huduma yako ndiyo iliyozimika kuliko zote." Hiyo ni kweli. Hiyo ni sahihi. Billy Graham anasikika zaidi kuliko mimi, na Billy Graham anasikika zaidi kuliko Oral. Oral anasikika zaidi katika siku moja kuliko ninavyosikika katika miezi sita. Tommy Osborn, Tommy Hicks, yeyote katika hao watu wacha Mungu, wanasikika zaidi. Kwa hiyo kadri yanavyotokea, ya kwangu inatupwa mbali zaidi ya hizo nyingine zote.. Ni jambo gani limetokea? "Ndugu Branham, wewe unasema hivyo … kuwa ulikuwa unatuambia kuwa wewe unaamini Neno kabisa na kila kitu, vema, ni kitu gani kimekutokea nini basi? Ni jambo gani limetokea?" Hilo ndilo tunalotaka kujua. Hilo ndilo tunalotaka kujua.

129 Sasa hebu liweke akilini mwako sasa. Uushushe mwavuli chini, na uutikise kuondoa mvua, na uufungue moyo wako kwa muda mfupi na usikilize. Kumbuka Biblia ilisema katika Mwanzo mlango wa kwanza, tulisoma ili kuweke msingi wa wazo letu la siku, na kila mbegu kwa jinsi yake. Itapasa izae kwa jinsi yake. Hiyo ni sahihi. Kila mbegu itapasa izae … Kumbuka, dunia imejaa mbegu na kuwa mvua itoe miche kwa jinsi zake.

Ninamini tuko wakati na kipindi cha mavuno. Hamwamini hilo? Nyote mnakubaliana na hilo. Tuko karibu na wakati wa mavuno. Sasa, mbegu zimekwishapandwa. Hilo ndilo jambo lililoko kwetu. Mbegu tayari zimekwishapandwa. Ee, Mungu, natamani ninyi mngeweza kuona kitu kilichopita mbele yangu wakati huo. Mbegu zimekwishapandwa. Kumbukeni kuna wakati wa kupanda mbegu, ndipo wakati wa mavuno. Wanajua kuwa walisema hivyo.

130 Vema. Sasa, kumekuwepo na mbegu aina tatu zilizopandwa. Ya kidhehebu - Billy Graham; yeye alikuwa mpanzi mkuu. Oral Roberts kwa ajili ya Wapentekoste. Mbegu za Kipentekoste zimekwishapandwa. (Sasa ninazungumza kuhusu shirika la dini.) Na ndipo Neno limeshapandwa. Sasa itabidi muelewe, enyi watu. Singesema haya kama Mungu hakuniambia. Nataka myapate haya vizuri na kwa uwazi. Mbegu za aina tatu zimeshapandwa. Ndiyo sababu upandaji umekakaribia kumalizika. Unaona? Umekwisha. Sharti mbegu zipandikizwe kabla mvua haijanyesha (Hiyo ni sahihi?) au la sivyo yule Roho. Sasa, hapo mnakwenda kupinga, lakini hebu mtulie msikilize kwa muda mfupi. Sharti mbegu zipandwe ndipo mvua inyeshe na kuzitia mbegu maji. Hiyo ni sahihi? Sasa nataka Kuna mtu yeyote ndani hapa anayeelewa Kiebrania? Anayejua maneno ya Kiebrania? Vema, basi mpekue ili kuyapata kama mnataka.

131 Sasa tunasikia mengi mno na mashirika mengi sana ya dini na kila kitu kingine wakiongea kuhusu tumo katika "mvua ya vuli" Upuzi. Hakuna kitu kama hicho. Sasa, ee, Ni … Kuna kitu kinatokea. Ninaweza kuona tu kikipita mbele yangu. Nimedaka huyo Roho, unaona. Amina. Najua hili ni ile Kweli; ni HIVI ASEMA BWANA. Maono, unaona, yanakwenda tu na kurudi. Siwezi hata kuyaelezea hapa. Kila wakati ninapotazama, ninaona yakipita mbele yangu namna hii na yanafunuka na kwenda hivi na kutazama upande huu. Nimejaribu kuwatazama jamaa ambao wameketi chini hapa. Natazama huko na kila mahali, natazama kama ndio lile, unaona.

Vema, hebu turudi nyuma na tulijaribu tena sasa na niwe na hakika ninalo ndani pale. Sielewi kile hasa kilichotokea kwenye ule mwelekeo.

132 Naamini kuwa ni wakati wa mavuno. Mbegu zimepandwa. Mbegu za kidhehebu za makanisa kama ya Kiinjili, kama Wabaptisti na Wapresibiterian na Walutheri na mbegu za Kipentekoste zimepandwa katika shirika la Kipentekoste, na watu mashuhuri kama Oral Roberts, Tommy Hicks, na Tommy Osborn, watu mashuhuri wa Mungu, unaona. Na naamini kuwa Neno la Mungu lisiloghoshiwa limepandwa mbali na yoyote ya hayo mashirika ya dini.. Hilo ndilo jambo lenyewe, unaona.

Mbegu lazima iwe na … Mmea wa mbegu lazima uwe na maji ya mbegu kabla haujaota. Lazima uwe na maji kabla ya ile mbegu iliyopandwa kuota.

Sasa, "Vema," unasema, "Ndugu Branham, kumekuwa na yetu …" Najua, hiyo ni sahihi. Nimelidaka wazo lako sasa, unaona; huwezi ukalificha sasa. Vema, kwa hiyo muwe waangalifu yale unayowaza.

133 Sasa, mbegu lazima ipandwe na ndipo lazima ipate maji ili iote. Sasa, unasema, "Vema, Ndugu Branham (Nitaeleza mawazo yenu hapa), tumekuwa na maji." Iwe hivyo. Hilo ni sahihi. ….Umekwishakuwa na maji. Umewahi kupanda kabeji au chochote au mbegu au kitu fulani au kingine namna hiyo, siku zote … kama havikupata maji

wanamwaga tu kidogo juu yake.

Vema, lakini subiri sasa, tulikuwa na nini katika ule wakati wa kupanda? - ile mvua ya masika. "Ee," unasema, "Ndugu Branham, upuzi." Sasa subiri kidogo. Unachukua lile neno la masika katika Yoeli 2 na kulitazama na uone kama neno la Kiebrania … unakwenda katika Kiebrania na uone kama hali- … kama unapenda kuliandika, m-o-u-r-e-h, moureh, na uchukue neno la Kiebrania na ulitafsiri na uone moureh inamaanisha nini - kufundisha. Mvua ya kufundisha imenyesha. "milioni moja zaidi katika arobaini na nne" - Wabaptisti. Fulani, Fulani - washiriki katika kanisa. Oral Roberts, na ndugu wengine wakiwa na uhamasishaji wa Kipentekoste … au ule uahamasishaji mkuu wa Kipentekoste na wakawafikia mamilioni, unaona, hiyo ni sahihi. Na Mbegu imetoka, lile Neno, kwa ajili ya wachache - lile kundi.

134 Sasa tazama. Sasa kumbuka lile neno, m-o-u-r-e-h, moureh humaanisha kufundisha, ile mvua ya masika. Linasema Mvua ya moureh, mvua ya kufundisha. Mvua ya kufundisha imekwishanyesha.

Billy Graham ameuwasha moto ulimwengu. Wapentekoste wameuasha moto ulimwengu, na Neno limeuwasha moto ulimwengu. Sasa tatizo ni nini sasa? Sasa anasubiri mvua ya vuli. Hapo ndipo ulimwengu utakapozaa matunda yake. Ee, natumaini mnalielewa.

135 Ndipo aina ya mbegu uliyopanda shambani mwako itakuwa aina ya zao utakalolivuna. Kama madhehebu yanahitaji washirika zaidi, hicho ndicho watakachokipata. Hicho ndicho walicho nacho. Wapentekoste wanataka Wapentekoste zaidi, hicho ndicho watakachokipata. Vema. Lakini Neno linakwenda kuzaa wana na binti wa Mungu. Hilo linakuja pia. Tazama, tazama ile mvua kuu ya vuli inayopaswa kuwa imenyesha - jinsi watakavyopanda juu ya kuta na kuruka na jinsi watakavyokuwa jeshi wakija. Subiri kidogo tu. Aina ya zao utakalopata ni aina ya mbegu uliyopanda shambani mwako.

136 Vema, aina mbili za kidhehebu … mnaelewa? Zile aina mbili za kidhehebu zitaungana kwenda Sodoma. Lakini Neno litakaa na wateule, ile Mbegu ya Kifalme. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu." Malaika wawili walikwenda, wahudumu wawili waliopakwa mafuta, walikwenda Sodoma kujaribu kumtoa mtu aliyekuwa amerudi nyuma, (alikuwa na sehemu ndogokuhusu Mungu) na mke wake, bibi arusi wake - mnajua kilichomtokea yule bibi arusi; alifedheheka. Na watazame binti zake na utazame kile kilichoanguliwa baada ya wao kutoka. Siku zote kuna "unywele ndani ya biskuti." Mnajua hilo ni kweli. Samahani kwa usemi huo, lakini mnajua, kitu cha kuziba, kwa hiyo hilo ni … ilikuwa hivyo siku zote; tunajua hilo. Sasa huwezi kulikataa Neno la Mungu!

137 Lakini kulikuwa na Mmoja aliyekaa na Abrahamu aliyetoa ishara. Hilo ni sahihi?

Vema, vema, mmoja alibaki … Abrahamu na kundi lake waliitwa nini? - mbegu teule ambayo kamwe haikwenda chini kule. Wao walikuwa mahujaji. Walisafiri hapa; walisafiri kule. Walisafiri hapa; walisafiri kule - bila kufungamana na dhehebu lolote. Lakini dhehebu lilikwenda na kujitengenezea mji, na Lutu akawa kuhani, au askofu, au … mnajua, chchote kilichokuwa kule, mtu mkubwa, akikaa mjini na kutoa uamuzi, ambao anasema, "kasisi mkuu", "Hapana, hatukubali kumkaribisha yule mtu miongoni mwetu; la, bwana! Yeye hakubaliani na thiologia yetu. Hatuwezi kuwa nalo." Kuna Lutu wa zamani. Ameketi pale. "Ikiwa hawezi kuwa na hati toka kwenye kundi letu, hatuwezi kumkubali hata kidogo." Nani aliyekuweka uwe mwamuzi juu ya Nyumba ya Mungu, ninyi mliochanganya mbegu? Neno la Mungu litahubiriwa vyovyote vile!

138 Mtakatifu Martin alikwenda kwenye kundi kama lile, na yule mtu hata hakuweza kusimama kumpa heshima baada ya yeye kulivunja lango. Hata Mungu akaunguza vazi lake, nyuma yake; akamfanya asimame na kumsalimu yule nabii wa Mungu aliyeingia mjini. Hiyo ni sahihi. Kiti chake kilishika moto pale alipokuwa amekaa, kile kiti cha enzi alichokalia. Hiyo ni sahihi. Umesoma historia ya kanisa. Naam, bwana. Alikwenda kule akiwa na Neno la kweli, akafanya miujiza na ishara na kuthibitisha juu ya Neno ambalo yeye alikuwa. Walikuwa na uaskofu wao wenyewe na walikuwa na kile walichotaka, na hicho ndicho walichotaka tu; lakini Mungu anakwenda kuhakikisha kuwa … lazima kuwe na watoto wateule ndani mle, na Yeye yampasa kuwapata. Hiyo ni sahihi.

139 Hivyo, kumbuka, ilikuwa nini? Sasa hebu tusimame kwa dakika moja. Wakati fulani Lutu alikuwa na uchaguzi kuwa mtu wa kidhehebu yeye mwenyewe. Sivyo? Wakati

fulani alikuwa na uchaguzi kusafiri na Abrahamu, lakini kuupenda ulimwengu kulimsonga hata kumtoa nje. Hicho ndicho kinachofanyika leo. Na kumbukeni, wale kule Sodoma hawakuwahi kuona hata moja ya ile miujiza ya Kiungu. Walikuwa na upofu; na kuhubiriwa kwa Neno hupofusha macho ya wasioamini. Hilo ndilo Billy Graham na wengine walifanya - walipofusha macho ya wale wasioamini kule. Hiyo ni sahihi. Sasa huwezi kukataa kuwa Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja … " Na lipo hapa katika Biblia. Litakuwa jambo lile lile kwenye kuja kwa Mwana wa Adamu.

140 Sasa tazama, lakini kulikuwa na Mmoja ambaye alikuwa Neno, na Yeye alikaa wapi? - na wale walioahidiwa, wateule. Neno alikaa na wateule. Na Neno la Mungu leo litakaa na Mteule! Ni Mbegu ya Kifalme ya Abrahamu kwa ahadi.

Lilifanya kazi ya jinsi gani? Lilipodhihirishwa kwenye miaka mia nane baadaye katika umbo la Yesu Kristo, lilifanya kazi zile zile ambazo Yule alizifanya kule, alizofanya Neno, kwenye lango hemani kwa Abrahamu - Akiwa ameketi na kulipa hema kisogo, akamwambia Abrahamu kuwa jina lake lilikuwa Abrahamu sio Abramu, ambalo limekuwa hivyo siku zote (jina lake nini …), lakini jina lake lilikuwa Abrahamu kwa sababu Mungu alikutana naye siku chache kabla ya hapo na kumwambia jina lake lilikuwa Abrahamu. Akasema, "Mke wako yuko wapi …" sio S-a-r-a -i, S-a-r-a-h Mke wako Sarah yuko wapi? " kama vile Yeye hakujua.

Akasema, "Yuko hemani nyuma yako."

Akasema, "Nitakutembelea …" Mimi, kiwakilishi binafsi. "Nitakurudia wakati uu huu mwakani (Loo!), nawe utapata mto ambaye mekuwa ukimtarajia. Mvua ya vuli inajiandaa kunyesha. Umeishikilia ile mbegu kwa muda mrefu sasa, kwa kuamini, na unamtarajia mtoto atakayekuja, naye anakuja!" Hilo ndilo Kanisa halisi leo, unaona, ile Mbegu teule. "Umekuwa ukimtarajia nami nitamtuma kwako." Nini kilichosema hilo? - Neno.

141 "Ee", unasema, "Huyo hakuwa Neno." Samahani. Abrahamu alimwita Elohim - huyo ni Mwenyenzi Aishiye bila mwanzo wala mwisho. Yeye alikuwa Neno - Elohim. Yeye alikuja wapi? - kwa mbegu ya Abrahamu.

Sasa, kumbuka. Yeye hakuhusiana kwa lolote na madhehebu. Yeye alikaa moja kwa moja na wateule na kuhubiri (hiyo ni sahihi), na kuonyesha ishara. Naye Yesu alisema … Sasa subiri kidogo.

142 Ndipo Sarah, ndani yake mwenyewe - tazama ule uchafu, unaona. Sasa, hakika kwa kutokuamini lile, Mungu angeweza kumuua pale pale. Je, ulijua hilo? Naye akatoka na kumkana Abrahamu. Alicheka kwa ndani, kwa maneno mengine alijicheka katika hali ambayo mtu mwingine asingetambua. Sasa kamwe labda hakutabasamu ila ndani ya moyo wake [Ndugu Branham anaigiza Sara akicheka - Mh.] alicheka kidogo. "Mimi mwanamke mzee, wa miaka mia, miaka hamsini imepita tangu nipite hali ya kuzaa ya mwanamke, wakati wa uhai nimeishi naye miaka hiyo yote. Mbona, hatujaishi kama mume na mke kwa miaka ishirini na tano, labda thelethini, unaona. Na Yeye anasema, nitakuwa na furaha na bwana wangu!" - Abrahamu, mume wake. Hao ndio namna ya wake mnaopaswa kuwa, mngekuwa. Paulo alisema kitu kile kile. Mpende mumeo kiasi hicho. Sio tu kuchanganya mbegu kitu fulani hapa, unaona. Kumbuka mawazo yako. Tutaliendea hilo mchana huu katika wazo la tumbo la uzazi.

143 Kwa hiyo sasa lakini katika hilo, alimpenda Abrahamu sana akamwita bwana wake. "Bwana wangu akiwa mzee, pia, na mimi mzee, nami niwe na furaha pamoja naye tena?" Na Sara … [Ndgu Branham anamwigiza Sara akicheka - Mh.] Na malaika alimwonyesha Abrahamu kuwa Yeye alikuwa Nani, kwamba Yeye alikuwa Neno! Akasema, "Kwa nini Sara amecheka?" Hivyo Abrahamu akamwita aje, naye akasema, "Sikucheka."

Bwana akasema, "Lakini ulicheka!" Nini? Hiyo ni neema. Unaona, pale pale Mungu angemuua, pale pale, lakini asingeweza kufanya hivyo! Unaona upumbavu wetu? Angeweza kuua kila mmoja wetu, lakini Yeye hawezi. Ili amuue Sara, Yeye ingebidi amchukue Abrahamu kwa sababu Sara alikuwa sehemu ya Abrahamu. Wao walikuwa mmoja katika mwungano! Na kuchukua Kanisa na kuliangamiza, Yeye hawezi kufanya hilo, kwa sababu ni sehemu Yake Mwenyewe Kristo, sehemu Yake Mwenyewe, lile Neno likifanyika mwili. Kristo, sehemu Yake Mwenyewe. "Neema ya ajabu, ni sauti tamu jinsi gani." Je unalipata hilo? Hangeweza kulifanya. Mnalielewa? Yeye asingeweza kumuua

Sara. Asingeweza kutoa uhai wake, kwa sababu Sara alikuwa sehemu ya Abrahamu. Unaona, yeye alikuwa nyama katika nyama yake na mfupa katika mfupa wake.

144 Katika makosa yetu … Usiseme, "Vema, nilikosea." Hapana, hilo hali- … Abrahamu alikosea vile vile, unaona. Lakini Yeye hangeweza kuchukua Kanisa. Yeye hawezi kuua Wateule. Yeye hawezi kuchukua uhai wako, kwa sababu wewe ni sehemu Yake Yeye Mwenyewe. Wewe ni Neno. Neno liko ndani yako. Limejidhihirisha Lenyewe, likajithibitisha Lenyewe - upendo, furaha, amani, uvumilivu. Maneno yote ya Mungu, unaamini kila moja - yakitenda kazi, Mungu akitenda kupitia kwako. Unaona, wewe ni sehemu ya Neno ambalo ni Kristo. Na tunafundishwa kuwa Yeye ni Neno, na sisi ni nyama ya nyama Yake na mfupa wa mfupa Wake. Ndivyo ilivyo. Sasa tunakuja kwenye jambo fulani.

145 Moureh, moureh - mvua, mvua ya masika, akidai mvua imekwisha kupita. Sasa, kumetokea nini? Mvua ya masika ilikuwa inapandwa. Mvua ya vuli ikanyesha. Kulitokea nini? - Sodoma na wasodoma wake wakaunguzwa!

Abrahamu akapokea mwana wa ahadi.

Yesu alisema, "Waache wakue pamoja. Magugu yatafungwa vititavitita na kuchomwa. Ngano itakwenda ghalani," unaona. Ile mvua ya vuli iko karibu. Tutapata … Sitaki kusubiri sana juu ya hilo kwa sababu ninalo jambo zuri hasa nyuma hapa juu ya hilo, unajua, unaona.

146 Yale madhehebu mawili yataungana. Pentekoste na haya mengine na yataungana, lakini Neno Atakaa na Mbegu ya ahadi ya Abrahamu kama alivyofanya wakati huo. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa wakati ule …" Mnayo masikio ya kusikia? Macho ya kuona? Ufahamu wa kuelewa? Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa. Je, haikuandikwa," je, Yeye angesema kama Yeye angekuwa amesimama hapa asubuhi hii? Asinge- … je, Yeye asingesema hili: "Je, haikuandikwa kuwa, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa kwenye kuja kwa Mwana wa Adamu." Huoni mavuno mawili yakija hapa? Yakipokea mvua yao ya mwisho. Yamekuja kwenye ile mvua ya mwisho. Unaona? Basi kunatokea nini? Malaika na Bwana wanaondoka. Ndipo mvua iliponyesha.

147 Vema, sasa angalia kwa makini. Sasa, naamini nilikuwa kwenye somo hili hapa; naam, juu ya mvua, na ile ya vu- kwa ajili ya mvua ya vuli. Ishara zote zinaelekeza kwenye mwisho sasa. Kila mtu aaminiye Neno la Mungu anajua hilo. Hata …

Hebu niishie kwenye jingine moja hapa hapa. Nitakwenda kutaja majina. Simaanishi kuwa mjeuri lakini yanipasa … Nimemwambia Mungu sitashambulia. Ningekuja hapa hapa na kueleza tu kile hasa nilichokijua maisha yangu yote, na basi kuna mambo fulani hapa mwishoni nitakayojizuia nisiyaseme, najua, lakini nitaeleza kwenu kadri atakavyoniruhusu kufanya. Kwanza nina- … Bibi Wood anajua kuwa baada ya kuwa na hili na kurasa nyingine zaidi mbali na huu, Roho Mtakatifu alisema, "Usifanye hilo." Je, nilikuita, Bibi Wood, na kusema Yeye aliniambia kuwa nisilifanye? Kwa hiyo nilirudi na kuomba na usiku ule Yeye alinijia katika ono na kusema, "Nenda kwenye hili. Chukua hili na uliweke pale kwa sababu hawataweza kuelewa hili.Sio wakati kwa ajili ya hili; weka hili hapa," na nikafanya hivyo. Hiyo ni sahihi. "Kutii ni bora kuliko dhabihu," unaona.

Vema - kutii.

148 Sasa, sasa tazama, tuko … inakuonyesha tuko kwenye wakati wa mwisho, hata mfano wa mwanamwali mwenye busara na mwanamwali mpumbavu wako pamoja nasi. Sasa tazama, makala isiyo ya busara - mwanamwali (samahani), yule mwanamwali mpumbavu ndiye mbegu mchanganyiko. Unaona, yeye alikuwa na mbegu bila mafuta, unyevunyevu wa kuifanya iote. Sasa, na yeye anafanya nini? Yale makundi mawili, kundi la Kipentekoste na lile dhehebu la kidunia, makundi ya Kiinjili yameibuka pamoja. Unaona? Kwa ajili ya nini? - yanakwenda Sodoma (sasa angalia) kuvuna haya mavuno.

149 Angalia, mwanamwali mpumbavu, mwanamwali. Je, umeshaona hili … hata mmoja wa marafiki zangu wakuu, msomi hasa, mtu mwerevu, mwenye akili nyingi, Mpentekoste mwenye busara … Na niligundua kuwa ndugu zangu walioko katika mikutano ya kiroho ya wafanya bishara Wakristo wanamsifu Mungu kwa shangwe kwa sababu ndani pale wanao wahubiri Waeskopali, mapadri wa Katoliki. Nashangaa kama wale watu wamelala fofofo. Mnatambua … Wanasema, "Ee, ni jambo kuu ulilowahi kusikia, Ndugu Branham. Mbona hawa watu wa kanisa la Episkopali huja pale na kusema

wanaye Roho Mtakatifu. Wananena kwa lugha; wamefanya haya mambo. Utukufu kwa Mungu! Nakwambia, wao ni … Mbona, kanisa lao limebadilika, ″Ee jamani, Ndugu, hamjui hicho ni nini? Hiyo ni ishara.‟.

150 Wakati wanamwali wenye busara wanapotaka mafuta … au namaanisha wanamwali wapumbavu, wanapotaka mafuta, na wakati wanapoyanunua, huo ndio wakati ambao Bwana Arusi anakuja! Ee, enyi Wapentekoste, tatizo ni nini? Vema, hamwezi kuliona hadi Mungu awaonyeshe; hilo ni jambo moja la hakika. Kama hamkuzaliwa nyuma kule, mkachaguliwa tangu asili kwa hilo, mtalikosa. Heri masikio yawezayo kusikia; heri mioyo iwezayo kuelewa, kwani wakati umekaribia. Kila ishara ikiuelekea, unaona.

151 Tazama aina ya miamsho waliyo nayo. Miamsho mikuu wamekuwa nayo. Inaonekana mizuri, sivyo? Unasema, "Vema, Ndugu Branham, sasa umetupatia kwenye ukingo." Hapo ndipo nilikowataka. Mtajuaje lililo jema na baya? Lipime kwa Neno. Hiyo ndiyo njia ya kutofautisha kama ni sahihi au kosa. Ndivyo hivyo; lipime kwa Neno. Angalia jinsi lisemavyo kuhusu Neno. Roho yoyote, tazama kile isemayo kuhusu Neno. Kama inakataa Neno, si ya Mungu. Unaona? Hata kama ikoje, kama inakataa Neno, si ya Mungu. Tazama, ipe jaribio la Neno na uone kitakachotokea. Yesu alituonya juu ya mambo haya - Mathayo ile sura ya 24 na ile aya ya 35. Nataka tu kuinukuu hiyo kwa sababu … kwa ajili ya kanda.

152 Hebu subiri kidogo. Sasa, tumebakiza kama dakika ishirini tu tumalize, na nina hakika hatuwezi hata kumaliza theluthi moja ya somo hili zima, ila yanipasa nisome hili kwa vyovyote vile, unaona. Mathayo 24:35:

Sasa sikiliza kwa makini kile Yesu alichosema. Sasa, jinsi hili … jinsi Yeye alivyotuambia kuwa zile roho mbili zitafanana mno, itawadanganya wale wateule halisi kama ingaliwezekana. Mnajua hilo, sivyo? Sasa, itakuwa kweli? Naam, bwana. Mathayo 24:35 inasema:

Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe.

Sasa, Yeye … kwamba zile roho mbili zitakaribiana mno … Sasa yapasa iwe hivyo. Yapasa iwe hivyo. Dhehebu la Kipentekoste yapasa litende halisi mno kama halisi ilivyo hadi Yesu alisema ni wale walio Wateule tu ambao hawangedanganyika. Hilo lilinishtua kiasi cha kuniua. Lakini ninyi ndugu zangu wa kidhehebu, hamwezi kuona ni kwa nini, kwa nini nimefanya kile nilichofanya? Itafanana sana hata kuwadanganya Wateule kama ingewezekana. Lakini Wateule walioteuliwa kwa ajili ya Uzima wa Milele … Sasa unazungumzia kuhusu kugonga hili, tutaligonga baadaye kidogo, tutaligonga hasa, unaona. Unaona, kumbuka Wateule ndio tu watakaolidaka hili.

153 "Vema," unasema, "unajuaje kuwa hauko sahihi?" Basi nijaribu kwa Neno. Njoo lipime dhehebu lako kwa hili Neno. Hebu tuone ni nani aliye sahihi. "Hakikisha mambo yote," Biblia inasema. Unasema, "Haileti tofauti yoyote; ubatizwe namna hii, ile …" Huwa inaleta tofauti! Hilo ndilo Shetani alilomwambia Hawa.

Mtu fulani tayari ameshabatizwa katika Matendo 19. Mtu mzuri Mkristo pia aliwabatiza, Yohana, Yohana Mbatizaji, Paulo alisema, "Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

Tulisema … yeye alisema, "Hatujui hata kama kuna Roho Mtakatifu."

Akasema, "Basi mlibatizwaje? Kama mngelikuwa mmepata, mngekuwa mnafahamu kuwa mnaye. Mnaona? Alisema. ″Unawezaje … mli- …

mlibatizwaje?‟

Akasema, "Kwa Yohana - mtu mkuu aliyembatiza Yesu."

Paulo akasema, "Huo haufanyi kazi wakati huu." Kwa sababu Yohana alibatiza kwa ajili ya toba tu, sio kwa ajili ya ondoleo la dhambi; Dhabihu ilikuwa bado kutolewa. Na waliposikia hili, walibatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo.

154 Vipi kama Musa alisema … Mungu alisema, "Musa vua viatu vyako"?

Yeye alisema, "Unajua nilivifunga na kuvikaza zaidi asubuhi hii Bwana. Nitaonyesha heshima zaidi; nitaivua kofia yangu." Hilo lisingefaa. Yeye hakusema kofia kamwe; Yeye alisema viatu! Na huyo ni Ibilisi anayejaribu kulipaka chokaa kama yeye alivyofanya na mama Hawa. Ni kila Neno ile Kweli kama tu Mungu alivyoliweka liandikwe pale. Hivyo ndivyo ninavyoliamini.

hakuna uzima ndani yao” - kama wakikataa jambo moja. Basi nionyeshe mtu mmoja aliyewahi kubatizwa kwa kutumia vyeo vya, Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Kwa nini mnalifanya basi? - ungamo, kuchanganya mbegu, watoto waliokufa, wototo haramu, waliokufa maradufu, waliong'olewa tangu kwenye mizizi. “Na kila shina ambalo … kila mti ambao Baba Yangu wa mbinguni hakuupanda utang'olewa.” Yesu alisema, “Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitapita.” Sasa unaona ni kwa nini nimesimama jinsi nilivyo.

161 Nionyeshe sehemu moja, kama si laana kwa mwanamke kukata nywele zake. Ndiyo hivyo. Ndipo unanikasirikia. Basi watu husema, “Ndugu Branham ni nabii. Ee mwamini wakati tu anapoongea na watu, akiwaambia dhambi zao na mambo kama hayo, lakini anapokwenda kufundisha, usiamini hayo.” Vema, ewe mnafiki. Hujui chochote! Je, Biblia haisemi Neno la Bwana lilikuja kwa nabii? Mimi sijajita nabii, mimi sio nabii. Lakini ni ninyi mlioniita hivyo; nasema kile mlichosema. Na ndipo mnageuka na kusema jambo kama hilo. Msiseme hamkusema. Ninayo kanda iliyonasa hayo mliyoyasema. Hamkujua hilo, sivyo? Nataka tu mkanushe kuwa hamkusema wakati mmoja, hilo ndilo tu ntaka mseme. Nitakufungulia kanda usikie sauti yako mwenyewe ikikurudia.

162 Kama Yane na Yambre walivyompinga Musa - watenda miujiza, lakini Neno lilikuwa wapi, Neno la kweli? Kulikuwa na jamaa wakitenda miujiza. Kulikuwa na jamaa ambao wangeweza kufanya kila kitu katika mstari wa miujiza ambao … lakini kulikuwa na manabii wawili waliopakwa mafuta wakisimama pale, au nabii mmoja na msaidizi wake. Kulikuwa na nabii aliyepakwa mafuta aliyeitwa Musa, akasimama pale, alikuwa na HIVI ASEMA BWANA. Na mwishoni, lote lilidhihirishwa - kabla ya ukombozi. Je, hilo ni sahihi? Wale walioitwa watenda miujiza wakafa moja kwa moja.

163 Sasa, kile wanachojaribu kufanya, wanajaribu kutengeneza mvua ya vuli. Upuzi! Mbona, ile mvua ya vuli itafyagia dunia ndugu. Kumekuwa na mvua ya masika ikipanda Neno. Hiyo ni sahihi. Sasa utaona kile ile mvua ya vuli itafanyiza. Utakuta kuwa kutakuwa na ushirikiano. Wapentekoste na makundi yote yataungana, na watawafungia mlango wale jamaa ambao hawatalisikiliza hilo na hata hutaruhusiwa kufungua mdomo wako. Sawa! Hapo ndipo Yeye ataka

pokuja. Hapo ndipo Yeye ataonyesha. Ndipo mtakapoona mvua. Ee, jamani, tulia; kaa kimya; liache liende.

164 Ee, lakini Neno lilikuwa na yule nabii mpakwa mafuta kwa sababu Neno la Bwana lilikuja kwa nabii. Sasa, Mungu habadilishi utaratibu Wake. La, hapana. Kamwe habadilishi utaratibu Wake. Sasa, ilikuwa nini? Kulisimama watatu tena. Kulitoka Yane na Yambre wakitenda miujiza, kama wale waliokwenda Sodoma, wakafanya muujiza mmoja mdogo - kupofusha watu macho, unaona. Abrahamu akasimama kule, mpakwa mafuta, pamoja na Mungu na msaidizi wake Sara. Sawa hilo? Hapa walisimama Yane na Yambre wakitenda miujiza - chochote kile ambacho Musa angefanya katika ishara ya miujiza, ishara - na pale alisimama Neno aliyepakwa mafuta, yule nabii, akiwa na msaidizi wake - msaidizi wake. Ee, natamani ningehubiri juu ya hilo sasa kwa kama masaa mawili.

165 Vema. Katika Mwanzo 1, kumbuka, kila mbegu kwa jinsi yake. Lazima iwe hivyo daima. Kuna mifano hiyo yote. Mtu fulani ambaye angesema, ambaye angeamini, kwamba kanisa litapitia kipindi cha dhiki kuu, nashangaa ungepata wapi mbegu kwa ajili ya hilo? Lini hata … “Vema,” unasema, “Naamini inasema hili kwamba watapitia …” Hilo ni sawa. Je, uliona nyuma kule ambako mvua ilinyesha juu ya aina nyingine? Ilianguka wapi? Nuhu alikuwa ndani ya safina kabla hukumu haijaja. Sodoma - Lutu alikuwa nje ya Sodoma kabla halijatokea. Hakika, hatupitii katika kipindi cha dhiki; unakwenda katika Unyakuo mojawapo ya siku hizi. Hakika. Nini … kwa nini yabidi uhukumiwe? Yeye alisimama mahali pangu pa dhiki - Yesu Kristo. Pale ndipo ilipotokea dhiki kwa ajili yangu, naam. Nilimpokea, na huru - “Nitakapoona damu nitapita juu yenu.” Hiyo ni sahihi. Musa alikuwa salama … alilindwa pamoja na Israeli dhiki kuu ilipoanguka. Hiyo ni sahihi.

166 Vema, kila mbegu lazima ije kwa jinsi yake. Mungu alimfanya mtu kwa mfano Wake. Kwa jinsi Yake awe Neno Lake duniani. Alijidhihirisha katika Yesu Kristo. Ilikuwa nini? - Mungu alikuwa katika Kristo. Huyo ni mtu wa jinsi Yake, unaona? Wakati Mungu ambaye ni Neno … wangapi mnajua Yeye ni Neno? Wakati Neno lilipokuwa ndani ya Kristo, mtu, mtu mwanadamu, likijidhihirisha Lenyewe kupitia Yeye,; hilo lilikuwa

Mungu, Neno, katika Kristo akijidhihirisha Mwenyewe; na Mungu hapo mwanzo alimfanya mtu kwa mfano Wake, na huyo ndiye aina ya mtu ambaye Mungu anamfanya leo. Seminari na sehemu za kuatamia na kuangulia hugeuka kundi la mbegu mchanganyiko. Unaona, mashule. Lakini Mungu amwitapo mtu, yeye yu katika mfano Wake Mwenyewe. - Neno limefanywa hai ndani yake. Hiyo ni sahihi. Yupo hapo; huyo ni mtu wa Mungu. Mtu kwa mfano Wake, kwa sura Yake halisi. Na Yesu alisema, kwamba Yeye atafanya zile kazi nizifanyazo. Kwa hiyo Mungu alimfanya mtu kwa mfano Wake kwa jinsi Yake.

167 Jinsi yake - Jinsi Yake ni ipi? - Neno. Yeye ni Neno. Basi kama mtu akilikataa Neno, awezaje kuwa katika mfano wa Mungu? Nauliza tu swali. Jiulize mwenyewe. Unawezaje kuwa katika mfano wa Mungu na ulikatae Neno la Mungu, wakati Neno ni mfano Wake Mwenyewe uliojidhihirisha? "Ee," yeye anasema, "haimaanishi hivyo." Mfano wa Mungu uliojidhihirisha. Akasema, "Ee, nililisema, lakini sikulimaanisha hasa. Nilikuwa nimekosea pale. Ninalikubali. Hilo lilikuwa kwa ajili ya wakati mwingine. Sikulimaanisha hivyo." Ee, rehema, upuzi, maji machafu ya ibilisi ambayo alimnywesha Hawa. Usimruhusu ayasukumie kwenye shingo ya Mteule. La, bwana. Hawawezi kuamini hilo. "Njoo tu na ujiunge na genge letu." Usijiunge na chochote, yakupasa uzaliwe; sio kujiunga! Kiumbe kipya.

168 Ndiyo, kwa mfano Wake Mwenyewe wa jinsi Yake kuwa … kuwa Neno Lake lililodhihirishwa duniani. Sasa Yesu alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa. Unaamini hilo? Basi yatupasa kuwa nini? - wana wa Mungu, pia, pamoja na Neno lililodhihirishwa katika Kanisa, likiendeleza (huo ni Mwili wa Kristo wa siri), likiendeleza kazi zile zile ambazo Yesu alizifanya alipokuwa hapa duniani. Unaona? Hiyo ni jinsi iliyotokana na jinsi Yake.

Sasa unaweza kuwa na jinsi ya Lutheran iliyotokana na Lutheran; jinsi ya Methodisti iliyotokana na Methodisti; jinsi ya Katoliki iliyotokana na Katoliki; jinsi ya Pentekoste iliyotokana na jinsi yake; wa Umoja uliyotokana na jinsi yake; wa Utatu uliotokana na jinsi yake, lakini ikiwa wewe ni wa jinsi ya Mungu, hilo ni tofauti. Unaona, wewe ni mfano uliodhihirishwa wa Neno likijidhihirisha Lenyewe. Loo jamani! Mbona, Inapasa uwe hivyo. Maji yakianguka juu yake, yapasa lifanye hivyo.

169 Ndipo … basi humpa uzao, mfano wa yeye … baada … Mungu alimfanya mtu kwa mfano Wake. Sidhani nina muda kwa ajili ya msemo unaofuata; ni jambo lenye ubora wa kuvutia, lakini sitaki … Maneno ya Mungu yote yana ubora wa kuvutia, unaona. Na tazama hapa, pale nilipopaswa kuwa kwenye wakati wa chakula cha usiku, niko mbali na kukamilisha somo hili, unaona. Kwenye sehemu moja ya sita. Loo! Vema, naweza … hebu na tuachie hapa. Mnasemaje? Basi tu … Sasa ni wangapi wanaweza kurudi mchana huu? Inueni mikono yenu. Vizuri. Sitaki kuwaweka muda mrefu kupita kiasi. Sasa … Sitaki niwachoshe. Na sasa, mimi … Sasa ninyi vijana mnaorekodi kwenye kanda, acheni kanda ziendelee kwa dakika chache, na nitalimaliza hili kwa muda mfupi mimi mwenyewe. Vema, bwana.

170 Sasa, tu- … wazo letu la mwisho hapa lilikuwa kwamba Mungu alimfanya mtu kwa mfano Wake Mwenyewe aliyetokana na jinsi Yake Mungu. Mungu alimwumba mtu aliyetokana na jinsi Yake Mwenyewe. Mnalielewa?. Mtu kwa jinsi Yake.Vema alikuwa mtu wa jinsi gani? Kama ukiangalia nyuma na kuona kile alichokuwa wakati Yeye alipofanyika mwili, huyo ndiye aina ya mtu anayemfanya. Je, hilo ni sahihi? Mtu aliyetokana na jinsi Yake. Amina. Hiyo ni sahihi, sivyo? Huyo ndiye namna ya mtu Wake.

Wakati mwingine, wakati mmoja Yeye alimwambia mtu mmoja: "Wewe umetokana na moyo Wangu Mwenyewe." Mtu wa aliyetokana na moyo Wake Yeye Mwenyewe - Daudi. Mnakumbuka hilo? Roho wa Mungu ndani ya Daudi, nyakati zote mpakwa mafuta hukataliwa. Daudi, mfalme aliyekataliwa, Daudi alipanda mlimani wakati watu wake mwenyewe … nitahubiri hili katika dakika tatu zijazo. Wakati watu wa Daudi wangekuwa, wa jinsi yake mwenyewe walimwondoa madarakani, mwana wake mwenyewe, na kumtoa kwenye kiti cha enzi. Daudi alishuka kule, na hata mmoja wao akaja akimtemea mate - yule mfalme mpakwa mafuta. Huyu mtu mzee akaja akiwa kiwete katika fundisho lake (Biblia ilisema kuwa alikuwa kiwete, unajua), na akaendelea kumtemea mate yule mfalme. Mtazame Kristo. Wakimtemea mate! Yule tarishi pembeni mwake, akimwakilisha malaika, akavuta upanga na kusema, "Je, kichwa cha yule mbwa kiendelee kuwepo … anamtemea mate mfalme?" Yule malaika akasema, "Nitamuua!"

171 Daudi akasema, "Rudisha upanga wako. Yanipasa nifanye hili." Akakwea juu ya mlima wa Yesrusalemu, akatazama nyuma (mfalme aliyekataliwa) akalia. Miaka mia nane tangu pale Mwana wa Daudi, yule Roho aliyekuwa ndani ya Daudi kwa sehemu, alisimama kwenye mlima ule ule, mfalme aliyekataliwa akitemewa mate na kudhihakiwa. Je, ni sahihi hilo? Naweza kuwazia Mungu alisema, yule malaika alikuwa akitembea pale pamoja Naye wakati Yeye alipokwenda Kalvari namna hiyo: "Je, kichwa cha yule mbwa kiendelee kuwa juu yake?"

"Mwache." Loo, jamani, unakuja wakati.

Lakini vipi kuhusu Daudi aliporudi? Hadithi ilibadilika. Daudi alikuja amepanda farasi akiwa mshindi. Huyu mtu alikuja mbio akililia rehema. Hakika, mwache. Yeye atakuja siku moja katika nguvu. Ndipo kicheko kitageukia upande mwingine. Hiyo ni sahihi, waache tu.

172 Lakini, Mungu alisema, "Daudi wewe ni mtu uliyetokana na moyo Wangu Mwenyewe." Mungu anapomuumba mtu, anakuwa wa jinsi Yake Mungu. Daudi alisema, "Maneno Yako nimeyaficha moyoni mwangu ili nisikutende dhambi." Kitu pekee alichohitaji kilikuwa mvua. Daudi angekuwa sahihi kama angekuwa na ile mvua, lakini Roho Mtakatifu alikuwa hajatolewa bado. Yeye alikuwa na Neno na Neno lilikuwa ndani yake, naye aliweza kulijua; alisema, "Nimelificha moyoni mwangu, Bwana. Haliwezi kuchanua na kutenda kama ambavyo lilipasa kufanya, lakini nimelificha pale Bwana. Nimelificha." Lakini Yesu alipokuja, ambaye alikuwa Neno lililodhihirishwa, alichukua uzima wa mbegu ndani mwake na kuurudisha kwenye Neno sasa. Na kama kikombe cha Daudi kilifurika, vya kwetu vyapaswa kufanya nini? Bila Roho. Amina. Je, Yeye si wa ajabu? Mnampenda?

Yeye ni wa ajabu, ajabu, ajabu?

Bwana wangu Yesu ni wa ajabu?

Macho yameona, masikio yamesikia,

Yaliyoshuhudiwa katika Neno la Mungu; Bwana wangu Yesu ni wa ajabu?

Je, Yeye si wa ajabu? Wangapi wanampenda? Wangapi wanampenda? Loo, Yeye ni wa ajabu.

173 Sasa, inakwaruza marafiki. Inakwaruza mno. Sikupenda kuwa hivyo mimi mwenyewe. Naam, natumaini mnalielewa hilo, unaona. Lakini leo natoa ufafanuzi kwa nini nimefanya yale niliyoyafanya.

Sasa, kwa mchanganuo mdogo kabla hatujaondoka kwa ajili ya chakula cha mchana ni hivi: Nataka mjue kuwa nime- … hili limekuwa sababu yangu, na nia yangu ni Neno la Mungu. Na kusudi langu ni kumpendeza Yeye. Na siwezi kusikiliza kila kitu na kuliamini Neno la Mungu; wala kusikiliza kila kitu na kumpendeza Mungu. Nia yangu ni kujua Neno Lake na kumpendeza Mungu kwa kumtumikia kwa Neno Lake. Sio kwamba nina chochote kilicho kinyume … Sasa kila mtu aliyepo hapa ndani aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu aliye katika kundi la Wateule labda wakati mmoja alikuwa Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresibiterian, Mpentekoste, au kitu fulani au vyovyote mahali fulani. Sasa, mnajua hilo. Mnajua hilo. Kwa hiyo basi, mnaona unaposema, "Waendee," hilo ndilo likupasalo kutenda. Kuna mtu fulani ndani kule kama ukipanda mbegu; kutakuwa na mavuno siku moja. Itaanguka … Baadhi yake itarudi na kusema, "Ah yeye si lolote ila … yeye ni mdanganyifu." Je, hawakusema kitu kile kile kuhusu Bwana wetu? "Hakuna lolote kwenye hilo." Vema basi, kwa nini huniulizi? "Yeye si lolote ila muongo." Basi liangalie kwa Neno. Unaona, kama sio Neno, basi linadanganya, unaona. Sasa, kama thiolojia yako inatofautiana na Neno, basi haiko sahihi.

174 Sasa, wengine watapita na kusema, "Vema, unajua nini, naamini nitalijaribu jambo hili kwa kitambo kidogo." Atakabwa. Hiyo ni sahihi. Lakini unapoondoa yote kutoka ndani yako, useme "Bwana Yesu, kuanzia sasa na kuendelea sio mimi tena, bali wewe." Basi litazaa mara mia. Unaamini hilo? Nami naliamini pia. Lakini pamoja na uhuru na haki kwa wote. Hiyo ni sahihi. Naam, bwana. Naweka reheni utii wangu kwa Bwana wangu, unaona, kuhubiri Neno Lake na kusimama juu ya Kweli Yake ikiwa itagharimu uhai wangu. Nitaendelea tu hivyo hivyo.

Kwani nita- … litakuwa jambo kuu kwangu, sio kutaka kulifanya, ila kama inanipasa kulifanya, nitamwaga damu yangu katika dunia hii kama wale waliokufa katika matundu

ya simba; kama wale waliokufa juu ya misalaba; wale waliopasuliwa vipande kwa misumeno - wale waliofukuzwa kutoka mashirika yao ya dini na kutangatanga wakiwa wamevaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, na wakiwa fukara. Itakuwa heshima kubwa kwangu kama wale wanafunzi wa Kristo waliporudi na yote kuhesabika kuwa furaha kwa sababu waliweza kukabili shutuma iliyoletwa kwenye Jina Lake. Wangeteseka hivyo kwa ajili Yake, kuteseka kwao kidogo. Sitaki kuteseka; hakuna mtu anayetaka kuteseka. Ningependa kuunganisha mikono yangu na madhehebu yote na kusema, "Ndugu twendeni." Ningependa kufanya hilo. Ikiwa nitalifanya, natoa mkono wangu kwenye mkono Wake Mungu. Kufanya hivyo kuwe mbali na mimi daima. Kama nitasimama mwenyewe, nasimama na Yeye na Neno Lake.

175 Kama Eddie Pruitt alivyosema, "Nasimama juu ya Kristo, aliye Mwamba imara; ardhi nyingine yoyote ni mchanga unaodidimia." Na Kristo Ndiye Neno. "Hapo mwanzo …" Na ni kitu gani? Kila neno huleta … kila mbegu huzaa kwa jinsi yake. Mbegu ya kidhehebu itazaa kwa jinsi yake. Shirika la Kipentekoste litazaa kwa jinsi yake. Baptisti litazaa kwa jinsi yake. Ni kitu gani? - shirika, daima, daima.

Tutakwenda kulionyesha mchana huu, Bwana akipenda, jinsi walivyoanza, na nini kililisababisha, na wapi Biblia inasema wangeazisha, na jinsi watakavyoishia - mwisho utakuwaje hasa.

176 Mungu awabariki wote mlioko katika magari. Wengi wenu mlioko ndani ya magari ambao hamkuweza kuja ndani, mnaosikiliza kupitia hiki kipaza sauti. Na Mungu awabariki mnaosimama kuzunguka hizi kuta na ninyi mliokaa hapa asubuhi hii. Na naamini kuwa kwa neema za Mungu, sijaleta maudhi yoyote. Lakini najiweka wazi mimi mwenyewe.

Sasa, kama unaamini jambo hilo ambalo nimelisema asubuhi hii, je hungeweza kusimama hivyo hivyo? Hakika utaweza. Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi.

177 Baba wa mbinguni wa rehema, hatujaribu kufunga mkutano ila kuusimamisha kwa mapumziko kidogo kwa muda mfupi. Na sasa hizi mbegu zilizopandwa asubuhi hii, na ziwe zimeanguka juu ya udongo mzuri wenye rutuba. Na zizae kwa wingi, Bwana, wingi wa Uzima wa Milele. Sasa tunaomba, Baba, kwamba hizi mbegu zilizopandwa zitakaa zikisubiri mvua ya vuli kunyesha. Wakisubiri - wale wangojeao Bwana, watapata nguvu upya. Mungu, na tusipite mbele ya Neno; tukae na Neno. Tujalie Bwana.

Tubariki sasa na wale wanaoondoka kwenda kula, naomba uwape chakula chao cha mchana na ubariki chakula chao na uwape nguvu na kuwarudisha mapema kabisa mchana huu. Bwana, hebu wawe wameketi hekaluni hapa wakisubiri. Na hebu Bwana unisaidie ninapokwenda kuomba na kurudi. Naomba kwamba uende kunipaka upya mafuta mchana huu. Nijalie Bwana, kwamba niweze kuleta kile ninachoamini kuwa Neno Lako kwa watu. Nijalie Baba.

178 Naomba kuwa utambariki mpendwa wetu mchungaji, Ndugu Neville, ndugu yetu wa thamani - dakika chache zijazo ataingia majini hapa na kundi la watu waingie katika ubatizo. Na, Baba, kama kuna yeyote hapa asubuhi hii aliyebatizwa tofauti na ubatizo wa Kikristo ule wa mtumishi Wako mkuu Paulo - naye alisema kuwa alikuwa na Neno la Mungu ndani yake - naye alisema "Ikiwa mwanadamu au malaika (hata malaika akishuka kutoka Mbinguni, kama Shetani alikuwa katika umbo la malaika) akija na kusema lolote tofauti na lile alilosema, na alaaniwe." Baba, tunajua kuwa hilo limeandikwa katika Maandiko, na naomba, Baba, kwamba lita- … litazama mioyoni mwao kuwa Paulo alikuwa ndiye hasa aliyefanya watu ambao walikuwa hawajabatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao, yeye ndiye aliyewaagiza wao kubatizwa tena. Hebu hilo liende kwa watu Baba. Hebu watambue kuwa hii ibada ya ubatizo itakayofuata mara - hebu watambue kuwa hiyo ni Kweli, wakijua kwamba hawawezi kuleta hata neno moja katika Maandiko kuthibitisha wazo lao la mungu aliye na nafsi tatu Baba, bila shaka tunaamini utatu wa ofisi Zako - wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Kwa hakika mno tunaamini hilo, Bwana, lakini sio kukufanya wewe kuwa miungu watatu; kukufanya Wewe Mungu mmoja anayehudumia ofisi tatu - Ukiwa vyote Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, na Jina la huyo Mungu aliitwa Yesu Kristo. Sasa hilo ndilo Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

179 Baba, hebu watu walione hili na watii ubatizo wa maji kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao. Na hebu haya maneno machache kwa ajili ya ubatizo yaanguke kwa kina

sasa ndani ya moyo wa kila mmoja, kwani hatujui tunao muda mrefu kiasi gani uliotubakia, Baba. Mwisho unakaribia sana. Adui, kama tunavyotarajia kuzungumza juu yake mchana huu, anatanuka zaidi, anazidi kuwa mkakamavu wakati wote. Tangu wachukue kiti cha enzi, wameendelea moja kwa moja mbele hali wamekikalia. Bwana, tunaliona kila upande. Sio Ukomunisti, Bwana. Hebu watu waweze kuelewa kuwa huo ni Utawala wa kiroho wa Kirumi, mama kahaba mkuu wa zamani na makahaba wake; na tunawaona, Bwana, akiwa sanamu ya mnyama na tuko hapa.

Baba Mungu, turehemu sasa, na hebu sote tuingie kwenye usalama, katika safina na tuwe tayari kwa ajili ya mvua ya vuli. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

180 Sasa kwenu ninyi mlioko hapa katika jengo hili, sasa kama mnataka kutoka nje na kupata chochote cha kula, vema. Na kama mnataka - na kurudi. Ingieni hapa haraka tu mwezavyo baada ya huduma. Sasa, hebu tusimame kwa muda mfupi. Hebu tusimame sote. Wangapi wanaamini Neno la Bwana, inueni mikono yenu. Amina. Ee, mshukuruni Bwana. Oh jinsi ninavyompenda Yesu.

O, jinsi ninavyompenda Yesu;

O, jinsi ninavyompenda Yesu; (Ndugu Branham anaombea leso)

O, jinsi ninavyompenda Yesu; Kwani alinipenda kwanza

181 .Neno Lililonenwa Ndiyo Mbegu Ya Asili

Kila mtu anajisikia vizuri sasa? Vema. Sasa, tutaanza moja kwa moja sasa hadi usiku wa manane, na ndipo tuta- … Tuna furaha mno kwamba Bwana anatusaidia na kutubariki.

Sasa, kabla hatujaanza tena, hebu tuwe tu na neno kidogo la maombi kwa Huyu Mmoja Ambaye tunamzungumza Naye.

182 Baba wa Mbinguni mwenye rehema, unasikia ushuhuda wa huyu mtu mzee mtauwa, mtakatifu. Katika nyakati yeye na mke wake, wakifanya kazi pamoja, na jinsi mke wake alivyoweza kukushikilia na kukuomba Wewe umfanye mume wake awe mhubiri, Naye yuko hapa sasa akiwa mhubiri. Na ndipo alipokuwa amelala pale akifa, madaktari wazuri kuliko wote nchini wakisema kuwa amekwenda, "Hawezi kuishi ila kwa masaa machache. Amekwisha; mwili wake umeliwa na kansa."; hangeweza kutembea hatua nyingine kamwe- maambukizo kwenye vifundo vya miguu na kadhalika yamemmaliza. Na yupo hapa, miaka kadha baadaye, bado akitembea. Tunakushukuru mno Baba. Inathibitisha kuwa Neno linapopandwa, na kunyeshewa, litazaa mazao.

Sasa tunaomba, Baba, kwamba utaturuhusu tuyaweke kwa mpangilio mchana huu maneno yanayotoka kwenye Neno Lako,. Hili ni Neno Lako, na tunataka kuliweka kwenye mpangilio kama tu jinsi lilivyo, na ndipo ulimwagilie maji, Bwana, kwa Roho. Tunaomba, tunapojisalimisha wenyewe Kwako pamoja na Ujumbe, kwamba utatutumia katika Jina la Yesu. Amina.

183 Sasa kwa kuharakisha. Mke wangu alikuwa akiniambia asubuhi hii kuhusu jinsi ilivyo ngumu watu … unajua, na miguu yao ikilemaa na mambo- wanawake, na watu wengi kama mimi wakizeeka na kuwapasa kusimama namna hiyo. Nalithamini hilo- uaminifu wenu. Na sasa, tutakwenda moja kwa moja kwenye Ujumbe na kuendelea. Sitaki kuharakisha sana, na bado nataka kuharakisha vya kutosha kujaribu kulimaliza mchana huu kama nitaweza kumaliza. Ndipo mara tumalizapo tunakwenda moja kwa moja Tiflon, Georgia, sio kwa ajili ya … mkutano wa kuendeleza; tuko kwenye ukumbi wa shule ya sekondari ya juu pale kwa usiku mmoja tu. Hiyo ni kesho usiku, na ibada ya mahubiri tu; na nitakuwa na somo dogo la kawaida au jambo nililohubiri hapa hapa kwa sababu ni kutembelea watu tu kule. Hawajawa na utaratibu wa kawaida wa kuwa na mikutano au chochote.

184 Kwa hiyo, sisi … na sasa tuna … tuliachia asubuhi hii tukiongea juu ya somo letu lililopatikana katika Mwanzo sura ya kwanza, aya ya 11, zaidi: Neno Lililonenwa Ndiyo Mbegu ya Asili. Na sasa kusudi langu asubuhi hii na leo ni kujaribu kuwaeleza watu- kujaribu kuwaeleza watu juu ya matendo yangu sasa, kwa nini nimefanya mambo niliyoyafanya. Na kwa kutambua kuwa hizi kanda zinanaswa na zitapelekwa nje; watu wengi inaelekea watakuwa wanazisikiliza baada ya mimi kuondoka duniani, ikiwa Yesu atakawia kurudi; lakini nataka kusema kuwa naamini Neno la Mungu, kuwa … kuwa ni Kweli.

185 Sasa tuliachia pale ambapo … juu ya siku za mwisho. Nini kimetokea kwenye huduma … ya wainjilisti wale ambao miaka michache iliyopita walikuwa wakiwasha moto nchi na inaonekana kana kwamba wote wameacha tu. Sasa, simaanishi wametoka shamba la huduma. Bado wanaendelea, bali hakuna matokeo, inaonekana hivyo. Hawafiki popote. Unaona? Tatizo ni nini?-shamba limepandwa mbegu, unaona? Sasa kumbuka, usisahau …

186 Mtu mmoja aliniambia nieleze tena lile neno la Kiebrania tena. Katika Yoeli sura ya 2 (Yoeli 2:28) pale ambapo ananena juu ya kuja kwa mvua ya masika na ile ya vuli, neno masika ni neno la Kiebrania m-o-u-r-e-h, moureh, ambalo maana yake ni kufundisha. Kwa maneno mengine, itakuwa mvua ya kufundisha na mvua ya mavuno. Sasa tumekuwa na mvua ya kufundisha, na sasa tuko tayari kwa ajili ya mvua ya mavuno. Unajua mvua ya kwanza ni pale ambapo unapanda mbegu. Ile inaanzisha kukua kwa mazao yako. Ndipo kabla hata hayajakomaa, kunatokea zao lingine. Hiyo ndiyo wanayoita mvua ya mavuno. Tunajua inapokuwa-mvua za majira ya kuchipua, na ndipo inanyesha kwenye mwezi wa Juni, inakuza mazao yako.

187 Sasa, mvua tuliona kuwa ilikuwa ni Roho. Na sasa tuliachia pale nilipotoa mawazo yangu kuhusu jambo lote litakavyokuwa. Hilo ni, naamini kuwa ile … kuwa ile mvua imekwishaletwa - ile mvua. Hiyo ndiyo sababu tumenyamazishwa, kwa sababu ardhi tayari imepandwa mbegu. Si rahisi upapate mahaliambapo hapajapandwa mbegu. Na imekwenda kupitia redio, televisheni, kanda za kunasia sauti, neno, kila kitu; imepandwa nchini kote. Nchi imepandwa mbegu. Sasa ni mbegu gani zilizopandwa, hutaweza kupata kitu kingine chochote kutoka kwake isipokuwa zile mbegu zilizopandwa mwanzo. Unaelewa sasa? Itakuwa ni mbegu zile zilizopandwa. Roho atashuka, ila Yeye ataleta mavuno ya zile mbegu anazoshuka juu yake. Sasa kumbukeni.

188 Vema, nabashiri kuwa yale makundi mawili ya kidhehebu, Pentekoste na makundi ya Kiinjili, yatafanya kazi pamoja katika dhehebu, yataungana pamoja, na yatakuwa washirika (yote) wa Baraza la Muungano wa Makanisa au Baraza la Makanisa. Tayari wao ni washirika wake-wote. Na kwa njia ya wao kutakuja ulazimishaji au ususiaji, ambako kutakomesha kila kitu isipokuwa kile kilicho cha ule muungano wa makanisa. Hicho ndicho … Biblia ilisema kuwa kungekuwa na ususiaji, hata kwa njia ambayo itawafanya watu wasinunue wala kuuza hadi wawe wamepokea hii Alama ya Mnyama, ambayo ni Dini ya Kirumi, na alama ya mnyama, ambayo ni Uprotestanti, ambayo alama … mnyama na uwezo, mamlaka ili kumpa ile alama uhai wa kunena, na ilifanya hivyo. Na hilo ndilo Shirikisho la Makanisa wakati wanapojiunga pamoja.

189 Sasa kuna vijana wengi hapa. Sijui Yesu anaweza kuja mchana huu; Anaweza kuja mwaka ujao. Sijui Yeye atakuja lini. Ila kumbuka, kama sitaishi hadi niione ile siku ya kuja Kwake-ambayo natumaini nitaiona, na kwa namna fulani anaamini nitaiona-sasa kama sitaiona, usiache hili Neno litoke masikioni mwako na moyoni mwako. Kumbuka tu, nasema katika Jina la Bwana. Sasa, naamini kwa moyo wangu wote, hivyo ndivyo jambo hilo litakavyoishia. Kutakuwepo na muungano, ususiaji. Sehemu zote kama hii hapa zitafungwa. Na hamtaweza kusema hadi mpate kibali au leseni toka kwenye hili shirikisho la Makanisa ili muweze kuwa kufanya ibada.

190 Ni karibu … inaonyesha kuwa inatenda hilo hata katika madhehebu. Inaonyesha mambo yalikofikia. Naam, bwana, inakupasa uwe nacho. Na hapo ndipo litakapoishia. Huo ni ubashiri wangu, nikiwa mtumishi wa Kristo katika ufahamu nilio nao wa Neno na uvuvio; hapo ndipo litakapofika. Ile … Ishara zote zinaelekeza mwishoni. Ni hivi karibuni tu nilimaliza kuhubiri juu ya hilo.

Na hata wanawali wapumbavu wameanza kulilia mafuta. Sasa kumbuka, yeye alikuwa bikira, na ikiwa yeye ni bikira, yeye ni kanisa. Unaona, tutafikia hilo mchana huu katika Ufunuo 17. Ikiwa yeye ni bikira, yeye ni kanisa, kwa sababu kanisa ni bikira. Paulo alisema, "Naliwaposea Kristo mkiwa bikira safi." Yule kahaba wa Ufunuo 17 alikuwa kanisa. Yohana alimstaajabia kwa sababu ya … ya uzuri wake, kile alichokuwa; yeye alikuwa kitu kizuri, hata hivyo ndani yake ilikutwa damu ya kila mtakatifu wa Yesu Kristo-walikuwa wameuawa katika yeye. Hiyo ni sawa.

191 Naamini ni milioni 68 katika kitabu cha kumbukumbu ya wafia imani ambao Kanisa la Katoliki la Rumi liliwaua tangu siku za Mtakatifu Augustino wa Hippo. Waprotestanti milioni sitini na nane wameuawa na kuwekwa kwenye kumbukumbu ya wafia dini na Kanisa Katoliki kwa sababu ya kutokukubaliana na fundisho lake. Haistaajabishi Biblia

iliposema, "Ndani yake kuna damu ya kila mfia imani."

Sasa, sasa Yesu hakusema wakati ungekuja ambao wangewaua ninyi, huku wakidhani walikuwa wanamtendea Mungu kazi; na dhamiri zao zikiwa safi kuhusu hilo. Wao sio wanafiki. Wanaamini hilo; wanafundishwa hilo. Na wakati lile Neno … Neno linapopandwa pale, inabidi lilete mazao. Hakika inabidi kuleta. Kumbuka, tunakaa na Mbegu. Hilo ndilo somo letu-Mbegu yetu. Neno la Mungu lililonenwa ni Mbegu Unaona? Yalipasa lirudi kwenye Neno, na lile Neno litazaa kile linachosema.

192 Hiyo ndiyo sababu naamini uponyaji wa Kiungu; hiyo ndiyo sababu naamini maono; hiyo ndiyo sababu naamini Malaika, hiyo ndiyo sababu naamini huu Ujumbe, ni kwa sababu unatoka kwenye Neno la Mungu. Na chochote nje ya Neno la Mungu, sikiamini. Kinaweza kiwe hivyo, lakini bado nitakaa tu na kile Mungu alichosema na ndipo niwe na hakika kuwa niko sahihi. Sasa Mungu anaweza kile Yeye apendacho; Yeye ni Mungu. Lakini ili mradi nakaa na Neno Lake, basi najua hiyo ni sawa. Na naamini hilo.

193 Sasa, huyo mwanamwali mpumbavu ni mwanamke, yeye ni kanisa, lakini ni mpumbavu. Unaona? Yeye amekuwa tu mzembe. Na hata hivyo anaitwa … yeye mwenyewe anajiita bibi arusi. Na kumbuka kila kitu kinakwenda katika tatu kwa ajili ya ukamilifu. Tatu ni tarakimu ya ukamilifu. Ofisi za Mungu - Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Mungu Baba, alikuwa Mungu aliyekaa katika ile Nguzo ya Moto. Alikuwa anajaribu kuwavuta Israeli waje Kwake. Hawakuja. Mungu, aliye Baba, aliishi katika Mwana, ambalo lilimfanya Yeye Mungu Mwana-Mungu yule yule, sura ya Mungu iliyodhihirishwa, Mbegu ya Mungu iliyodhihirishwa, akijaribu kuwavuta watu waje Kwake-wakamsulubisha. Roho Mtakatifu ni Mungu yule yule ambaye hapo mwanzo alikuwa ndani ya Mwana wa Mungu na sasa hapa ofisi nyingine ya Mungu katika siku za mwisho, akiishi katika kanisa, akijaribu kuleta Neno kwa watu (Neno lililonenwa kama zile ofisi mbili nyingine zilivyofanya), na wanalikataa. Ni jambo lile lile. Ni ofisi tatu au madhihirisho ya Mungu mmoja katika utendaji. Na Mungu katika watu Wake leo ni Mungu katika utendaji. Unaona? Ni Mungu katika watu.

194 Bwana akipenda, nataka kunena juu ya hilo kesho usiku-Mungu katika anga Lake, Mungu katika Mwana Wake, Mungu katika watu Wake, na kadhalika. Sasa nimekwishawahi kulihubiri hilo hapa, hapo awali, naamini.

195 Sasa basi, huyu mwanamwali mpumbavu alipokwenda kununua mafuta- alitumwa kununua mafuta. Alipokwenda alikuwa amechelewa kupita kiasi. Kwa nini? Kwa nini, marafiki?-mbegu zimeshapandwa. Kulikuwa na watatu wakati ule wa Sodoma. Siku zote kumekuwa na hesabu ya watatu kila wakati. Kuna kuja mara tatu kwa Kristo. Yeye alikuja mara ya kwanza kumkomboa Bibi Arusi Wake. Safari inayofuata Anakuja katika Unyakuo kumnyakua Bibi Arusi Wake. Anakuja tena katika Utawala wa Miaka Elfu pamoja na Bibi Arusi Wake. Kila kitu ni katika tatu tatu. Tatu ni tarakimu ya ukamilifu. Tano ni tarakimu ya neema. Saba-ukamilisho; kumi na mbili - abudu; ishirini na nne … au arobaini-kujaribiwa; na hamsini ni yubile. Neno Pentekoste hasa humaanisha yubile-hamsini. Unaona?

196 Sasa, na sasa Mungu katika tarakimu Zake, Yeye ni mkamilifu katika tarakimu Zake; Yeye ni mkamilifu katika Neno Lake; Yeye ni mkamilifu katika utendaji Wake; Yeye ni mkamilifu katika kila kitu kwa sababu Yeye ni Mungu mkamilifu. Na tunaona kuwa katika hawa wanawali-sasa tazama, pale anaitwa Kahaba mkuu katika Biblia. (Sasa, nataka dada zangu waniwie radhi. Ni … Hicho ndicho Biblia inachosema. Leo nanena tu wazi.) Humwita Kahaba mkuu mama wa makahaba, ambayo ni kitu kile kile.

Sasa, kama utaona, kuna kahaba mkuu aliyenenwa katika Biblia (hilo ni kanisa) Kahaba aliyenenwa katika Biblia (hilo ni kanisa), na Bibi Arusi aliyenenwa katika Biblia ni hilo Kanisa. Hapo kuna watatu. Tutayafikia baadaye kidogo kuonyesha wale bibi arusi ni wa nani na jinsi gani wamekataliwa na yote kuhusu hilo Bwana akipenda.

197 Sasa, jambo la kwanza … nataka niseme hili kabla sijalisahau. Kamwe msiogope Ukomunisti. Ukomunisti unafanya kazi tu katika mikono ya Mungu. Ni mfumo wa uovu kama tu alivyokuwa Mfalme Nebukadneza, lakini Yeye alimtuma kule na kuwaondoa Waisraeli kutoka nchini kwao kwa sababu ya kutokutii kwao. Nabii alipowaambia kilichokuwa kinakuja na kuwaambia wakae katika nchi yao na kumkumbuka Mungu, hawakufanya hivyo; waliendelea tu vyovyote vile, na mfalme akaja moja kwa moja na kuwapata hata hivyo, kwa sababu yeye alisema yeye angekuja. Ukomunisti ni kitu ambacho … Sababu Ukomunisti ukainuka ni kwa sababu ya Kanisa Katoliki kuenenda

kinyume cha sheria huko Russia. Walichukua fedha yote na wakakusanya kila kitu na kuficha, na hicho ndicho tu walichofanya. Na hicho ndicho hasa kilichounda Ukomunisti.

198 Wakati yule mvulana mdogo alipofufuliwa kule Finland, wale maaskari wakuu wa Kikomunisti wakiwa wamesimama pale wakinipigia saluti nilipowapita, na machozi yakitiririka mashavuni mwao walisema, "Tutampokea Mungu kama huyo"-hakika, Mungu awezaye kufufua wafu na kusimamia Neno Lake, hakika. Unaona? Lakini inapokuja kuwa ni kwenda kanisani tu na kuishi kama Shetani na kila kitu kingine, kama wengine wote walioko ulimwenguni wafanyavyo, bila kuonyesha matendo yoyote, basi hawataamini kitu hicho. Na nikisema kwa unyofu wa moyo, hata mimi siuamini. Hiyo ni sawa. Hiyo ni sawa. Hakuna Andiko linalosema Ukomunisti utatawala dunia, ila kuna Andiko na Maandiko yote husema mfumo wa dini ya Kirumi utatawala dunia. Kwa hiyo weka jicho lako hapo.

199 Tazama usiku huu; tazama tu kilichotokea hata usiku uliopita - huyu mbunge wa Kentucky alisema kuhusu kuwa na M-Republic katika-katika kiti juu kule sasa akiwakilisha jimbo la Kentucky na kusema, "Yeye ni Mprotestanti na uprotestanti haumaanishi lolote kwake"-ni Mkatoliki.

Wanakuwa wajasiri wawezavyo. Na kumbuka, kuna mambo mengine yanayoambatana na hilo. Wakati wa wanawali wapumbavu-tunaliona hilo. Mambo yale ambayo haikuwahi kutokea kamwe-kuwa mtu yeyote miongoni mwao; walimu katika vipindi vyote wangeweza kusema haya mambo kama tunavyoweza kusema sasa, kwa sababu yapo hapa.

200 Sasa, wanawali wapumbavu na mbegu iliyochanganywa ya Kipentekoste (hilo ni jambo lile lile - kuchanganya na mambo ya ulimwengu) … Sasa kumbukeni, mimi ni Mpentekoste, lakini si Mpentekoste kwa dhehebu. Nalichukia hilo. Mimi ni Mpentekoste kwa matendo. Lazima tuwe na … Wamethodisti ni Wapentekoste; Wabaptisti ni Wapentekoste; Wakatoliki ni Wapentekoste kama upentekoste wenyewe umetendeka maishani mwao. Huwezi kufanya Pentekoste kuwa shirika la dini kwa sababu ni tendo la ndani, na ni Mungu, na Mungu hawezi kufanywa shirika la dini.

201 Sasa … sasa, Yesu alituambia hayo mambo yangekuja, sasa … alituambia kuhusu yale ambayo yangetokea-mwanamwali mpumbavu angeinuka na yale mambo ambayo angefanya, na jinsi watu wangepiga kelele katika siku zao na kutaka mafuta lakini wangekuwa wamechelewa kupita kiasi hata wasipate. Unaona? Sasa tazama hao watatu … yale makanisa matatu. Ndiye huyo malaya hapo; hakuja bila sababu. Sasa yeye hujifikiria mwenyewe nafsini mwake. Ndiye huyo mwanamwali mpumbavu, ambaye ni kanisa la

Kiprotestanti. Na kulikuwa na Bibi Arusi, unaona? Sasa, hizo ni hatua tatu za kanisa katika siku za mwisho. Sasa tazama, tutazileta moja kwa moja nje na kutoka Kitabu cha Mwanzo na kuzileta hapa na kuziweka katika nafasi yake katika kitabu cha Ufunuo katika ule Unyakuo, Bwana akipenda.

202 Haya mambo yote yanaonekana kama ni kitu halisi cha kweli. Pentekoste inaonekana kama ni kitu halisi cha kweli . Wanafikiri wana …

"Kwa nini mimi ni wa shirika la Pentekoste?" Hiyo haimaanishi lolote zaidi kuliko ungeishi katika zizi la nguruwe! Isingeleta tofauti yoyote. Isinge- … Ni shaba iliayo na upatu uvumao. Naam, haidhuru wewe ni wa wapi, kama hujazaliwa kwa Roho wa Mungu na kupokea Roho Mtakatifu - na sababu - ikiwa hujampokea-huamini Neno lote la Mungu, bado hujampokea Roho Mtakatifu. Vema. Hiyo ni sahihi kabisa. Roho Mtakatifu-Unapoisikia ile Kweli, na Roho Mtakatifu hakuongozi kwenye Hiyo, basi kuna roho nyingine ndani pale inayokuweka mbali Nalo. Kwa hiyo ile roho uliyo nayo ndani siyo Roho Mtakatifu.

203 Vema, sasa tunakuta kama-tuliendelea kusema kama Yane na Yambre walivyompinga Musa (tulizungumza kuhusu hilo), jinsi gani haya mambo yangekuwa katika siku za mwisho. Sasa, na nukuu ya mwisho tuliyokuwa nayo ilikuwa kwamba Mungu alifanya kila mbegu kwa jinsi yake; ile iliyo Yake, unaona. Ndipo wakati Yeye alipomfanya mtu Wake kwa mfano Wake- alikuwa mbegu ya Neno Lake. Na Yesu alipofanyika mwili, Yeye alikuwa mwili wa Neno la Mungu. Na tunapolipokea Neno la Mungu, ndipo tunakuwa Neno la Mungu katika mwili wetu, unaona? Yapasa kanisa liwe katika hiyo hali.

204 Sasa, ndipo baada ya Yeye kumfanya mtu kwa mfano Wake-"kwa mfano wa Mungu alimuumba mtu …" sasa baada ya Yeye kufanya hili (sasa usilikose hili), baada ya Mungu kumfanya-mtu Wake kwa mfano Wake Mwenyewe kwa Neno Lake Mwenyewe lililonenwa-sasa yule alikuwa mtu mkamilifu, lakini pale anguko lilipokuja, ilikuwa pale Yeye alipochukua toka kwake zao lililotokana na uumbaji na kumfanyia bibi arusi. Hapo ndipo tatizo liliko sasa. Kama ungekuwa wa kiroho, tayari ungekwishalipata hilo, unaona? Yeye- Haikuwa Adamu aliyeingia katika matatizo. Haikuwa Adamu aliyelishuku Neno; ilikuwa bibi arusi wake aliyelishuku Neno. Na sio Yesu aliyelishuku Neno, kwani Yeye alikuwa Neno; ni bibi arusi Wake.

205 Pale ndipo kuchanganya mbegu kunapokuja-hakukuja kupitia Adamu. Aibu kwenu ninyi ambao hamlioni hilo! Sio kosa la Adamu. Hakuhusika na hilo. Kama kifo kilitokana na Adamu, basi kilitokana na Mungu. Kifo kilikuja kwa kuchanganyisha mbegu. Kifo hakiwezi kuja kwa Neno la Mungu. Kifo huja kwa kulichanganya kwa njia ya dhehebu na maungamo ya imani. Badala ya Kristo, maagizo ya dhehebu - badala ya Neno. Kifo hakiji kwa njia ya Neno. Neno ni Uzima. Yesu alisema, "Maneno Yangu ni Uzima," na Roho huhuisha lile Neno na kulifanya Uzima. Kulichanganyisha, pale ndipo kifo kinapotokea. Na kama Adamu, yeye akiwa Neno la Mungu, Neno Lake lililonenwa, Mbegu Yake ya asili (kwani yeye alikuwa wa kwanza pale … kwa uumbaji), basi Adamu Wake wa pili alikuwa pia kwa uumbaji (Neno lililonenwa). Mnaelewa? Sasa Adamu hakudanganya … hakudanganywa lakini bibi arusi wake alidanganywa. Kristo leo hii hadanganywi. Neno halidanganyi. Ni bibi arusi ndiye anayedanganya kwa kutumia Neno. Unaliona?

206 Sasa, Yeye alimpa Adamu bibi arusi-mfano wa Adamu wa pili. Yeye alimpa Adamu wa kwanza bibi arusi; bibi arusi akaanguka. Akampa Adamu wa pili, Kristo, bibi arusi; huyo bibi arusi akaanguka. Hiyo ni sawa kabisa. Kwa nini?-huyo bibi arusi si yule wa asili, yeye ni zao lililotokana na uumbaji wa asili. Bibi arusi leo ni zao lililotoka katika uumbaji wa asili. Unaona, yeye anajiita mwenyewe kuwa ndiye bibi arusi. Lakini kile alicho, ametengenezwa kwa mali ghafi ya shirika la dini, sio kwa Neno-liko Neno ndani yake kiasi cha kulifanya liwe kitu kama zao linalotokana na Neno, na kulifanya la kinafiki. Hawa aliamini sehemu kubwa ya Neno, lakini alishuku sehemu Yake moja. Leo hii hawezi hata kuelewa Matendo 28 … au Mathayo 28:19 ikilingana na Matendo 2:38. Unaona? Linamchanganya. Hiyo ni sehemu moja ndogo kati ya nyingine mamia.

207 Sasa, yule bibi arusi wa Adamu alikuwa mfano wa bibi arusi wa Adamu wa pili. Sasa, bibi arusi wa Adamu-bibi arusi wa Adamu hakuweza kusubiri. Mungu alikuwa amewaambia Adamu na Hawa: "Mkaongezeke na kuijaza nchi." Lilikuwa jambo ambalo lingekuja-ahadi. Hawa bado hakuwa mke wake kwa sababu Adamu hakuwahi kuishi naye. Bibi Arusi wa Kristo bado hajawa Mke Wake; karamu ya arusi yapasa iwepo. Unalielewa? Angalia, ee hili ni jambo la kina sana! Hawa aliharakisha, naye alifamya nini?-alichanganya mbegu yake. Aliichanganya na mbegu ya nyoka; na alipoichanganya, alileta - alileta nini? Alileta mtoto wa kifo-mtoto ambaye-Hawa alipotosha kila mtoto baada ya huyo. Na wakati kanisa la Yesu Kristo lilipopotoshwa katika wakati wa Rumi, baada ya kuzaliwa na bikira na likatolewa kwa Kristo kwenye Pentekoste, kanisa-lilifanya nini? Lilijichanganya na fundisho la Kirumi. Na kanisa la Kiprotestanti limefanya jambo lile lile. Haliwezi kusubiri.

208 Mwanamke Fulani aliyechumbiwa na mwanaume mzuri, mdogo, msafi, na kabla hawajaoana, yule mwanamke alikuwa amefanya nini? Anakutwa akiwa na mimba ya mtu mwingine. Basi mbegu yake mwenyewe iliyokuwa imeposwa, mwili wake mwenyewe ambao ulikuwa umeposwa na mvulana rafiki yake, mchumba aliye mume wake kwa makubaliano, unakutwa umejaa mbegu ya mwanaume mwingine. Ni jambo la kuchukiza jinsi gani! Hilo ndilo hasa alilolikuta Adamu.

Hilo ndilo Kristo alilolikuta. Hakuweza kusubiri. Hilo ndilo tatizo la watu leo hii. Hawawezi kumsubiri Roho Mtakatifu halisi kuchukua nafasi ya Kanisa. Inawapasa kuunda kitu fulani, wafanye kitu fulani - ushahidi wa kwanza, kunena kwa lugha-kupata washirika wengi katika kanisa, namna hizi za miozo kabisa badala ya kumngojea Bwana kwa ajili ya udhihirisho halisi wa ufufuo wa Kristo akijitambulisha Mwenyewe miongoni mwa watu. Kanisa haliwezi kusubiri.

209 Kanisa lilifanya nini? Lilikwenda na likapata mimba ya udhehebu. La kwanza lilikuwa Assemblies of God; ndipo likaja Oneness, ndipo yakaja mengine baada ya hilo. Sasa yule anayejiita bibi arusi amepata mimba kwa namna zote za miozo, aibu. Wanawake

hawawezi kuangalia kile Neno la Mungu linachosema ila kile cha ulimwengu, hata wanaume, au hata wahubiri. Ndipo umwite huyo bibi arusi!

Ni kitu gani? Kanisa limepewa mimba. Bibi arusi wa Kristo amepata mimba kwa ulimwengu - anavaa kama ulimwengu, anatenda kama ulimwengu, makanisa makubwa, mazuri … Nini … inaonyesha kile alicho. Yeye ni wa Shetani! Hicho ndicho Shetani alichokifanya kwanza, ilikuwa ni kujaribu kujenga ufalme mkubwa na mzuri mbinguni na kwa ajili ya hilo akatupwa nje- akatengwa na ushirika wa Mbinguni. Na hiyo ndiyo sababu bibi arusi wa kisasa wa Kristo ametupwa nje, kwa sababu ametengwa mbali na Mungu, kwa sababu yeye ni kahaba mkuu na sio bikira. Ni la kina, lakini naamini mnalielewa.

210 Bibi arusi wa Adamu hakuweza kusubiri, lakini alichanganya mbegu yake kinyume cha sheria, kinyume cha sheria. Tunapaswa kuliamini Neno la Mungu na Hilo pekee.

Sasa ndugu, hapa na mnaosikiliza kanda mnaona ninavyoshikilia lile Neno, neno kwa neno. Nimekwishakuwaambia na naamini hiyo ndiyo Kweli ya Mungu. Mungu ameilinda Biblia. Inampasa kuhukumu ulimwengu na kitu fulani-kupitia Yesu Kristo ambaye ni Neno, na hili Neno lilifanyika mwili kuwa Yesu Kristo … Nalifanya tu litowelee ndani. Kumbuka, lile Neno. Na sasa Yeye analikuta kanisa limechafuka lote. Unadhani Yeye angeoa kitu kama kile? Haiwezekani kamwe. Yeye ni Mtakatifu.

Kanisa lisingeweza kusubiri. Uhalifu wa sheria, hicho ndicho alichokikuta Adamu.

211 Sasa ndugu, dada, tazameni nyuma. Kama mtatazama kivuli cha kitu chochote, ni uthibitisho halisi wa sura halisi inayokuja. Kwa hiyo unamwona Adamu alikuta mke wake ana mimba. Na Hawa akasema, "Nyoka alinidanganya."

Sasa, tuna-una-nitalichukua katika njia zote kwa muda mfupi, Bwana akipenda, unaona, niwaonyeshe kuwa haiwezekani liwe kitu kingine zaidi ya kuwa hicho.

212 Sasa, bibi arusi wa Adamu hakuweza kusubiri, ila alitangulia kwanza. Hivyo ndivyo livyo leo hii, bibi arusi wa leo. Anataka kuunda kitu fulani. "Utukufu kwa Mungu."- inampasa kulifanya kwenye jukwaa. Inampasa awe na kila kitu, unaona. Anafanya nini- anaunda kitu fulani.

Tazama linakokwenda. Unaweza kuona kuwa halina kitu chochote; ni hali ya ovyo isiyotambulikana. Sawa kabisa. Kama haikuwa hivyo, ulimwengu huu ungekuwa unawaka moto kwa nguvu za Mungu; kanisa lingekuwa kwenye moto; ee, nini … wafu wangefufuliwa na namna ya mambo yote yangetukia. Lakini ni kitu gani kilichokwishapandwa katika bibi arusi kabla Kristo hajaja Kwake, kabla hajamjia ili apande mbegu Yake Mwenyewe ndani ya bibi arusi? Bibi Arusi alikuwa na nini? - mbegu ya magugu, ulimwengu, mbegu ya kidhehebu. Hiyo ndiyo sababu huyo bibi arusi anavuna mavuno yake sasa hivi. Natumaini hu- … siwaudhi, ila natumaini linazama hadi pale ambapo naamini Mungu amewapa. Unaona?

213 Sasa, bibi arusi alichangaya mbegu yake kinyume cha sheria, kwa ulimwengu kinyume cha Neno. Alikuwa anajaribu kutafuta nini? (Sasa sikiliza kwa makini.) Alikuwa anatafuta nini? - hekima! Hekima! Na hicho ndicho amekifanya leo hii. Alipeleka wahubiri wake mashuleni, "wakaatamiwa" kwenye mashine, saikolojia, namna zote za vitu ambavyo viinge- … hata haviko katika Biblia. Na "anaatamia" mayai yake. Na anapomaliza kuatamia, analeta zao la kundi la watu ambao watakuwa na suluhu na chochote na kukataa Ujumbe halisi wa Mungu, hali huyo bibi arusi asijue kile anachokifanya.

Yeye hajui chochote kuhusu hilo. Haamini-hajui kuwa anakosea. Hata Hawa hakufikiri kuwa alikosea. Hawa alidhani kuwa alikuwa sahihi. Na kama huo ulikuwa mfano, na huu ni kinyume na mfano, itapasa itende jinsi ule mfano ulivyofanya. Sasa hilo ni-kwangu mimi ni kama tu mbili mara mbili ni nne.

214 Sasa tazama, kulitokea nini kwa watoto wa Hawa? Yule wa kwanza aliyezaliwa-sasa kama Mungu alisema, "Ongezeka (kwa bibi arusi wake, kwa bibi arusi wa Adamu) na kuijaza nchi," hilo lilikuwa agizo la Mungu; na Hawa angelikuwa ameshafanya hilo, na Adamu asingelichanganya mbegu - kuzichanganya pamoja. Lakini kulitokea nini? Adamu alipokuwa tayari kumjia Hawa, Hawa tayari alikuwa mama. Unaona ninachokimaanisha?

Sasa jambo lile lile limetokea kwa kanisa la Kristo, bibi arusi wa Kristo. Sasa tunarudi nyuma zaidi kuliko hilo kwa dakika moja. Angalia, katika huyu bibi arusi,

alifanya nini basi? Mtoto wake wa kwanza anazaliwa, alikuwa mtoto mwanaharamu, na alikuwa amejaa kifo na akasababisha kifo. Na kila mmoja tangu hapo ni kifo! Sasa mnaona inapasa iwe kujamiiana. Kwa nini unakufa kama haikuwa kujamiiana? Mungu anapotoa agizo ambalo haliwezi kupotea! Neno la Mungu ni la Milele! Haliwezi kushindwa! Yeye aliposema, "Zaeni mkaijaze nchi-hilo lilikuwa kusudi la Milele la Mungu. Ukilitekeleza huwezi kufa, kwa sababu ni Neno Lake. Ingekupasa uwe hai. Na kama yule mtoto angekuwa amezaliwa kwa usahihi, kusingekuwepo kifo; lakini Hawa hakusubiri.

215 Hilo ndilo tatizo leo. Unataka huku kuiga kwa kujifanya kulia, kuruka, kunena kwa lugha, au kitu fulani, badala ya kusubiri Neno halisi la Mungu kudhihirishwa kwa Bibi Arusi. Wale wanalipokea Neno la Mungu ni Bibi Arusi wa kweli, akizaa watoto. Hawawezi kufa. Mtoto anayezaliwa na Bibi Arusi kwenye Neno hawezi kufa kwa sababu yeye ni Neno. Amina. Mlielewa hilo? Hawezi kufa kwa sababu yeye ni - yule mtoto hawezi kufa kwa sababu yeye ni mtoto aliye Neno; yeye ni mtoto aliye mbegu; yeye ni mtoto wa Milele. Haleluya!

Hicho ndicho hasa alichokuwa Yesu Kristo-Mtoto wa Milele aliyenenwa. Hangekufa, lakini Yeye alifanya hivyo ili kwamba alipe deni. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo lingelipwa. Hakuna mtu mwingine angeweza kulifanya hilo; wote walizaliwa kwa kujamiiana kufuatia ya mpango wa Shetani. Unalielewa? Unaona?

216 Lakini kila mtu, haidhuru kama yeye ni papa, padre, askofu, chochote alicho, anakufa kwa sababu yeye ni-yeye mbegu mchanganyiko. Ni hivyo hasa! Yeye alizaliwa kati ya Shetani na Hawa. Wanaweza wakaita hilo chochote wanachotaka, ilikuwa ni Shetani na Hawa. Lile Neno la asili halikuwa na uhusiano na jambo hilo. Neno la asili lilikuwa Uzima. Adamu alichanganyisha Neno na hiyo ikaleta kifo! Na wanaweza wakaita hilo chochote wanachotaka, ilikuwa ni Shetani na Hawa. Lile Neno la asili halikuwa na uhusiano na jambo hilo. Wakati kanisa leo wanaojiita Wapentekoste, wanaojiita Wabaptisti, chochote wanachotaka, wanapolichanganya hili Neno na kanuni za kanisa, linazaa mtoto aliyekufa. Na huyo bibi arusi hawezi kuwa na uzima ndani yake. Yeye amekufa na watoto wake wamekufa.

Mungu alisema, "Nitamtupa katika kitanda cha uzinzi na kuua watoto wake." Mungu alisema hivyo katika Ufunuo. Wangapi wanajua hilo ni sahihi? Atamweka katika kitanda cha uzinzi (pale ndipo alipo), na kuua watoto wake, hata kwa moto. Tunatazama pale-kunatokea nini kwa magugu yaliyoko miongoni mwa ngano?-yatateketezwa kwa moto. Ee, huwezi kulifanya Neno liseme uongo. Ni ile Kweli. Wakati mwingine mnalishuku-lakini tunaweza kulifanya lisiwe sahihi, lakini kama utaliacha liendelee moja kwa moja, litakwenda moja-mbili, moja-mbili, moja-mbili, moja-mbili, na kuendelea. Alimtupa katika kitanda cha uzinzi. Hawezi kuzaa chochote ila watoto waliokufa.

217 Ndipo kama dhehebu linaweza tu kuzaa mtoto aliyechanganywa mbegu, kwa nini unataka kuwa wa dhehebu? Sasa ndugu, hiyo ndiyo sababu niko kinyume nalo. Yeye ni kahaba mkuu kwanza. Biblia ilisema yeye alikuwa- kahaba. Hayo ni maneno ya wazi, lakini niliwaambia kuwa ningenena kwa uwazi leo. Kile yeye alicho. Anafanya uasherati wa kiroho kwa kuchukua taratibu na kanuni za imani ya kanisa badala ya Neno, akifundisha watoto wake kufanya jambo lile lile.

Sasa, watoto wake wanatoka katika tumbo la uzazi wakiwa wamekufa. Inampasa kahaba huyo afe. Hiyo ni sahihi kabisa. Hivyo hivyo tu kama kila mtu-sikiliza, kwa hakika tu kama kila mtu mwenye mwili wa kufa anayetoka katika tumbo la uzazi la mwanamke atakufa kwa sababu yeye ni mbegu iliyochanganywa, haramu na watoto wake ni haramu. Hiyo ni sahihi. Natumaini hilo haliwapiti juu ya vichwa vyenu.

218 Sasa, Yehova aliwahi kuwa na bibi arusi wakati mmoja. Adamu alikuwa na bibi arusi, Yesu alikuwa na bibi arusi. Yehova alikuwa na bibi arusi. Mnajua hilo? Ilibidi Yeye amwache. Anakuwa kahaba mkuu, kwa hiyo akamwacha. Hicho ndicho hasa Yeye alichosema. Alikuwa kahaba mkuu, malaya. Nini kilichomsababisha kutenda hilo? (Natamani tungekuwa na wakati wa kulisoma. Naweza kufikia baadhi yake baada ya muda mfupi.) Sasa hivi, ilikuwa katika wakati wa Samweli Israeli walipokuwa na mfalme, Mungu, na Israeli alikuwa bikira. Israeli alikuwa azae kitu fulani. Na kulitokea nini? Alianza kutazama huku na huko na kuona mataifa mengine yakiwa na mfalme, kwa hiyo alitaka kuwa kama hao wengine wote.

219 Ninyi Wapentekoste mliochukuliwa na mawimbi, hilo ndilo hasa mlilofanya. Wakati huyu mhubiri mzee aliyeketi hapa, karibu afikie miaka mia moja leo, wakati

Wapentekoste walipoanza kwa vishindo nyuma kule, usingeweza kusema chochote kuhusu shirika la dini. Wasingesikiliza hilo. Waliita hayo ni mambo ya shetani, na wale watu walikuwa sahihi! Lakini ulifanya nini? Ilikupasa utende kama yale makanisa mengine. Ilikupasa uunde shirika la dini. Ndipo, kama Yeye alivyosema, mliweka nyuzio kati yenu. Mlienda kwenye kufundisha, … ? … kutufundisha (utukufu kwa Mungu!) namna hii na kuruka juu na chini na kunena kwa lugha na kusema, "Mwandikishe huyu amekuwa mshirika, ameshapokea!" Hajabatizwa ilivyo sahihi-sio kwa maji wala kwa Roho. Amekosea. Matunda yake yanamthibitisha. Anayo namna ya mbegu isiyofaa kukuza. "Mungu abarikiwe, ndugu, tutaweka mikono yetu juu yako hapa na kukufanya mzee wa kanisa! Nakuambia kile u- … tutajenga hili shirika la dini hapa hadi liwe kubwa kuliko lile la Assemblies!" Hivyo ndivyo limekuwa likienda tu. Soma historia ya Pentekoste na uone ikiwa hivyo sivyo, au ya kanisa lingine lolote.

220 Wabaptisti wanataka kuwashinda Wamethodisti. Wamethodisti wanataka kuwashinda Walutheri. Walutheri wanataka kuwashinda Wakatoliki. Kila mmoja anataka kushinda-kumshinda mtu fulani. Unaona, hiyo ni … hiyo ni roho ya shirika la dini. Lakini Yesu alisema, "Lakini ni wachache watakaookolewa. Mlango ni mwembamba na njia imesonga nao ni wachache watakaoiona." Wachache tu. Ikiwa Yeye alisema wachache (hilo ni Neno la Mungu, ile mbegu), kutakuwa na wachache. Haitakuwa makumi ya mabilioni na mabilioni. Itakuwa tu wachache watakaoiona. Wale waliochaguliwa tangu asili kwa ajili ya hilo, wanalisikia. Ile mvua ya masika imekwishanyesha sasa.

221 Sasa, Yehova alikuwa na bibi arusi ambaye alimpenda, lakini akawa kahaba. Huyo bibi arusi mkuu alifanya nini?-alifuata ya nguvu nyingine za ulimwengu. Na Yeye Jehova alifanya nini kwa huyu nabii wa kiungu, mzee, aliyepakwa mafuta (ambalo Neno la Mungu huja kwa nabii)? Yeye alimchukua yule nabii mzee, Samweli, akamwendea; akasema, "Watoto, njooni karibu nami kwa muda mfupi, nataka nizungumze nanyi, ninyi nyote. Mnatakia nini mfalme? Yehova ni Mfalme wenu. Mnatakia nini ungamo la imani? Biblia ndiyo ungamo lenu la imani. Biblia ndiyo ile Kweli. Maungamo ya imani ni ya uongo. Umekufa, zilizotungwa na wanadamu." Nionyeshe Imani ya Mitume katika Biblia. Yeye aliyewahi kusikia kitu kama hiki? "Naamini katika ushirika wa watakatifu." Yeyote anayeamini katika ushirika wa watakatifu anaamini katika kuwasiliana na mizimu. Ushirika na waliokufa. Kuna Mwombezi mmoja pekee kati ya Mungu na mwanadamu naye ni Kristo, Naye hajafa, ila Yeye yu hai milele na milele, alifufuka kutoka kwa wafu. Waprotestanti humeza hilo na ukosi mweupe na sijui lingine, pamoja na katekismo zote za makanisa, wanalimeza vivyo hivyo. Wanalipenda, hakika, kama wengine ulimwenguni.

222 "Ee , unajua tuliwahi kuwa Wapentekoste. Tulisimama kwenye kona na matari mikononi mwetu na kuomba; na wanawake wakiwa wamesimama pale na nywele zao ndefu zikining'inia na wakimsifu Mungu na vitu kama hivyo." Lo, jamani, mnajua vyema kuliko kufanya hivyo. Mkristo halisi angekudharau waziwazi. Wakiwa wamesimama pale na nywele ziliokatwa namna hiyo na wamejipaka rangi kiasi cha sufuria kubwa namna hiyo na gauni linaloonekana kama nguo iliyobana mno hata ikashikamana na ngozi, na kwenda kutembea ukiwa hivyo, na huko unajiita wewe u mtakatifu wa Mungu? Unajua vyema kuliko kufanya hivyo. Hata Ulimwengu unajua vyema kuliko kufanya hivyo. Aibu kwenu. Ni heri ungekaa mbali na pembe hiyo … kama huwezi kutenda zaidi ya hilo. Sikosoi, sijarukwa na akili. Ninawaambia ile Kweli, na mtaona katika siku zijazo kuwa … Lakini ni kama ambavyo imekuwa siku zote, na siku zote litapita juu yao na ndipo hawataliona hadi liwe mbali kupita kiasi. Wamefanya hivyo kila wakati. Wamekwishalifanya na kulifanya.

223 Bibi arusi wa Yehova alitaka kwenda kufanya ukahaba pamoja na watu wengine, kama hao watu wengine. Hicho ndicho alichotaka kufanya Bibi Arusi wa Yesu Kristo. Na mzee Samweli, ambaye Neno lilikuja kwake … Neno lilikuja kwa nani?-kwa manabii. Yule nabii mzee alikwenda na kusema nini, "Sasa subirini kidogo watoto. Kwa nini mnataka kutoka nje, ili mkatafute nini?" Akasema, "Nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ila lile lililotukia?" Mnakumbuka hilo? Wangapi mmewahi kusoma hilo? Hakika mmesoma. "Nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ila lile lililotukia?" Na jambo lingine, nilikwenda na kuwa na mikutano mikubwa, au na kadhalika, na kuchukua fedha zenu zote? Je, niliwahi," akasema, "Niliwahi kumuomba yeyote-" Nazungumza kuhusu Samweli sasa. Neno la Bwana lilikuja kwa mtu fulani. Akasema, "Je, niliwahi kuwaomba kuchukua-kuweka kiasi fulani na kufanya hivi na hivi?"

Wakasema, "hapana," "hapana, hukuwahi kufanya hilo. Hukuwahi kutuambia lolote ila lile lililokuwa sahihi."

Akasema, "Basi kwa nini mnataka kuliendea hilo?"

Wakasema, "Samweli, uko sahihi sana, lakini tunalitaka hata hivyo."

224 Hilo ndilo hasa ambalo Kanisa la Pentekoste lilifanya. Hiyo ndiyo sababu sijiungi nao. Hakika, nataka nibakie mwanamwali mbele za Mungu pamoja na Neno Lake. Iwapo wao-hainipasi kuwa na maonyesho makubwa na vitu kama hivyo. Nimevikataa. Sikutaka kujifunga mwenyewe. Hiyo haikuwa hekima yangu; hiyo ilikuwa hekima ya Mungu. Kama ingenipasa kwenda nje basi ningeweza-ningekuwa najipendekeza hapa na pale kwa watu na kwa Shetani na kuwaambia,, "Ndiyo, ilinipasa kuwa na kiasi hiki kwa ajili ya matangazo ya televisheni, na kuwa na kiasi fulani cha hiki; inawapasa mnilipie," Ilinipasa niweze kudhibiti vitendo vya watu wengine vilipogusana na huduma yangu namna hiyo pia. Lakini sikuwahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ila lile lililotukia. Sikuwahi kuwaambia lolote isipokuwa Neno. Hukumuni wenyewe. Je, nimewahi kuwaomba mnipe chochote? Hapana, bwana. Hapana, Mungu amekuwa msaada wangu katika hilo. Sina mipango mikubwa ya shughuli zitakazohitaji misaada ya watu. Sina hata mmoja. Kila mmoja aliye wa Mungu atamsikia Mungu! Atajisikia tu kuongozwa na Roho pa kwenda na lipi la kufanya na alifanye hilo. Hayo ndiyo tu yaliyo ya lazima. Lishike hilo, sio mipango mikubwa ya kiuchumi yenye kuzalisha mamilioni ya dola za Kimarekani, mamilioni na mamilioni na mamilioni, na baadhi yao sasa wakijenga mamilioni na mabilioni ya dola ndani yake.

225 Sijisikii vibaya kuhusu kukosoa. Ni ukosoaji halali. Sitaki kumtia mtu yeyote uchungu, ila ni heri kumtia mtu fulani uchungu kuliko kumtia Mungu uchungu. Kama Mungu alikuagiza na kukutuma hapa kufanya haya mambo na kuyathibitisha miongoni mwa watu, basi unapaswa kulisikia. Ninawaambia ile Kweli. Mungu anathibitisha kuwa ni ile Kweli. Kwa-sio ishara pekee, ila Yeye analithibitisha kwa Neno Lake kuwa ni ile Kweli. Hiyo ni sahihi kabisa.

226 Kwa hiyo bibi arusi wa Yehova alitoka kwenda kufanya ukahaba, na huyo bibi arusi alifanya nini? - alizaa kundi la watoto wa haramu tena. Je, hiyo ni sahihi? Tunajua ni ile Kweli. Hata wachukuliwa mateka na Mfalme Nebukadneza na kadhalika. Biibi Arusi wa Kristo amefanya jambo lile lile. Shida ni nini?-hawezi kusubiri. Ee, hapana. Uh uh-hawezi tu kusubiri.

Inawapasa watengeneze kitu fulani. Hawawezi kumngoja Roho Mtakatifu aje na aingie katika Kanisa. Unaona, Iinabidi wapate watu wengi zaidi katika dhehebu lao. Kama ingekaa kama ilivyokuwa nyuma kule miaka mia moja iliyopita, au miaka hamsini iliyopita, wakati Pentekoste ilipoanza kwanza katika hii siku karibuni, Neno liliopoanza kuhubiriwa, kama ingekaa hivyo, labda haingekuwa na washiriki hamsini leo. Hiyo ni sahihi. Lakini wangekuwa wameoshwa kwa damu. Wangalikuwa na nguvu za Mungu ndani yao! Ulimwengu ungetikiswa kwa kishindo kikubwa mno cha Neno lililofanyika mwili likinenwa neno kwa neno. Lakini leo, mbona, ni shaba iliayo na upatu uvumao. Hiyo ni sahihi. Imekuwa upuzi, kitu cha kudhihakiwa, aibu kwa ulimwengu, aibu kwa Mungu.

227 Niliingia mahali, ndugu watatu-ndugu wawili na mimi tuliingia mahali fulani ng'ambo ya Springfield, Missouri asubuhi ile nyingine kwa ajili ya kifungua kinywa tukitokea Arizona, na bibi mdogo pale ambaye Ndugu Wood alinionyesha alifanana na dada yetu Collins-mwenye nywele rangi ya shaba, akiwa na fundo kubwa la nywele kwa nyuma-na Ndugu Wood akasema, "Je, yule si anafanana na mke wa Ndugu Willard Collins?"

Nikasema, "Ni hivyo." Hapa akatoka bibi mzee, na nikasema, "Nafikiri yule ni mama yake. Tazama lile fundo kubwa la nywele." Nikasema, "Hilo ni hapa hapa karibu na Kanisa la Assemblies of God, makao makuu ya Assemblies of God; pale ndipo-ndiyo sababu wako hivyo." Na kundi la akina dada wadogo wakiwa wameketi pale na nywele zilizolazwa namna hii; hao walikuwa wanafunzi. "Vijana wadogo wasiojijali, na wote pale, unajua, wakipiga makelele, wakibeba-Biblia zao chini ya kwapa zao.

228 Kwa hiyo tuliwatazama hadi wote wakatoka nje-wakibeza, wakicheka, wakipiga makelele tu kama wale wa kisasa-hilo ni zao la Pentekoste likija kwa ajili ya kesho-kama kuna kesho. Kwa nini! Kwa nini! Kwa nini!-kwa sababu hiyo ndiyo mbegu iliyopandwa.

Hiyo ni sahihi kabisa.

Wakati alipotoka nje, wote walitoka nje, huyu dada mdogo akarudi na kusema, "Je, ningeweza kufanya lolote kwa ajili yenu wote?"

Nikasema, "Ningependa kukuuliza swali."

"Naam, bwana."

Nikasema, (kama, kama mgeni, nilifikiri angeweza kutufahamu)-na

nikasema, "Je, ile pale sio shule ya Biblia?"

Akasema, "Ndiyo, bwana, ni shule ya Biblia."

Nikasema, "Nadhani mnapata biashara yote tokea pale." (Sasa, huyo alikuwa Ndugu Fred Sothman akiwa ameketi pale na Ndugu Banks Wood, wadhamini wawili wa kanisa.) Nami nikasema uh … Yule bibi mdogo akasema, "Naam, ni hivyo."

Nikasema, "Nadhani wewe ni wa humo?"

Akasema, "Hapana, samahani, mimi sio wa humo."

Nami nikasema, :Sababu nikawaza hivyo ni kwa sababu ya hizo nywele ndefu nzuri ulizo nazo. Na nafikiri yule ni mama yako?"

Akasema, "Hapana, bwana": akasema, "yule anafanya tu kazi hapa." Akasema, "Hapana, mimi si- ." akasema, "Napenda nywele ndefu. Ninaye binti mdogo, na namvalisha tu nywele ndefu pia." Na akasema, "mume wangu anapenda nywele ndefu."

Nikasema, "Mungu ambariki."

229 Na hivyo akasema, "Vema-" Akasema- Nikasema, "Mbona ni ajabu. Je, wale ni wanafunzi wa hapa, wale wasichana waliokata nywele namna hiyo, kama yule bibi wa kwanza?"

"Ndiyo."

Tulipotoka-nikasema, "Asante"; tukatoka nje. Nikasema, "Mungu aliweka yule mwanamke pale kwa ajili ya kukemea lile kundi la watoto haramu upande wa pili wa ule mtaa!"

Hiyo ni sahihi, haramu, kutafuta mambo ya ulimwengu. Wanawake wangapi waliomfuata Yezebeli, mke wa mkuu wa nchi, wangapi kati yao mnadhani wako Mbinguni usiku huu, leo? Unaona? Mambo ya ulimwengu-Kama unaupenda ulimwengu au mambo ya ulimwengu, upendo wa Mungu hata hauko ndani yako. Pale una-Ni nini hicho?-mazao yaliyo bora ya kesho katika Pentekoste-muondoko wa kidini ulio mkubwa kupita yote katika taifa hili. Ndivyo ilivyo. Huyo ndiye Bibi Arusi. Silipati hilo.

230 Vema, Upentekoste unajaribu kufanya nini? Ee, anatengeneza mruko kidogo kwenye jukwaa - sio kulikebehi; ni jema. Wanatengeneza jambo lingine. Kwa nini?-wapate washirika katika kanisa. Tatizo ni nini? Hawezi tu kusubiri. Unaona? Hawezi kungoja Mungu afanye hilo. Yawapasa wapate washirika mahali fulani. Kwa hiyo wanawaambia, "Inawapasa mfanye hilo," nao wanaondoka. Unaona, hiyo ndiyo mbegu ikiota. Inakupasa ufanye hilo.

231 Nime-Mimi ni mmisionari. Nimewaona Waafrika wakichukua damu ya mnyama na kujimwagia namna hii (uchi kabisa, wanaume na wanawake), wanajichora nyuso zao kwa rangi-hapo ndiko linakotoka; kupaka rangi hutoka kwenye tabia ya kipagani, sio kwa ajili yetu wanadamu, Wakristo, waamini; haikuwahi kuwa hivyo. Je, haikuwa mwanamke mmoja tu katika Biblia yote aliyewahi kujipaka rangi, huyo alikuwa Yezebeli, shetani.

Kwa hiyo basi yeye-wanapaka nyuso zao rangi, vitu virefu na vikubwa katika masikio yao kama matofali ya mbao (Wazulu) ni vipande vya mbao, hufanya nyama ya sikio kuning'inia pale - wakati mwingine hugawa midomo yao na kuitoa nje (wakidhani linaonekana zuri), wanapaka damu kwenye matiti yao na, na ndipo kwenye miguu yao na mambo, na ndipo huchukua na kufanya milia kama pundamilia, na kupiga kelele, wanacheza katika roho na kunena kwa lugha, na kuabudu mashetani: ushahidi wa Roho Mtakatifu!

232 Sasa nimekuwa kule India walipokuwa na wale watembeao juu ya moto na kila kitu kingine na kudhani ni kweli. Sanamu kubwa pale na vito vya thamani katika masikio

mahali pa hereni na vitu kama hivyo, na wanaitesa miili yao na kuichoma na vitu vikali, na kujipiga na kushona midomo yao kama walikuwa wamesema uongo, na kutubu kwa kujitesa na kuweka upanga mwembamba katika midomo yao hapa au kwenye videvu vyao kupitia puani na kuitoa nje namna hiyo; wanachukua ndoana za samaki kubwa, kama mipira ya mti wa Krismasi, wanakwenda na kuijaza maji na kuishikiza kwa ndoana maelfu juu ya miili yao, moja kwa moja ikipenya katika miili yao, na kwenda pale na kucheza dansi kuzunguka hii sanamu namna ile , na kumwua mbuzi na kuabudu namna hii, na kutembea moja kwa moja kwenye moto mkali bila jeraha. Baadhi yenu Wapentekoste mnajaribu hilo!

233 Lakini lilifanyika-watoto wa Kiebrania. Lakini hawakuwahi kumjaribu Bwana Mungu wako; walitupwa tu ndani yake. Hawakujaribu kutengeneza kitu fulani. Hilo ndilo tatizo la Wapentekoste leo. Wanatengeneza jambo fulani! Hawawezi kusubiri! Ee Mungu, hawawezi tu kusubiri, kwa hiyo wanafanya uzinzi. Amina. Magugu ya kutengeneza kitu fulani, na linaleta nini?-kama lilivyofanya mara ya kwanza, bibi arusi wa kwanza. Hawakuweza kusubiri.

Yule bibi arusi alileta kifo kupitia mtoto haramu ambapo sisi sote ni watoto wake. Mungu alikuja katika mwili ili atupe kuzaliwa tena kunakoturudisha kuwa wana na binti za Mungu wa asili. Unaona? Ndiyo hivyo. Mbegu sahihi ya Hawa haikutokea. Haikuwahi kutokea. Kwa nini? Aliichanganya, akaiweka mbali na yeye. Badala ya Adamu kuja kwake akiwa bibi arusi kwa wakati uliokubalika-kama tu Kristo ambavyo angekuja kwa lile kundi, Kristo angelipaswa kulijia kwa Kanisa Lake; Yeye aliahidi kufanya hilo. Mungu aliahidi wao kuongezeka, lakini ingewapasa kungoja hadi wakati wa Mungu.

234 Hilo ndilo tatizo leo. Hawataki kungoja wakati wa Mungu. Wanataka kupata kitu kingine, na kwa hiyo Shetani anakuwa na werevu pale pale ili awape huo. Waunde shirika la dini; liwe kubwa kuliko mengine.

Sasa mnaona ni kwa nini niko kinyume nalo? Hakika niko kinyume nalo pamoja na yote yaliyoko ndani yangu. Ili mradi Neno liko ndani pale, siku zote litakuwa kinyume na shirika la dini. Mungu yuko kinyume nalo. Mungu alisema kuwa Yeye alikuwa kinyume nalo. Hiyo ni sahihi. Huyo bibi arusi hakuweza kusubiri.

235 Kwa hiyo mbegu ya Hawa haikuwahi kutokea. Akiwa amechanganishwa mbegu na uongo wa Shetani, bibi arusi mpenzi wa Adamu alinajisika. Vivyo hivyo na Bibi Arusi wa Kristo. Yule bibi arusi - nini kilichomfanya anajisike? (Bibi arusi wa Adamu sasa)-kwa sababu hakuwahi kudumu na Neno la Mungu. Hiyo ni sawa? Nauliza-sasa-ikiwa siyo hivyo, usiliseme; lakini kama ni hivyo, liseme. Sababu Mungu - Sababu ya bibi arusi wa Adamu-hapo kuna watatu: Adamu, Kristo, Mungu. Sababu bibi arusi wa Adamu hakuzaa ilivyo sahihi yule mtoto wa uzima ni kwa sababu hakuliamini Neno la Mungu. Kama hiyo ni sahihi, sema, "Amina." [Kusanyiko linajibu, "Amina."-Mh.] Sababu yule mke wa Yehova akafukuzwa, au bibi arusi wake, ilikuwa kwa sababu yeye alilikataa Neno la Mungu, Nabii. Hiyo ni sawa? Sababu yule bibi arusi wa Kristo akafukuzwa kwa talaka ni kwa sababu yeye amelikataa Neno la Mungu, kama alivyofanya Hawa, kama wale wengine; kabisa, wote ni makahaba, wote wamenajisika. Mume wao hajawajua. Walikuwa tayari wamepata mimba kabla ya mume wao hakuwajua.

Loo, Mungu , kama hilo sio la kuonekana lenye kuhuzunisha! Wazia kijana akimjia mwanamke na kumkuta akiwa na mbegu ya mwanaume mwingine ndani mwake. Ni jambo la jinsi gani! Hilo ndilo Mungu amelifanya. Hilo ndilo Adamu amelifanya. Hilo ndilo Kristo amelifanya. Loo!

236 Ndiyo, hakuwahi kukaa na Neno na akasababisha hali ya kuchanganya mbegu. Hicho ndicho Israeli alichofanya. Unaona pale aliko sasa? Hicho ndicho Bibi Arusi wa Kristo alichofanya. Unamwona pale aliko?-amerudi kule kule kwa wengine. Bibi Arusi wa Kristo wa Kipentekoste alifanya jambo lile lile.

Huyo bibi arusi hawezi kuzaa watoto wa kiroho wa Neno, kwani yeye mwenyewe ni mbegu mchanganyiko. Atawezaje kulifanya hilo wakati yeye mwenyewe ni mbegu mchanganyiko na madhehebu? Alijiunga nao na kila kitu kama vile tu wale walivyo. Yumo katika baraza la makanisa na kila kitu kingine, amechanganya tu mbegu mchanganyiko kama wale wengine walivyo. Anawezaje kulifanya hilo? Hawezi kulifanya.

237 Sasa, ninayo tu mengi ya kusema, na yanipasa tu kuyaharakisha haya. Mimi - kila moja ya haya ninayotaka kuhubiri juu yake, unaona.

238 Sasa tazama, yule Bibi Arusi wa kweli-Haleluya, huyo atakuweko! Kwa nini? Yeye alichaguliwa tangu asili. Yeye hatafanyika dhehebu, kwa sababu Yeye alichaguliwa tangu asili. Yeye hatafadhaishwa kuhusu dhehebu fulani, Yeye tayari amechaguliwa tangu asili, akae katika nafasi hiyo.

Tazama, kama Mariamu-nataka mlipate hili sasa na msilikose. Mko tayari? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linajibu, "Amina."-Mh.] Kristo atakapokuja kwa Bibi Arusi Wake, Bibi Arusi atakuwa bikira kama Mariamu alivyokuwa kwani Mungu hatamleta Kristo kupitia tumbo la uzazi la kahaba, wala hatamleta Bibi Arusi kwa njia hiyo. Hawezi kuleta Neno Lake kupitia kahaba wa Neno Lake. Hayo ni maneno ya kutisha, lakini hicho ndicho Biblia ilichosema. Nasema kile ilichosema kwa sababu hili lapasa lieleweke.

239 Yule Bibi Arusi wa kweli , kama Mariamu, atakuwa na tumbo la uzazi bikira kwa ajili ya Bibi Arusi wa Neno, ambaye ni Kristo. Wakati Kristo, alye Neno, ajapo kwa Bibi Arusi, Bibi Arusi atakuwa kama Kristo alivyo-bikira kwa lile Neno. Natumaini-natumaini linapita juu, Ndugu Neville. Na- Unaona? Natumaini mnaelewa. Kristo alikuwa nini?-Neno!-Neno la Mungu. Juu ya paja Lake alikuwa na Jina limeandikwa, "Neno la Mungu." "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno … akafanyika mwili, akakaa kwetu." Yeye ni Mungu, na Mungu ni Neno. Na Bibi Arusi Wake atakapokuja, huyo Bibi Arusi atakuwa tunda lile lile alilo Kristo-alivyo bikira!

240 Je, Kristo alikuwa wa dhehebu? Yehova alikuwa wa dhehebu? Wala Bibi Arusi Wake hawi wa dhehebu! Yeye ni sehemu ya Kristo. Yeye haitaji fundisho la kanuni; hawezi kuwa na lolote. Yeye atakuwa bikira halisi. Jinsi gani?-kwa matendo. Amina. Ataitikia kila Neno analolisema Mungu kwa "Amina. Amina. Ee, 'na iwe kwangu kufuatana na neno lako.' Amina." Loo, jamani! Hilo ndilo lenyewe. Itikia Neno la Mungu.

Uwe na tumbo la uzazi lililo bikira. Bibi Arusi atatokea wapi?-kwenye tumbo la uzazi lililo bikira, Neno. Yesu alitokea wapi?-kwenye tumbo la uzazi lililo bikira. Unaona?

241 Adamu alipomjia mke wake alimkuta ana mimba. Mke wake alikuwa amefanya jambo fulani. Alikuwa amejichanganya. Alikuwa-amechanganya mbegu ya mtoto, na mtoto akafa. Lakini Yusufu alipokuja kwa bibi arusi wake alikuwa amepata mimba, lakini ya Uzima. Mke wa Adamu, au bibi arusi wa Adamu, wakati Adamu-kabla hawajakaribiana-kama tu Yusufu na Mariamu, kama tu Kristo na kanisa sasa (hamlioni? Unaona)-na kabla hawajakaribiana (Adamu na Hawa), Hawa alikuwa amepata mimba kwa mbegu ya uharibifu toka kwa nyoka; na Adamu alipomjia mke wake alimkuta amepewa mimba ya kifo. Unaona? Kifo! Kwa vipi?-kiroho, akafa kimwili; lakini Yusufu, mwanadamu, alipomjia mke wake (utukufu! Ilikuwa vigumu kumshika!), alikuwa amepata mimba kwa Uzima, Neno la Mungu ni mwili miongoni mwenu.

242 Kurejesha lile Neno lililonenwa! Kurejesha lile Neno la Mungu lililokuwa Neno hapa - lililokuja kupitia tumbo la uzazi la mwanadamu. Amina! Mungu atalifanya vyovyote vile. Yeye alilinena, na inapasa iwe hivyo. Ee, utukufu!

Amina! Huyo ndiye Mungu wetu. Ee, hilo ni jambo la kina, ndugu, ikiwa ninaweza kuliyeyusha-mnaweza kuligonga. Pale ndipo Yeye alipowakuta.

243 Adamu alipomjia mke wake, alikuwa amepata mimba kwa mbegu isiyo halali. Wakati Yu - Ile mbegu ikafa! Yusufu alipokuja kwa mke wake, alikuwa amepata mimba. Sasa nini kilisababisha utofauti katika utiwaji wa hizo mimba? Kwa sababu yule mke wa Adamu alishuku Neno. Hiyo ni sawa? Bibi arusi wa Yusufu aliliamini Neno. Hiyo ndiyo tofauti. Kwa hiyo hicho ni nini basi? Ni Neno! Loo, lile Neno la thamani! Lilikuwa- Ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu! Haleluya! Pale pale ndipo makao yangu. Yaache madhehebu yote na kila kitu kingine kianguke na kufanya kile watakachokifanya. Nasimama juu ya lile Neno.

Hiyo ndiyo sababu nimefanya kile nilichofanya. Hiyo ndiyo sababu nimeyatupa chini madhehebu. Unasema, "Mbona yeye tu ni-Huvunja makanisa." Walisema hilo hilo kuhusu Bwana wetu. Wanalisema tu kila wakati, unaona.

244 Sasa, Adamu alimpata Hawa. Kristo anakuja kwa Bibi Arusi Wake. Anamkuta wapi? - jambo lile lile. Kwa nini? Bibi Arusi alipoanza pale mwanzo-(Sasa sikiliza, sitaki mlikose hili.) Alipoanza pale mwanzo alikuwa bikira. Alikuwa anaendelea vyema. Aliendelea vizuri katika kanisa la kwanza. Lilikuwa zuri mno. Mungu alimpa Bibi Arusi, na huyo bibi arusi alifanya nini? Kama unajua historia, katika mwaka wa 606 alikwenda moja kwa

moja kule na kujipa mimba kwa fundisho la Kirumi, au shirika la dini. Na kuanzia hapo na kuendelea, yule mama kahaba wa zamani katika Biblia akazaa makanisa, nayo yalikuwa makahaba, huyo ni kahaba mkuu-hao ni Waprotestanti-kwa sababu walikuwa, kila mmoja alikuwa amezaliwa kutoka kwake na kila mmoja akachukua mkondo wake mwenyewe-shirika la dini. Sasa mnaona ni kwa nini niko kinyume nalo? Vema.

245 Sasa, kuzaliwa kwa Neno ni Kristo. Sio lililonajisiwa … pamoja na madhehebu. Kanisa la kwanza - hakukuwa na madhehebu, ni Neno tu na kumiminwa kwa Roho. Ndugu, lile-Mungu alilitandaza Neno chini namna hiyo na Roho Mtakatifu akalinyeshea, na bibi arusi akawa katika mwendo wake. Yule Bibi Arusi akazaa watoto, hakika, lakini hili kanisa haliwezi kufanya hilo. Limegawanyika kimadhehebu kupita kiasi, unaona, haliwezi kufanya hilo. Limechanganyika na ulimwengu. Tazama kile walichofanya.

246 Sasa, sasa tazama, Mungu alithibitisha Neno Lake kupitia mwili Wake. Hiyo ni sawa? Ndipo bibi arusi akaenda akifanya ukahaba kama mke wa Adamu alivyofanya katika Edeni na mke wa Yehova alivyofanya katika siku za Samweli, alipomchagua mfalme, akampa Mungu talaka (mume aliyemchumbia) na Neno Lake na nabii Wake (njia ya kutokea Neno Lake), na kwenda akifanya ukahaba kama yale mataifa mengine; na Mungu akampa talaka! Jambo lile lile kama Yeye alivyokwishafanya leo. Tendo lile lile.

247 Wana wa bibi arusi, walifanya uzinzi (unaona) pamoja na bibi arusi, Mwana wa Mungu - Bibi Arusi Wake kutoka Pentekoste, akiwa bikira na Neno, alifanya ukahaba na kuzini kama tu alivyofanya mke wa Adamu, kama tu alivyofanya mke wa Yehova; na hapa yuko mke wa Mwana-anafanya ukahaba, akizini na miungu wa Kirumi (wingi), miungu, na kwa ajili ya mpenzi wake, wale miungu wa Kirumi, alijaribu kumchukua mume wake mwenyewe na kumgawa katika sehemu tatu-ili awapendeze wapenzi wake! Mungu uwarehemu! Hakika, wanao mamia ya miungu, ee hakika-Astate, mungu jua, na Balaamu, mungu jua, na malkia wa mbinguni na huo upuzi kule. Kwa hiyo bibi arusi, ili awapendeze wapenzi wake waovu. Mungu hakunena kule kwenye Wimbo Ulio Bora na kusema juu ya mke wake ambaye hakuwa lolote ila kahaba na akiwa amekaa tayari kila wakati na kuchukua kila mpenzi aliyekuja. Nanena wazi, lakini hicho ndicho Biblia ilichosema. Kila mwanaume aliyetaka kutembea naye aliweza kutembea naye. Hilo ndilo jambo lile lile ambalo bibi arusi wa Kristo amelifanya-alijiweka wazi kwa kila uchafu wa kizamani, tabia mbaya ya kila shirika la dini waliyokuwa nayo. Anafanya jambo lile lile.

248 Ninakwenda kukosolewa kwa ajili ya hili. Hiyo ni sawa, ninakwenda kubarikiwa kwa ajili ya hilo vile vile. Lakini hilo linakwenda kuwa ile Kweli, Kweli ya Mungu, kwa sababu Yeye anataka isemwe, na hapa-najaribu kadiri niwezavyo kuisema Hiyo. Unaona?

249 Bibi arusi alijaribu kuwapendezesha wapenzi wake wengi. Kwa kufanya hivyo akachanganya mbegu, alijaribu kuchanganyisha mbegu ya wapenzi wake na Neno la Mungu; hivyo lisingefanya kazi; kwa hiyo bibi arusi akasema, "Nalikana hilo hadharani" na kufanya Neno lake mwenyewe. Sasa anadai kuwa yeye mwenyewe ni Neno. Lakini usiwaruhusu Wakatoliki-au waprotestanti waitwe Wakatoliki kwa sababu wanafanya jambo lile lile katika baraza la makanisa yao-wakifanya ukahaba. Si ajabu wanaitwa makahaba! Hilo ni chungu, sivyo? Hilo linashtua ngozi yako ya mgongoni, lakini hivyo ndivyo ilivyo ili kuwaamsha wakati mwingine.

250 Hicho ndicho hasa bibi arusi alichofanya. Alimwacha Yesu, Mume Neno, na kama Samweli - walimwacha Samweli na kumchukua Sauli, wakamwacha nabii aliyepakwa mafuta kwa Neno na kumchukua mfalme mwenye fimbo ya kifalme; wakati ambapo hatimaye angalikuja kwa Mfalme, mwenye fimbo ya Mfalme, katika Utawala wa Miaka Elfu, lakini sasa amekataliwa. Bwana alikwenda kwa Mataifa kwa ajili ya kupata Bibi Arusi. Hiyo ni sawa? Hilo ni Neno.

Sasa, bibi arusi alimwacha Yesu, aliye Neno - Yesu, aliye Neno, na kuolewa na mwanaume mwingine aitwaye papa akiwa na kanuni za imani. Sasa hajampata Yesu; anaye papa. Sasa hatujawa na - Protestanti haina Yesu; ina dhehebu, jambo lile lile - alama ya mnyama.

251 Kwa hiyo bibi arusi huyo hawezi kuzaa watoto wa Neno, hata mmoja. Yeye mwenyewe ni kahaba. Biblia ilisema yeye alikuwa hivyo. Alikuwa na kikombe mkononi mwake na alikuwa anatoa fundisho lake kwa watu ambalo lilikuwa chukizo, uchafu wa uasherati wake. Uasherati ni nini? - ni kuishi katika uchafu. Na kwa fundisho lake analowapa watu, ni uchafu wa uasherati wake Na wafalme wa dunia na wote

walileweshwa kwa mvinyo ya uasherati wake. Sahihi kabisa, watazame. Kijana, watakuchinja koo lako kwa dakika moja kwa ajili ya hilo. Sio Wakatoliki tu, hata Waprotestanti.

252 Sikilizeni, enyi Wamethodisti. Ninyi mliomuua John Smith? Sasa shangilieni. Ingawa siamini katika fundisho lake, wala siamini katika fundisho lenu. Hilo silo, hilo ni ninyi. Hiyo ndiyo sababu John Smith alikuwa tu na haki ya kutosha kuhubiri dini yake hapa katika hili taifa kama mnavyofanya, lakini mlimuua hapa Illinois; mlimpiga risasi bila sababu, kwa sababu alikuwa na kitu kidogo tofauti. Ndipo mnapiga kelele kuhusu Kanisa Katoliki. Tokeni kwenye lile kundi la kipuzi ninyi Wamethodisti mliowekewa Uzima wa Milele. John Wesley angeamka katika kaburi lake, akitenda hivyo. Hakika angefanya hivyo. John Wesley hakuwahi kuanzisha kanisa kama hilo. Kundi la akina "vijana wenye utovu wa nidhamu" na akina "Elvis" lilifanya hilo baada ya kifo cha John. Hiyo ni sahihi. Siyo John Wesley. Siyo wale wapentekoste wa zamani waliofanya matokeo kama haya. Ni kundi lile lile baada ya hiki kifo. Hiyo ni sahihi. Yesu Kristo hangeanzisha kitu kama tulicho nacho sasa kinachoitwa Pentekoste; wala Roho Mtakatifu hangeanzisha, lakini ni kitu fulani mlicho nacho hapa Yake; lakini Roho Mtakatifu ni kitu ambacho hawawezi kukiua sasa. Atamchukua Bibi Arusi vyovyote vile. Atamchukua mmoja vyovyote vile. Mungu alisema angelichagua kimbele.

253 Bibi arusi alimwacha Yesu, Mume wake aliye Neno, aolewe na papa, kwa hiyo hawezi kuzaa, kuzaa kiroho - anaweza kuzaa kidhehebu sasa; anazo mbegu nyingi za hilo - hawezi kuzaa kiroho, yeye - kwa sababu alikuwa kahaba. Kitu pekee anachoweza kutoa ni uzima wa kidhehebu na kujitangaza kwingi kwa fujo na makelele. Kanisa Katoliki lenyewe limeundwa kutokana na mambo kadha ya ushirikina wa Kikristo pamoja na rundo la utamaduni wa Kirumi, kanisa la Pentekoste ni baya tu kiasi hicho hicho - kundi la wanaorukaruka na kupiga kelele na kunena kwa lugha na vitu kama hivyo. Wakati hali hiyo inapopoa - hasira za kutosha kupiga makonde na kukutoa nje ya kusanyiko lao. Kama Mungu alikuja ndani kule na kufufua wafu, kama hukubaliani nao, wangekutoa nje, kama wewe sio wa shirika lao la dini.

254 Sasa, huyu mama kahaba wa zamani (Narudi kwake kwa muda mfupi), anadai kuwa na uwezo wa kusamehe dhambi, lakini huukumiwi kufuatana na madai yako; hujulikani kufuatana na madai yako. Unajulikana kufuatana na matendo yako. Angewezaje kusamehe dhambi? Mtazame. Yesu alipofanya jambo lile lile, wao … Alisema, "Nihukumuni; nionyesheni pale nisikoliamini Neno." Huyu kahaba anadai kuwa na uwezo wa kusamehe dhambi, lakini hilo linakuja tu kwa njia ya Neno. Hiyo ni sahihi. Mungu ndiye pekee anayeweza kusamehe dhambi. Hiyo ni sawa? Je, wale Mafarisayo hawakusema hilo? Nia ilikuwa nini - tatizo la lile kundi la wanafiki. Kwa nini? - kwa sababu hawakuona kuwa lile lilikuwa Neno likiwa limesimama nao! Yeye ni Neno! Utukufu kwa Mungu! Hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kusamehe dhambi. Yeye alikuwa Mungu! Yeye alikuwa Neno lililodhihirishwa.

255 Sasa kanisa Katoliki husema Yesu aliwapa uwezo. Yeye alifanya hivyo. Yeye alilipa kanisa uwezo. Hiyo ni sahihi. Tunaamini hilo. Mabinti zake wote, mabinti zake wa kidhehebu, ni makahaba, "Ndugu Branham, hilo ni neno kubwa." Hilo sio neno langu; hilo ni Neno Lake Bwana. Hilo ndilo hasa. Sio langu, ni Lake.

Vema, vipi? Unasema, "Wanakuwaje?" "Wanakuwaje makahaba? Mbona, ni watu wazuri. Hata …" Sisemi lolote kuhusu hilo. Sisemi kile walicho. Sisemi Wakatoliki kuwa sio watu wazuri. Ni wazuri kama watu wengine walivyo. Ni wanadamu kama tulivyo. Lakini tunapolilinganisha na lile la zamani, kanisa Katoliki liko makosani. Waprotestanti ni wazuri vile vile kama wao - Wamethodisti ni wazuri vile vile kama Wabaptisti au Wapentekoste, au mtu mwingine yeyote. Wao ni sawa.

256 Lakini jambo lenyewe ni kwamba, yeye anawezaje kuwa kahaba? Kwa nini? Mpe jaribio la Neno. Hivyo ndivyo utakavyolijua. Mjaribu kwenye Neno mara moja na uone kile anachosema. "Ee, bila shaka tunafundishwa katika seminari kuwa siku zile - ni - ilikuwa namna ile, lakini (ha - ha) hiyo ilikuwa nyuma kule katika siku za mitume. Hiyo ilikuwa kwa ajili ya mitume pekee." Ninyi mnaoitwa Kanisa la Kristo - "semeni pale Biblia inaponena na kunyamaza …" Vema, ningependa kusikia mkinena sasa. Hapana, mnyamaze. Neno la Mungu hunyamazisha kila kitu, Ndugu. Hakuna mtu anayeweza kujivuna. Hiyo ni sahihi.

257 Mabinti zake wote ni makahaba. Kwa vipi? - kwa lile lile kama mama yao - kufanya

tu uasherati wa kiroho dhidi ya Neno. Hivyo ndivyo Kanisa Katoliki linavyokuwa kahaba mkuu. Hivyo ndivyo mabinti zake wanavyokuwa makahaba. Jambo lile lile, uasherati wa kiroho dhidi ya Neno. Yeye na binti zake wana tumbo la uzazi la ukahaba. Kifo pekee ndicho kinachotokea kwao. Mungu hawezi kuleta uzima kupitia kifo, na chochote kinachozaliwa kikiwa kimekufa hakiko hai. Na kama Ayubu alivyosema, "Unaweza kutoa kitu kisafi kutoka kilicho kichafu - hapana hata kimoja." Sawa. Vema, yeye mwenyewe atawezaje kuzaa wakati amekufa nafsini mwake? Anawezaje kuwa mwanamwali wakati yeye ni kahaba? Unaona, hilo ndilo lenyewe. Hilo ndilo jambo lote.

258 Loo jamani, sasa tutakwenda kugonga jambo fulani la kina kirefu, lililojaa vitamini toka Mwanzo hadi Ufunuo. Tazama, na kahaba mkuu pamoja na binti zake wana matumbo ya uzazi ya kikahaba. Kifo tu ndicho kinachoweza kutokea kwao. Kama unataka kujiunga na shirika la dini, ukidhani uko sahihi, unaona kule unakotua. Unatua moja kwa moja katikati ya kifo. Kabisa tu. Kama huwezi kuliona hilo, wewe ni kipofu wa kiroho, unaona.

259 Sasa, hebu turudi nyuma sasa na tuanze tena na tulirejee jambo fulani. Mnakumbuka mahubiri ya Jumapili iliyopita yalikuwa nini? Mlango wa kuingia kwenye Nafsi. Mnakumbuka? Sasa, kuna tumbo la uzazi la kimwili; kuna tumbo la uzazi kwa ajili ya roho. Mnaamini hilo? Kuna tumbo la uzazi la kiroho na tumbo la uzazi la kimwili. Na dhamira ni tumbo la uzazi la roho. Kwa nini? Sasa kumbukeni, niliwaambia Jumapili iliyopita na kulichora hapa kwa ajili yenu, kuna milango mitano ya fahamu inayoingia ndani ya mbegu kutokea nje: unaona, kuonja, kuhisi, kunusa, na kusikia; tano upande wa ndani: dhamiri, na kadhalika, kutoka ndani-tano. Sasa kwenye upande wa uzima kuna mmoja tu. Yaani wewe una uhuru wa kuamua kukubali, kupokea, au kutoa. Unaona?

260 Hivyo ndivyo uzinzi-hivyo ndivyo uzinzi unavyofanywa kiroho. Wakati wewe, ukijua vyema kwa Neno la Mungu, kwa kuchanganua katika akili, unaingiza ndani uongo wa shetani dhidi ya Neno la Mungu-hilo ndilo hasa alilofanya Hawa. Kwa kuchanganua katika akili kwanza kulikokuja kwa kuamini uongo wa Shetani ndani ya tumbo la uzazi la damira yake, hilo likachafua nafsi yake, likaweka kifo katika nafsi; ndipo tendo la asili likatendeka. Na hiyo ndiyo njia pekee ambayo mwanamke anaweza kufanya uzinzi dhidi ya mume wake ni kwanza kumruhusu mwanamume mwingine amzungumzie hilo na ndipo ampokee mwanamume mwingine ambaye siyo mume wake. Ndipo awe amefanya uzinzi. Na wakati Bibi Arusi wa Yesu Kristo anaporuhusu maungamo ya imani na kanuni za imani zinazotungwa na mwanadamu vichukue mahali pa Neno la Mungu, anafanya uzinzi.

261 Je, Yesu hakusema, "Amtazamaye mwanamke amekwishazini naye moyoni mwake-amtazamaye mwanamke na kumtamani amezini naye tayari." Kwa nini? Aliliruhusu likaja katika akili yake. Hilo ni tumbo la uzazi; linaanzisha mambo yaendelee. Shetani anaingia ndani-tulipandwa kwa Neno.

"Siku moja nitaleta uzima duniani na kuiumba upya, na kuijaza nchi." Kile Hawa alichoshindwa kufanya, Mariamu alikifanya. Mariamu alichukua Neno. Hawa alichukua uongo wa Shetani. Mariamu alichukua Neno la Mungu. Na kupitia mbegu ya Mariamu dunia inajaa tena kupitia Bibi Arusi Wake, kupitia Neno, ataleta Utawala wa Miaka Elfu. Kupitia huyo Neno linakuja, na Neno linapandwa katika kila moyo uliochaguliwa tangu asili, na Roho hushuka na kuunywesha, na hawatakufa. "Nitamfufua tena siku za mwisho." Ee Ndugu na Dada, hilo-hilo ni halisi.

262 Ni kitu gani? - dhamira ni tumbo la uzazi kwa ajili ya Roho. Nini?-kuingiza au kutoa. Hivyo ndivyo wanavyofanya uzinzi, ni kuchukua-kuruhusu roho fulani ya Shetani iweke ndani yao jambo fulani dhidi ya Neno la Mungu; ndipo anakuwa amefanya uzinzi. Hawa alipokea (sikiliza hili) mbegu ya neno ya makosa, uongo wa Shetani, dhidi ya Neno la Yehova. Matokeo yalikuwa kifo.

263 Sasa, tutaliacha somo hili katika dakika chache zijazo, lakini nataka niwe nimelipangilia hapo vema kabla halijafika chini mahali nitakapoweza kuishia. Ninakwenda kuruka ukurasa mmoja hapa kuhusu hilo - katika dakika moja.

264 Sasa tazama, Hawa nini? Alifanya nini? Alipokea mbegu isiyo halali. Alilifanyaje?-kwa kuamini uongo wa Shetani. Wangapi wanasema hilo ni sahihi? Kwa nini, hakika ni sahihi, hakika. Alipokea uongo wa Shetani. Alileta nini kwa kufanya hilo? Shetani alisema, "Unajua hili ni tukufu. Hili ni jambo zuri mno. Ulijua kuwa uliumbwa kwa ajili ya

hilo? Mbona, uliumbwa kwa kusudi hili hasa."

"Ee, niliumbwa kwa kusudi hili?"

"Ee ni la kupendeza macho. Ni zuri. Unge-ungejaribu hilo."

"Lakini Bwana Mungu alisema 'siyo-siyo-siyo hilo, bado. Hatupaswi kufanya hilo! Hapana, hapana!" "Lakini, unajua-"

"Ee, tukifanya, tuna-"

"Ee, hakika hutakufa." Yule Shetani mwenye ulimi mwerevu. Hana kwato na mkia kama uma, hapana, kama wanavyojaribu kuwafanya muamini. Yeye ni mwerevu nyuma ya mimbara. Hiyo ni sahihi. Au mmoja wa hawa vijana wenye utovu wa adabu akiwa na nywele zilizochanwa na kuning'inia kama bata, akiwa amekaa chali pale tayari kumdhuru binti wa mama fulani. Huyo ndiye yule kijana mdogo mzuri anayekuja hapo. Ee, nitaliachia hilo.

265 Sasa, lile tumbo la uzazi-Hawa alipokea mbegu ya neno isiyofaa. Sasa, sikiliza kwa makini sasa. Tunakwenda kulizamisha hili chini mioyoni; Bwana akipenda. Alipokea neno lisilofaa. Hilo neno lilifanya nini?-ilikuwa uongo wa Shetani, alisema Hawa angekuwa mwerevu; mbona, angeweza kuwa wa kanisa kubwa, angekuwa anaheshimiwa vyema mjini; mbona, angekuwa kama wale watu wengine. Hakika, hilo ndilo hasa aliloamini bibi arusi wa Yehova. Hilo hasa.Hilo ndilo hasa Shetani angejaribu kulisema Neno lilipokuja kwa Mariamu, lakini yeye alimfukuzilia mbali.

Akasema, "Hili lawezekanaje?"

Akasema, "Roho Mtakatifu atakujilia juu yako. Ni Neno la Mungu."

Akasema, "Na iwe kwangu kufuatana na Neno Lako." Hilo lilileta Uzima. Hilo ndilo lenyewe.

Vema, je, ulijua kuwa Shetani alisema, "Wote watakucheka."

Yule msichana mdogo mwenye afya nzuri hakusikiliza hilo. Akaenda moja kwa moja Uyahudi na, "Unajua nitakuwa na mtoto"; kabla ya kuhisi lolote, kwa sababu Neno tayari limekaa pale. Hilo lilitosha. Haikumpasa kwenda kwenye mstari wa maombi mara ya pili. Naam, bwana; aliliamini hilo. Hakuwa na dalili yoyote ya kiumbe hai ndani yake hata kidogo; hakuwahi kuwa na dalili kamwe ya uja uzito, hakujisikia kitu chochote; kila kitu kilikuwa tu jinsi kilivyokuwa tangu awali, lakini aliendelea kumwambia kila mtu, "Nitapata mtoto." Kwa nini?-Mungu alisema hivyo. Hiyo ni nini?-Mbegu ya Kifalme ya Abrahamu.

266 "Nitapata mtoto, Abrahamu kwa yule mwanamke?" "Mungu alisema hivyo."

"Vema, uliniambia hayo miaka ishirini na tano iliyopita." "Ninajua, lakini Mungu alisema hivyo. Ndiyo hivyo. Hilo ndilo lenyewe. Ndicho kitu hicho hicho."

Unasemaje leo? "Vema, unajua dhehebu litakutupa nje."

"Lakini Mungu alisema hivyo; Mungu alisema hivyo" "Vema, unajua, ukibatizwa namna hiyo -"

"Vema, Mungu alisema hivyo. Ndilo hilo. Ndilo hilo."

124

Huyo hapo bikira wako; yuko hapo. Siyo kwa ubatizo tu, ila chochote kingine-Neno lote, unaona. Kwa hiyo,

267 nini … Hili lilikuwa yote mawili kimwili na kiroho kwa Hawa. Kwanza na wakati wowote-Sasa, nimekwishakuwaambia na nimewaomba asubuhi hii, akina dada, mnisamehe ili niweze kutaja kutaja hilo - wakati wowote ambao mwanamke anachukua hatua kufanya kosa - nazungumza kuhusu Kristo na Bibi Arusi sasa-lakini wakati wowote mwanamke anapochukua hatua ya makosa, inabidi kwanza aipokee katika mawazo yake. Hiyo ni sahihi. Mtu fulani mwerevu yampasa kumshawishi, naye anaisikiliza kinyume cha uamuzi wake mwenyewe uliopaswa kuwa bora zaidi. Ndipo tendo linafanyika. Kwa hiyo kwanza, lilimgonga Shetani-liligonga mawazo ya Hawa, na katika tumbo la uzazi la mawazo yake yeye alishuku Neno la Mungu ndipo likaja tendo halisi.

268 Na njia pekee ambayo tunaweza kuzaliwa mara ya pili ni kupokea kwanza Neno katika tumbo la uzazi la mawazo, na ndipo Roho huja juu ya hilo na kulileta hilo. Hilo

ndilo lenyewe. Hilo ndilo linalofanya hicho. Hilo ndilo fundisho halisi la Injili Ndugu. Naamini kama Mtakatifu Paulo angekuwa amesimama leo angefundisha jambo hilo hilo saa hii. Vema.

Matokeo yalikuwa nini kwa Hawa?-kifo cha kimwili na kiroho. Matokeo ni nini ya wale wanaopokea neno lingine, linakwenda katika huu mzaha walio nao leo?-kifo cha kimwili na kiroho. Mwili na roho vitaangamia vyote, havitakuwepo tena. Hiyo ni sahihi kabisa.

269 Tazama, tumbo la uzazi la Mariamu-Tumbo la uzazi la Mariamu, ubongo wake, unaona, ulikuwa tumbo la uzazi la bikira. Kwa nini? Aliliamini Neno la Mungu. Haidhuru mtu yeyote alilikosoa kiasi gani, vitu vingapi mtu fulani alivisema, hilo halikuhusika nalo; yeye aliamini Neno la Mungu licha ya hayo.

Ee, natamani ningeweza tu kuwawekea hilo mlione vizuri. Mnalielewa? Unaona, kwanza, ilikuwa mawazo yake. Kabla ya tendo kutokea katika tumbo lake halisi, lile tendo lingetokea ndani hapa kwanza ili kuruhusu Roho aingie, kufanya ile kazi nyingine yote. Ee, kabla ya kutokea kuzaliwa halisi kwa kiroho, lile Neno lingeingia katika akili yako; uliamini. "Yeye ayasikiaye maneno Yangu , na kumwamini Yeye aliyenituma, anao Uzima wa Milele, na kamwe hataingia hukumuni (au kupitia katika kipindi cha dhiki kuu), ila amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ndilo hilo.

270 Loo, jamani! Sasa tazama; tumbo la uzazi ni bikira, akili yake, ni akili bikira ya kuamini Neno la Mungu. Vema, unasema, "Ndugu Branham, isingeweza kuwa hivyo: haiwezekani. John Wesley angelikuwa ameliona hilo; Fulani angelikuwa ameliona hilo."

Hakika, shetani angeweza kumwambia Mariamu jambo lile lile: "Wewe ni nani? Kwa nini, wewe ni masikini kuliko wote hapa mjini. Wewe si chochote ila kijana, wa miaka kumi na sita-kumi na nane-chini hapa ukichota maji katika hii pampu; baba yako amekufa na mama yako akiwa mama mzee kipofu hapa. Sasa, itawezekanaje kwa vyovyote vile viwavyo - mama yake alikuwa Ana, tunaambiwa - itawezekanaje kwa vyovyote vile viwavyo upate …?"

"Sikiliza, mama yangu mzee ni kipofu, lakini ni mwanamke mcha Mungu. Amepanda mbegu moyoni mwangu kupitia midomo yake. Nimelisoma katika Neno la Mungu kuwa Mungu alisema katika Isaya 9:6: 'Bikira atachukua mimba.'"

271 Haleluya! Unaweza kuona Neno linachukua mwili. Ndivyo hivyo. Mungu anakwenda kuwa na Kanisa. Litazaliwa kwa Neno la Mungu kwa sababu ni Neno la Mungu lililo Hai. Unaliona?

"Unajuaje?"

"Kwa nini, ita-"

"Unajua kile unachokwenda kuitwa kuanzia hili na kuendelea? Unakwenda kuitwa …"

"Sijali kile ninachoitwa, hilo halihusiani jambo hili. Na liwe kwangu kulingana na Neno la Bwana."

Ee, kila mtu angeweza kusema hilo leo? Ee, kama watu wangeweza toka katika mioyo yenu hasa, sote, tungeweza kusema hilo, unaona … "Na iwe kwangu kulingana na Neno Lako, Bwana." Jamani! Umaanishe hasa. Mmoja au wawili au mahali fulani nje kule itachukua waliochaguliwa tangu asili wanaomaanisha hilo hasa, na, Ndugu, utaona cheche zikiruka, pale pale; hiyo ni sahihi-unapokuwa nacho pale kukutana nalo, lile linalokuja, ule ule umwagiliaji utakapoanza kuanguka juu ya lile Neno. Naam, bwana.

272 Sasa, kilikuwa kitu gani?-lile tumbo la uzazi la akili lililo bikira, tumbo la uzazi lililo bikira kwa ajili ya mtoto. Matokeo?-Uzima wa Milele. Hawa, akiwa mwanamke mzuri; kama alivyokuwa (akiwa mwanamke mzuri kama alivyokuwa, akiwa bikira kama alivyokuwa) akiwa bikira, kama alivyokuwa (akiwa mwanamke mzuri kaka alivyokuwa, akiwa kama alivyokuwa) lakini kwanza aliruhusu shaka kuingia kwa njia ya neno, uongo wa Shetani. Shetani alifanya nini?-aliunganika naye isivyo halali. Mtoto wa Hawa alikuwa nani?kifo.

Mariamu: akili iliyo bikira, tumbo la uzazi lililo bikira. Shetani alipojaribu kumjaribu, naye akaja-na malaika akamjia baadaye na kusema, "Utakuwa na mtoto," Shetani alisema, "Sasa ni vyema kukaa kimya kuhusu hilo." Malaika alisema, "Ni tendo la Mungu." Na bila shaka aliwaza juu ya Isaya 9:6; akasema, "Tazama mimi ni mjakazi wa

Bwana." Matokeo yalikuwa yapi?uzao wa bikira; Neno la Milele ndani yake, naye akaleta Uzima wa Milele.

273 Vema, bibi arusi wa Yehova, aliyechanganywa-bibi arusi wa Yehova, mbegu iliyochanganywa. "Ulisemaje sasa, Ndugu Branham? Asubuhi hii ulisema bibi arusi wa Yehova alifanya uzinzi."

Sitaliacha hilo. Sasa hebu tutazame kwa makini sasa. Sasa, tumebakiwa na kama saa moja, nadhani. Sasa ninayo baadhi hapa. Nitakwenda tu kuruka baadhi yake na kuanza kusoma katika dakika chache zijazo, unaona. Nisome tu kwa haraka tu niwezavyo ili kulileta jambo hili. Sasa saa moja nyingine naamini tutakuwa tumemaliza kama mtanivumilia na kuomba pamoja nami, unaona.

274 Sasa, ni wapi bibi arusi wa Yehova alikokosea? Vema. Yehova alituma nini kule Misri kwa bibi arusi Wake? Alimwahidi Abrahamu kuwa bibi arusi Wake, ile mbegu, ingekaa katika Misri kwa miaka mia nne. Hiyo ni sawa? Wakati ulikuja kwa ajili ya kutimizwa kwa Neno-je sisi ni wakati wa kutimizwa kwa Neno?-kwa ajili ya ukombozi, kutolewa nje. Vema, walilipataje Neno? Je, waliunda shirika la dini, kundi la watu pamoja (mapadre) na kusema, "Sasa, ndugu, tutakuwa na kura hapa, na limepita bila kupingwa kwamba tutakuwa na shirika la dini linaloitwa 'Mafarisayo' na kupitia hilo Mungu atafanya kazi"? Mungu hakuwahi kufanya kitu kama hicho, kamwe hakuwahi.

275 Je, Yeye aliwatumia nini?-nabii. Na Neno la Bwana lilikuja kwa nabii, alimwinua pale pale miongoni mwao, nabii, na kumpaka mafuta na kumthibitisha pale pale miongoni mwao juu ya kazi zile za mashetani, kwa miujiza na kila kitu kingine-kwa sababu Musa alikaa na Neno.

Alichukua lile kundi la watu: makutano ya watu mchanganyiko walianza pamoja naye. Walipovuka kuelekea nchi ya ahadi kabla hawajafika kule, bibi arusi Wake wa thamani alizini na Moabu. Niambie kama huyo bibi arusi wa Yehova hakulifanya hilo, sasa. Alilifanyaje? Nabii wa uongo aliyekuwa kinyume cha Neno la Mungu, hata hivyo alikuwa na ishara na yote - Mwenye kufuata taratibu zote za dini na ibada, alikuwa tu wa kiroho kama Musa au kama tu …?…

276 Tazama! Sikiliza! Sikiliza kwa makini sasa. Hapa amekaa Israeli kambini, wasiofungamana na madhehebu. Hiyo ni sahihi, ilikuwa nini? Walikuwa na nabii aliyepakwa mafuta pamoja nao. Alikuwa na Nguzo ya Moto, mwamba ule ambao ulitoa maji ili wanywe. Walikuwa wanendelea vizuri. Na tazama, walikuwa na madhabahu saba; hilo ni kamilifu. Juu ya madhabahu saba walikwenda wanyama saba walio wasafi-kondoo dume, na kondoo dume aliwakilisha kuja kwa Kristo.

277 Moabu-Kulitokea nini? Balamu alipokwenda kule, alijenga madhabhu saba, sawa tu na yale Israeli waliyokuwa nayo. Usizungumze juu yao kuhusu kanuni za msingi kwa sababu ni vyema ujue kile unachokizungumzia. Yesu alisema, "Lingewadanganya kama ingaliwezekana hata walio Wateule." Kufunua kiroho … Mnalielewa, lile Neno, na mnaona Neno likidhihirishwa.

Tazama, walikuwa hapa; na hapa kulikuwa na Moabu. Anaona-Hakuna shaka ila yeye alikuwa askofu, hakika, mtu mkuu, naye alijenga madhabahu saba. Aliweka kondoo dume saba juu yake-akisema kuwa yeye aliamini kuwa kulikuwa na kuja kwa Masihi. Ndugu, tukija kwenye usimamiaji wa mambo ya msingi ya imani, ilimpasa Mungu awatambue wote wawili.

Kaini alipomjengea Bwana madhabahu (Mwana wa Shetani, alimjengea Bwaana madhabahu), alijenga aina ile ile ya madhabahu aliyoijenga Abeli. Wote wawili waliabudu; wote wawili walikwenda kanisani; wote wawili walitoa zaka na sadaka zilizostahili. Wote wawili waliwajibika; walisujudu na kumwabudu Mungu yule yule - na mmoja alipokelewa na huyu mwingine akapotea. Inakuwaje?

278 Yesu alisema, "Juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa Langu." Kanisa Katoliki linasema, "Kuna mwamba pale, kanisa limejengwa juu yake; au ilena-Petro alikuwa huo mwamba." Na Kanisa Katoliki husema kuwa Petro amezikwa chini ya huo. Huo ni uongo, lakini-niwezavyo kuona wakati ule waliosema Petro alizikwa ndani pale, Biblia ilisema yeye alikuwa hapa Yerusalemu. Hakuwa kule - kamwe. Lakini hata hivyo, wanasema alikuwa kule. Kwa kweli hakuna kumbukumbu ya Paulo kuwa aliwahi kuwa pale, ila ni historia. Lakini wanasema Petro-Acha azikwe pale. Kama alizikwa pale, hiyo inaleta tofauti gani? Hilo halikuwa kile Yesu alichokuwa anazungumzia. Unaona, jinsi

walivyochanganya hilo jambo la kimwili.

279 Vema, Waprotestanti walisema, "Hapana! Yesu alisema Yeye alikuwa ule Mwamba."

Sasa, Yeye hakuwahi kusema hilo. Yeye alisema, "Heri wewe, Simoni mwana wa Yona; nyama na damu havikukufunulia hili"- "Wewe Ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu Aliye Hai." Nyama na damu - (Yeye hakujifunza hilo katika seminari.) "Siyo dhehebu fulani lilikufundisha hili, ila Baba Yangu aliye Mbinguni amelifunua Hili, na juu ya Mwamba huu (Kweli ya Neno la Mungu iliyofunuliwa kiroho) nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayatalishinda."

280 Moabu alifanya jambo lile lile. Alikuja chini kule, na akawafundisha wana wa Israeli; akasema, "Sasa tazameni hapa, marafiki." (Sasa hilo ndilo jambo lile lile walilofanya katika Pentekoste, sasa, tazama), "Sasa tazameni hapa, je, ninyi na sisi si wamoja? Je hatumwamini Mungu yule yule? Sisi ni wamoja." Wana wa Moabu walikuwa binti za Lutu. Unaona lile kundi lote lililotorokea chini kule? Bado ni "unywele ndani ya biskuti." Unaona? Ndio hao, waliozibwa vinywa. Unaona, walikuwa juu kule, nao walikuwa-"Kwa nini," alisema, "sasa, tazameni hapa, mnajua sisi ni wamoja." (Wangapi wanajua kuwa wale walikuwa watoto wa Lutu? [Hakika]-toka kwa baba yao mwenyewe - uzinzi.) Na wakasema, "Sasa, sisi ni wamoja. Unajua, ninyi Wamethodisti, na ninyi Wabaptisti, ninyi Wapresbiteri na wote; mbona hakika, tunahitaji baadhi ya mafuta yenu. Sisi wote ni wamoja." Nao walifanya nini? Walioa miongoni mwao! Na hilo ndilo Pentekoste ilifanya kwa Waprotestanti. Alioa katika Shirikisho la Makanisa; likajifanya lenyewe kuwa dhehebu, nalo liko wapi? Kama tu Israeli alivyofanya: alitengwa kwa yote mawili uasherati wa kiroho na wa kimwili. Mungu alimkataa tangu hapo na kuendelea. Hata wale watoto waliokuja kuwa Wasamaria walilaaniwa. Hiyo ni sahihi? Hakika alikuwa hivyo. Yehova alimwacha.

281 Bibi arusi wa Kristo alifanya jambo lile lile-alichanganya mbegu yake ya kidhehebu na kumwacha Kristo, mume wake aliyemchumbia. Nanyi kundi kavu la Wapentekoste; tatizo lenu ni nini? Ufunuo sura ya tatu na ile aya ya ishirini, tunakuta katika unabii, Yesu Kristo nje ya Kanisa Lake Mwenyewe katika hiki Kipindi cha Laodikia, akigonga mlangoni [Ndugu Branham analionyesha hili kwa vitendo mimbarani-Mh.] akijaribu kurudi-picha inayosikitisha kuliko zote katika Biblia. Bibi arusi wa Kristo alifanya nini? Aliingia kwenye ukahaba. Yesu ajapo, Yeye anagonga kwa ajili ya nani? Yesu anarudi kumpokea Bibi Arusi Wake; na Yeye alipokuja kugonga [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara sita-Mh.] mlangoni, Yeye alifungiwa nje.

282 "Kwa nini, huwezi kuja hapa; huwezi kufanya mkutano wa uamsho. Nipehebu nione vyeti vyako vya kusimikwa" - mtu aliyejazwa kwa Roho wa Mungu, Mungu halisi wa kweli-Neno la Mungu; Neno lilidhihirishwa katika huduma Yake. Hakuna jambo hata moja unaweza kusema dhidi Yake, la uovu au chochote. Nani awezaye kumshutumu Yeye juu ya hilo? Pitia dhehebuni: "Kwa nini yeye si wa Oneness; yeye si wa Assembly; yeye ni wa Utatu. Yeye si wa Utatu, yeye ni wa Assembly."

Ninyi maskini wanaharamu; aibu kwenu! Mungu akiwa nje; lakini Yohana alisema nini yule mjumbe wa mwisho kule kabla ya kuja Kwake)? "Yeye anaweza kumwinulia Abrahamu watoto katika mawe haya. Msije mkisema, 'sisi ni wa hili na sisi ni wa lile Mungu anaweza … kumwinulia Abrahamu watoto katika haya mawe."

283 Vema, tupoendelea sasa. Ee, ninalipenda hili mno! Bibi arusi wa Kristo, kama tu bibi arusi wa Adamu na wengine wote, walichanganya mbegu na kumtoa Kristo nje ya dhehebu lake, huyo bibi arusi. Hakika alifanya hivyo. Kwa kweli alifanya hilo. Alimkataa Mungu (mume wake wa baadaye) kama Hawa alivyofanya, alipokea magugu ya uongo wa kifo wa Shetani: kanisa lenye taratibu za kidini zilizokufa limezaliwa kutoka kwake. Sasa, unadanganya … unasema huo ni uongo!

Wapentekoste wenu wako wapi?-wana taratibu za kidini kuliko walivyo Wabaptisti. Hakika, unajua nini? Inaonekana kama picha mbaya sasa hivi, sivyo? Lakini Yoeli alisema nini katika Yoeli 2:28? "lakini nitarejesha, asema Bwana."

Hiki kipindi cha Laodikia-akigonga [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara nne-Mh.] mlangoni akijaribu kurudi-picha inayosikitisha kuliko zote katika Biblia.

284 Kama Adamu alivyomkuta mke wake akiwa na mimba ya mbegu ya kifo ya uongo wa Shetani aliouamini, Yusufu alimkuta mke wake akiwa na mimba ya Mbegu ya Mungu, ambayo ni Neno aliloliamini.

Haya yote yanahusu nini? Kitu gani ninachojaribu kusema? Sasa, kwenu ninyi watu mnaosikia kutoka vyombo vinavyonasa hewani, ninyi watu mlioko kwenye magari, kwenu ninyi watu mlioko hekaluni, je mnaona ni kwa nini nimekaa jinsi nilivyojaribu kukaa hapa na kushutumu hilo? Sio kwamba nina lolote dhidi ya wale wanaume, wale wanawake; sina hata jambo moja kinyume nao, lakini siwezi tu kuendelea juu ya - hiyo misingi. Siwezi tu kufanya hilo, kwa sababu ni makosa.

285 Jinsi-Nina Andiko hapa ningependa kulichukua juu ya Yesu, juu ya kujaribiwa Kwake; wakati Shetani alipojaribu kumpa Yeye, akasema, "Nitakupa hizi falme, zote za ulimwengu. Ni zangu." Unaona? Jambo lile lile alilokuja nalo kwa Hawa (unaona?) kwanza, kwa kubadilisha mkate-kuhusu kula na kadhalika-unaona. "Nitafanya hili lote kama utaniabudu-uje tu ujiunge na kundi letu …"

Yesu alisema, "Imeandikwa, 'mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.'"

286 Ni kitu gani? Baadhi yenu wahubiri sasa, mnahofia sana kushikilia msimamo wenu; mkiogopa kuwa hata hawatawaruhusu kuja katika shirika la dini: "Kipi kingine mtakachokifanya basi?-watawatupa nje!" Nawasikitikia. Jambo la kwanza, kwa udhaifu wenu. Hiyo ni sahihi. Imani yenu iko wapi katika Mungu? Waliniambia jambo lile lile. Hakika. Nimefanya kazi miaka kumi na saba, hadi Mungu aliponitoa nje na kunijenga katika hili, na ndipo nikawaza, "Sasa, Shetani na uje sasa." Tazama liliko. Unapotambua hakika kuwa Mungu amekufunulia Kweli ya hilo jambo, hakuna chochote ulimwenguni kitakachokushinda katika hilo. Ni hivyo tu. Huwezi kushindwa hata kidogo; sio wewe, ila Mungu aliyeko ndani yako. Sio Kristo, ila-sio mwili, ila lile Neno lililokuwa ndani Yake. Sio Mariamu, ila Neno lililozaliwa kutoka kwake.

287 Sasa, kwa hiyo mtu ataishi kwa kitu gani?-sio kwa tikiti yake ya chakula, ila kwa Neno la Mungu; sio kwa shirika lako la dini linalokupatia mahali. "Vema, ngoja niwaonyeshe hati zako za utambulisho. Je upo kwenye msimamo mzuri? Yanipasa niukague. Vema, naam, unaweza kuwa na cheo kwenye asilimia mia moja. Vema, tunaweza kukupokea kwa siku chache kwa ajili ya uamsho, kukujaribu tuone utakachofanya." U-u-u jamani! Mungu awezaje kufanya kazi katika kundi kama lile?-lililokufa maradufu, lililong'olewa kutoka kwenye mizizi, lililong'olewa, lililooza na kila kitu kingine. Lo, jamani, kuna lingine moja.

288 Ee, watu, Mungu awabariki. Nisikieni! Siwezi kuamini lolote ila Neno la Mungu na nataka liwe uhai wangu, kila kitu nilicho. Nataka mfanye vivyo hivyo. Hebu matembezi yenu, maongezi yenu, kwenda kwenu, kila kitu mkifanyacho, muwe katika Neno la Mungu. Hebu dhamira ya Kristo ije ndani yako, na hiyo itakupa mimba kwa Neno. Ikiwa sivyo-kama ukiruhusu dhamira ya dhehebu iingie, utapata mimba ya kidhehebu. Ukiruhusu dhamira ya Kristo iingie ndani yako, Yeye hawezi kulikataa Neno Lake Mwenyewe kwa sababu Yeye ni Mungu. Utapata mimba kwa Neno na kuliamini. Sijali kama wakikuweka nje, wakikutupa nje, wakikufukuza, na kila mlango umefungwa, utaendelea tu hata hivyo! Amina! (Loo!) Inanipasa kuharakisha.

289 Jamani! Kristo sasa anajipatia Bibi Arusi Yeye Mwenyewe ili apate mimba kwa Neno Lake Mwenyewe lililo Mbegu ndani ya tumbo la uzazi la Bibi Arusi (tumbo la uzazi la kiroho) na … ndani ya dhamira Yake (Bibi Arusi), na haitachanganyika na takataka yoyote ya kidhehebu. Yeye (Bibi Arusi) ni bikira Kwake (Kristo).

Ee, nakumbuka nikiwa nimeketi pale chumbani, siku tatu ndani pale nikiomba na nikimsubiri Bwana na kufunga. Wakati lile liliponigonga nikawaza, "Ee, Mumngu ni kitu gani? Niko hapa katika picha, nipo hapa! Kama nikilileta hili lote kwenye kanisa, nitakuwa wapi? Nitakuwanitawaweka mahali pa hatari, nifanye nini? Nimekwishaona kanisa kama kila mfano na kivuli na kila kitu kingine-inaonyesha limeshakwisha. Utafanya nini?

Na ndipo, nikawaza juu ya lile Neno. "Nitarejesha, asema Bwana; nitarejesha." Kumbuka, ule mti wa kale wa msonobari; moto unapoufikia na kuuteketeza kabisa, hata hivyo unapukutisha mbegu. Ile mbegu inaleta msonobari mwingine. Hiyo ni sahihi. Ile miti ya zamani inaunguzwa na shirika la dini na kila kitu kingine, lakini bado kunabaki Mbegu ya Neno, na kama … Neno la Mungu, itarudi moja kwa moja na kujizaa tena kwa hakika tu kama ulimwengu. Ndiyo, sasa, sasa, hawezi kulikosa hili.

290 Tazama, lakini Kristo-tunaamini tupo katika wakati wa mwisho, sivyo? Je, unaamini kuwa kabla hujawa na zao sasa, inakupasa upande mbegu? Unaona ni kwa nini

nimewaachia makanisa yanitoe nje, yakiniambia kila kitu; yakiniita namna zote za majina na kila kitu kingine na nikakaa sahihi na lileNeno? Unaona? Kuna mmea; mbegu imepandwa; imepandwa tayari, marafiki. Tayari imekwisha. Naweza kulisema sasa: imekwisha. Hiyo ni sahihi; imekwisha kupandwa (ee, naam); vivyo hivyo na mbegu ya kidhehebu, nyingine zote.

291 Kama ndugu yetu mkuu na wa thamani Billy Graham alivyosema hapa hapa Louisville-alisema, "Paulo angechukua Biblia-" alichukua Biblia na kusema, "Sasa Paulo angeweza kwenda mjini na kuwa na mikutano ya uamsho. Mtu mmoja angeokoka; angerudi pale mwaka uliofuata naye angekuwa na wengine sitini kutokana na yule mmoja." Akasema, "Naweza kwenda na kuwa na mikutano ya uamsho ya wiki sita na watu ishirini elfu wakaokoka na nikirudi katika muda wa miezi sita huwezi kukuta ishirini!"

Ni kitu gani? Hawajaokoka! Wao waliokokea udhehebu, ni hivyo tu. Hakika, inakupasa upande mbegu - unaona, unapanda mbegu ya kidhehebu, hicho ndicho unachokipata. "Njoo sasa, Ndugu; jiunge na kanisa; weka jina lako kitabuni." Hilo tu ndilo wanalolijua. Hiyo ni sahihi.

292 Pentekoste imefanya hivyo hivyo. Wananena kwa lugha na kadhalika. Hilo ndilo tu linalokupasa kufanya; basi umekwishampata. "Njoo; jiunge na kanisa." Vema, upate ubatizo wako wa makosa na kadhalika na uendelee, na hilo tu ndilo likupasalo kufanya. Unaona?

Lakini Kristo ajapo, Yeye anakuja kwa ajili ya bikira na-Kanisa lisilokuwa hata na doa moja au kunyanzi moja la kidhehebu au kitu kingine chochote, kanuni za imani zilizotungwa na dhehebu na kuchanganywa nalo. Litakuwa Neno na hilo pekee.

293 Sasa! Loo, jamani, hapa tumefika! Jina la Bwana libarikiwe! Sasa tunakuja kwenye Mwili kuwa Bibi Arusi wa Kristo. Kuwa nyama ya nyama Yake sasa, na mfupa wa mfupa Wake. Kwa nini-(nakuuliza swali) kwa nini mvua zenu zote kule nyuma hazikumleta Bibi Arusi kwa Kristo? Nataka mnijibu hilo!

Kama linajitokeza na limepitiliza muda wake; tunaliamini. Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, uvumilivu. Yeye anamwandaa Bibi Arusi Wake. Kwa nini hizi mvua-kwa nini ninyi Wapentekoste nyuma kule miaka michache iliyopita (mlipoanza miaka arobaini au hamsini iliyopita)-kwa nini hamkumleta Kristo, Bwana Arusi, kwa Bibi Arusi? Nitaliacha hilo lilowane kwa dakika moja. Kwa nini? Kwa sababu mlimpa mimba ninyi wenyewe kwa madhehebu yenu; hilo ndilo hasa mlilofanya. Yeye hawezi kumwoa kahaba. Atamwoa bikira. Nimeliweka katika hali ya uwazi sana, lakini hiyo ndiyo Kweli. Ulijue katika hali ya uwazi. Hupaswi kushangaa. Sibabaishi kuhusu hilo; nawaambia Kweli.

294 Kwa nini hamkumleta? Kwa nini hamkumleta Kristo-hamkumleta Kristo kwake? Kwa sababu bibi arusi hafai. Yeye alimkuta huyo bibi arusi kwenye uzinzi - ndiyo sababu hasa watoto hawaishi milele wanapozaliwa. Adamu alimkuta mke wake ana mimba. Hiyo ndiyo sababu ilimpasa Yehova kumchukua bibi arusi wa Mataifa-alimkuta bibi arusi wake ana mimba. Hiyo ndiyo njia hasa ambayo Kristo itampasa kujipatia Mwenyewe Bibi Arusi sasa. Yeye amelikuta hili linaloitwa kundi likiwa na mimba. Yeye anakwenda kusia Mbegu Yake; mtu fulani ataipata, kwa sababu wamechaguliwa tangu asili kuwa Kanisa mwishoni mwa safari.

295 Kama Adamu na Yehova, wao walikuta wa kwao wamepewa mimba kwa mafundisho ya kibinadamu ya madhehebu. Kama Kweli ya Mungu katika Mwanzo moja, kila mbegu imezaa kwa jinsi yake, hivyo wakati Roho alipomshukia Bibi Arusi huyo, mwanadamu alikwishakuwa pale kwenye tumbo lake la uzazi na kulijaza kwa mbegu za kidhehebu za mawazo yake mwenyewe, kwa hiyo hiyo ndiyo sababu akawa jinsi alivyo, na Kristo hakuweza kuja kwake. Umm, hilo ni gumu, sivyo?

296 Siku moja, nilikuwa juu kule Green's Mill, nilikuwa nikiomba kwa siku kadhaa; imekuwa miaka mingi iliyopita. Nilikwenda juu pale Mishawaka. (Sikuwahi kusema hili kwenye kanda hapo awali.) Nilikwenda Mishawaka. Mnakumbuka kuhusu yule mvulana mweusi? Niliwakuta watu wa

Kipentekoste; sikuwahi kujua kulikuwa na kitu kama hiki. Na nikaenda juu kule na kuwakuta, na nikawaza kuwa nilikuwa na kundi la malaika. Niliwaona wakinena kwa lugha na mambo kama hayo. Sikuwahi kulisikia hapo awali, lakini walikuwa pale,

wakikimbia huku na huku sakafuni wakinena kwa lugha. Nikawaza, "Jamani, hilo ni zuri sana!" Ile U.P.C na P.A ya zamani na aina zote hizo zilizoinuka. Walikuwa na-ilikuwa ni ubaguzi kati ya weupe na weusi; wao walilazimika kuwa na mkutano wao kule kaskazini. Na ulikuwa kule Mishawaka, Indiana.

297 Jamani! Nilikuwa na dola moja na senti sabini na tano-kiasi cha kunitosha tu kufika nyumbani. Nikatumia senti thelathini kati ya hizo katika kibanda cha zamani nikanunua - donati au keki ndogo za mviringo (zilizokwishakaa siku mbili au tatu hivi) nikateremka chini pale penye bomba la maji kando ya barabara, na kuteka kombe moja la maji, na nikaenda kwenye shamba la nafaka na kuchukua viti vyangu toka kwenye Ford yangu ya zamani na kuvilaza chini; nikalala usiku ule (nilikuwa nimevaa suruali yenye miraba) na fulana ndogo yenye mikono mifupi. Na asubuhi iliyofuata nikateremka tena. Sikutaka kula nao. Nilikaribishwa, lakini sikutaka kula nao kwa sababu sikuwa na chochote cha kutoa mchango.

Na kwa hiyo nilikwenda kukuta kuwa siku ile wangecheza dansi; na walikuwa wawe na mchezo wa kurukaruka kwa furaha; wangeimba katika Roho. Na nikawaza, "Ee, jamani, hilo linaonekana zuri! Um!" Mtu mmoja angeinuka na kunena kwa lugha, na huyu atoe tafsiri. Na, Ndugu, ilikuwa hivyo. Waliwaita watu nyuma kule kwenye kusanyiko, "Ee, Ndugu, hilo lilikuwa zuri sana!"

298 "Mwambie Dada Jones au Fulani, aje sasa hivi; Bwana anamwita"anakuja hapa. Hiyo ni sahihi.

Ndipo, huyu mmoja angenena kwa lugha, na mwingine angetafsiri. Nikawaza, "Loo, jamani! Jamani! Ule Utawala wa Mika Elfu unajiandaa kuanza. Ndio huu." Na kwa hiyo-niliwaza, "Kama tu ningeshika mikono ya hawa watu watauwa." Na nikamwendea mmoja wao nilipokuwa nje nikitembea huku na huku. Hawakunijua; Nilikuwa mtu mdogo pale. A kwa hiyo nikawa nikitembea kulizunguka kanisa na baada ya muda mfupi walipokuwa na mapumziko mafupi, nikakutana na mtu nje kule na-alikuwa mmoja wao-na nikashikana naye mkono na nikasema, "Hali yako Ndugu?"

299 Sasa, unajua Mungu amenipa karama ndogo hapa kupata mambo Yeye anapotaka mimi niyajue, unaona. Nikawaza, "Ikiwa ningeweza kumfanya anene na aseme jambo fulani, ningeweza kutambua kama lilikuwa kweli au la." Kwa hiyo nikamwona yule kama kingozi wake, na tukasalimiana kwa kushikana mikono. "Hali yako Ndugu?" akasema, "Hujambo?" Na nikaongea naye kidogo, naye alikuwa Mkristo halisi; alikuwa hivyo, nami nikawaza, Mungu atukuzwe!"

Baada ya muda nikaja kwenye kona na nikamkuta huyu mtu mwingine, na nikasema, "Hali yako Ndugu?" na nikaongea naye. Na kama niliwahi kuongea na mnafiki, yule alikuwa mmoja wao. Alikuwa mtu mwenye nywele nyeusi kichwani, na alikuwa na mtoto na mwanamke mwenye nywele za rangi ya shaba-watoto wawili kwa yule mwanamke mwenye nywele za rangi ya shaba. Nililiona katika ono, pale pale mbele yangu.

300 Sasa, nikawaza, "Sasa, nimechanganyikiwa kweli. Sasa, jinsi gani Roho yule yule-mmoja awe juu ya mtu-mtu mtauwa na mwingine juu ya Shetani, mnafiki?" Nikawaza, "Mungu, bora niliache lile jambo peke yake, sijui." Nilikuwa na umri wa miaka kama kumi na tisa, ishirini hivi, na nikawaza, "Ni bora tu niachane na lile jambo. Vema, sijui. Ingeliwezekanaje ulimwenguni jambo kama hilo? Siwezi kusema chochote kuhusu hilo, Siwezi kusema chochote dhidi ya hilo, lakini najua ya kuwa yule mtu yuko makosani." Na yule yule Roho, ningemwona, alishuka pale na kufanya kitu kile kile.

Nikawaza, "Kuna tatizo fulani hapa mahali fulani. Hilo ndilo lililokuwepo.

301 Nikamwambia huyu mtu-Yeye akasema, "Umewahi kumpokea Roho

Mtakatifu?"

Nikasema, "Siamini kuwa ninacho kile mlicho nacho ninyi."

Akasema, "Utukufu kwa Mungu! Umewahi kunena kwa lugha?"

Nikasema, "Hapana, bwana."

Akasema, "Huna Roho Mtakatifu."

Nikasema, "Vema, sidhanii kuwa ninaye." Unaona? Nikasema, "Hiki ni kitu kipya. Sijawahi kukiona au kukisikia." Nikasema-

Akasema, "Vema, ingia ndani pale umpate … hakika, ni wako."

Nikasema, "Asante bwana." Nikawaza, "Ndugu, sitaki kile ulicho nacho!" Ndipo basi nika-nikakitazama kidogo, na nikakizunguka kwa muda kidogo, na nikaendelea kuzungukazunguka, na nikaenda nje kwenye miti usiku ule, na kuwaza, "Mungu, nirehemu, nakwenda nyumbani." Na nikaenda nyumbani. Singeweza kusema lolote kuliunga mkono au kulipinga.

302 Wakati mmoja, nilikuwa juu hapa Green's Mill (pango langu dogo la zamani pale ambapo siku zote nakwenda mnapopajua). Nimekuwa pale kwa ajili ya jambo lingine. Siku nne au tatu nimekuwa pale nikifunga na kuomba. Ndani ya pango kumeharibika, na nilitoka mchana mmoja na-kuzuri na jua lilikuwa linawaka-majani. Kulikuwa na gogo la zamani lililoanguka chini namna hii chini yake tu (chini kuelekea kwenye kile kijito kidogo), na nikaketi chini pale nikifikicha macho yangu (nimekuwa kule kwenye pango la giza kwa muda). Na nikaweka Biblia chini namna hiyo, na nikawaza, "Vema, Naamini nitasoma baadhi kwenye Biblia." Na nikaegemea nyuma juu ya huu mguu hapa na nikajipumzisha tu mwenyewe na kuegemea kurudi nyuma; nilikuwa nimetapakaa vumbi mwili mzima.

303 Na nikaanza kusoma, na niliponyanyua Biblia, ilkuwa ni Waebrania ile sura ya 6, unaona. "Kwani haiwezekani kwa wale waliokwisha kuiona nuru; wakafanywa washiriki wa Roho Mtakatifu, kama wakianguka, kujifanya upya tena kwa kutubu. Kama-mvua ikija juu ya nchi mara kwa mara … kuibariki na kuiandaa … kwa ajili ya ile … miiba na michongoma, ambayo inakaribia kukataliwa … itateketezwa."

Nikawaza, "Vema, hicho ni kitu gani?-Simama!" Na nikawaza, "Hicho kilikuwa kitu gani?" "Ee," Nikasema, "Nadhani ni kitu fulani"-nikaondoka. Sikuwa-Nilikuwa juu pale nikiomba kuhusu jambo lingine. Na nikaiweka Biblia yangu chini tena. Nikasema, "" Vema, nadhani nitaifungua nipate kitu cha kusoma," namna hiyo, na upepo ukaja na kuirudisha nyuma. Nilikuwa katika Agano la Kale; ukairudisha nyuma kwenye Waebrania sura ya 6.

Nikatazama chini tena, na lile lile lilikuwa pale. Kwa hiyo nikatazama; nikaiinua, na kulisoma tena, jambo lile lile. "Vema," Nikawaza, "jamani! Bill, unakuwa mshirikina?"

304 Kwa hiyo, nikawaza, "Vema, nitapasoma hapa," na sinkuweza-nikaanza kusoma, na sikuvutiwa na chochote. Nikawaza, "Vema, naamini nitainua tu mikono yangu na kumsifu Bwana." Nikailaza Biblia chini namna hiyo; nikanyanyua mikono yangu kumsifu Bwana. Nilipoinua mikono yangu, upepo ukavuma, "whoosh," [Ndugu Branham anatoa sauti ya upepo-Mh.] ukavuma tena, na ulipovuma, nikatazama chini pale: Waebrania 6. Nikapasoma tena. Nikawaza, "Hilo linamaanisha nini? Sielewi." Nilikuwa nimesahahu kuhusu lile wazo la Kipentekoste. Ndipo-nikawaza, "Hilo linamaanisha nini?"

305 Na nilikuwa nimekaa pale na nikawaza, "Je, kuna kitu ndani pale Bwana?" Nikawaza, "Sasa, naamini katika kuteuliwa, naam-'wale waliokwisha kutiwa nuru; washiriki wa Roho Mtakatifu (unaona?), na wakaonja Neno la Mungu-'" Nikasema, "Hao ni wale waamini wa mpakani wanaokuja karibu kwenye jambo halisi na baadaye kurudi nyuma; kama wale waliokuwa katika wakati wa Yoshua." Yashua na Kalebi waliendelea, lakini hawa walikaa tu kwenye mpaka, unaona, walionja na kuona matendo mazuri ya Mungu, halafu wakayakataa.)

Watu huketi kanisani wakati wote, wakisema, "Naamini hilo, Ndugu Branham," lakini kamwe hawachukui hatua kuliendea. Unaona, haiwezekani kuvuka. Kwa hiyo basi huja mahali pale, na unahubiria wanawake wenye nywele fupi; mwaka unaofuata wana nywele fupi, hivyo hivyo. Wahubirie kwamba-wanafanya tu jambo lile lile, unaona. Kamwe hawaoni-waamini wa mpakani. Unasema, "Ee, ndiyo, naamini ni sahihi."

306 Nikasema, "Kwa kweli naamini hilo." Lakini hili-linapokuja mahali pale"Lakini michongoma na miiba ambayo inakaribia kukataliwa, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa." Nikawaza, "Hilo linamaanisha nini? Siwezi kulielewa."

Na nilikuwa nimekaa …?… na nikawaza, "Mungu, ikiwa hili ni jambo fulani unalotaka mimi nilijue, nipo hapa nikitafuta ono kutoka Kwako, Bwana, nijue tu kile cha kufanya kuhusu huduma chini kule, na nataka uniambie, Baba." Na nikatazama na nikaelekea (nilikuwa njiani juu ya Charleston)nikielekea New Market, njia ile (kukatisha kile kilima), na nikatazama na nikaona kitu kama upinde wa mvua ukining'nia juu ya bonde. Na katika huu upinde wa mvua, nikaona kitu fulani kikigeuka, na nikatazama, na kilikuwa

ulimwengu. Na hapa akatokea mtu aliyevaa vazi jeupe.

307 Sasa, wengi wenu ninyi watu hapa ni wachanga mno kujua hili. Mnakumbuka, tulipokuwa tunatangaza mbegu kwa-unaweka mfuko mkubwa sana pembeni mwako, na kutoa mkono wako na kuutupa? Bw. Wood, utakumbuka hilo-kutangaza mbegu namna hiyo. Unazichukua katika mikono yako na kuzitawanya namna hiyo. Unaacha upepo uzivumishe kwenye uchafu.

Na nikaona mtu aliyevaa vazi jeupe akikatisha namna hiyo, akisia mbegu. Na nikamtazama akienda sawasawa na mpinduko wa dunia. Na nikawaza, "Nashangaa hilo linamaanisha nini." Na ndipo, nikatazama; mara tu alipogeuka, hapa akaja mwerevu halisi, akija, akitazama namna hiyo. Alikuwa na gunia lililojaa na alikuwa akipanda magugu, nyuma yake. Alizunguka dunia; bado akitazama, akinyatia na akizirusha namna hii, na akaendelea kuizunguka dunia.

308 Ndipo nikaliona likija, na ngano ikaota na magugu yakaota, mashona nguo, miiba, michongoma. Na vyote vilikuwa vinakua pamoja. Na ukaja ukame mkuu, na nikaona ile ngano changa ikining'iniza kichwa chake, ikienda [Ndugu Branham anaigiza sauti ya kupumua kwa shida wakati wa kukaribia kufa-Mh.] kufa tu kwa ajili ya kukosa maji. Na nikaona mche mchanga wa miiba ukiwa unaninginiza kichwa chake [Ndugu Branham anaigiza sauti ya kupumua kwa shida wakati wa kukaribia kufa-Mh.] ikifa kwa kukosa maji. Na kila mtu akaanza kuomba maji, na mara moja mvua kuu ikanyesha kama jibu la maombi. Na mvua ikanyesha dunia nzima, na mara yale maji yalipoipiga dunia, ile ngano changa iliruka na kusema, "Utukufu! Utukufu! Utukufu! Utukufu!" Na mche wa miiba ukaruka na kupiga kelele, "Utukufu! Utukufu!

Utukufu! Utukufu!"

Vema, nikawaza, "Sasa hicho ni kitu gani?" Na ndipo tu-"Vema, ile ngano ilikuwa inapiga kelele, naweza kuona hilo; lakini ule mche wa miiba unamaanisha nini?" Ndipo Yeye akasema, "Soma Waebrania 6."

309 Mvua hunyeshea wenye haki na wasio haki. Hilo ndilo lililopo; hiyo ndiyo sababu hatukuwa na Bibi Arusi tayari kwa ajili ya Kristo sasa. Tulipanda mbegu za kidhehebu badala ya Neno. Imefanya nini?-ilileta watoto wengi zaidi wa kidhehebu. Hiyo ni sahihi. Lakini miongoni mwao kuna ngano iliyoanguka. Hiyo ni sahihi.

Lakini tazama, ile ile Roho inayomfanya mwamini halisi, wa kweli na halali kunena kwa lugha, ile Roho halisi inayomfanya mwamini Mkristo halisi (unaona, kwa sababu Inanyeshea Neno, Mbegu), ile ile Roho hufanya kitu cha badala yake, kama kuchanganyisha mbegu kwa Hawa, hufanya mbegu iliyochanganywa kuwa na furaha kiasi hicho hicho, kupiga kelele kiasi hicho hicho, kuwa na kufurahia hilo kiasi wanachofurahia wale wengine. Lakini Ukweli wake ni nini? Kutoka mwanzo ile ni mbegu ya makosa!

310 Kwa hiyo maonyesho yenu ya kimwili hayamaanishi chochote! Hata nikinena kwa lugha za mwanadamu na za malaika na sina upendo, hainifaidii mimi kitu. Hata kama nikiweza kuhamisha milima na sina upendo, hainisaidii kitu. Hata nikitoa mali zangu zote kulisha masikini na sina upendo, hainifaidii kitu. Kama nikinena kwa lugha kama mwanadamu na malaika, inakuwa shaba inayolia na upatu uvumao. Unaona, si chochote. Sikiliza, kanisa: Wapentekoste-si chochote! Kwa nini? Ni mbegu iliyochanganywa. Haiwezi kuja kwenye Neno.

311 Sasa, upo penyewe. Ule mwili unaozaa mwili wa Kristo tena lazima uweutoke kwenye tumbo la uzazi lililo bikira. Lile Neno, sawa! Hiyo ndiyo sababu-sikiliza hili-hiyo ndiyo sababu alizaa "milioni moja zaidi katika arobaini na nne." (Huo ulikuwa wito wa Kibaptisti wa kuwavuta watu) Hiyo ndiyo sababu madhehebu ya Kipentekoste yale-hayangeweza kutoa uzao wa kiroho kuleta madhihirisho na Kristo, kwa sababu ilikuwa tu mvua ya kusia mbegu, na linaleta kanisa la kidhehebu, na limejifungamanisha na - na madhehebu makuu ya Kiinjili, na limekwenda katika njia ya Kora. Limekwenda na madhehebu, hiyo ndiyo sababu.

312 Sasa hebu turudi nyuma kwenye Agano la Kale kwa ajili ya mifano, na ndipo ninakwenda kuanza katika dakika chache juu ya jambo fulani na niwaache mwende. Hebu turudi nyuma kwenye Agano la Kale kwa ajili ya mifano ili kuthibitisha haya mambo. Sasa, nimechukua masaa kadha hapa, nikiweka msingi huu. Sasa, tunakwenda kubadili somo, kubadilisha utaratibu. Sasa, kwanza, nina jambo fulani, nitakapofikia -

nina kurasa chache hapa, na ndipo nitaliendea - Loo, jamani, jamani, jamani - hakika siyo hilo! Inanipsa tu niharakishe kweli kweli. Sasa nitalisoma, unaona. Kwa haraka tu niwezavyo, kwa sababu najua hatuna muda ila mchache tu sasa, unaona. Sasa, mmechoka? [Kusanyiko linajibu, "Hapana."-Mh.] Hapana! Vema, basi ni mimi. Endelea, hiyo ni sawa.

313 Sasa, hiyo ndiyo sababu tuna haya mambo yote tuliyo nayo. Sasa haya mambo yote niliyosema, ikiwa hayaendani na Biblia - hayaoani na Neno la Mungu-ni makosa. Ni makosa. Na picha hii yote-sasa, nakwenda kuharakisha juu ya baadhi ya hili (sio kulieleza, ila tu kuliharakisha ili tuweze kulifikia; nawaahidi, kwa haraka tu niwezavyo).

Nina mahali hapa ambapo niliingia sana katika Roho. Nilikuwa-Niliandaa kaanisa nilionyeshe na kulihakikisha katika Neno hapa kile hasa ambacho kimekuwa kikitokea wakati wote huu, na ndipo nilipofanya, nikawaza, "Bwana, ninao watu waliosimama hapa sasa-nitakuwa nao wakiwa wamesimama kule; nitawaambia nini? Siwezi kutabiri ya mbele. Siwezi kuwaambia la kufanya. Nitafanya nini? Nitawaacha wakiwa katika hali ya hatari." Na nikainua mkono wangu na kusema, "Mungu, nadhani nafanya hili kwa mapenzi Yako. Sikuwahi kufanya hili, sikuwahi kulifanya huko nyuma."kwa sababu mbegu ilikuwa haijapandwa bado. Nikasema,, "Sasa, nina-nanaamini ni wakati wangu wa kulisema; lakini sasa, nitasema nini sasa?"

314 Na kwa dhahiri tu kama unavyosikia sauti yangu, kitu fulani kikasema, "Chukua kalamu yako." Nitawasomea kwa dakika moja. Na nilipomaliza lile jambo likawa pale, lile jibu tu. Wala sikuwa nikijua hata kile nilichokuwa nikikiandika. Nilianza tu kuandika; na nilipomaliza, nikaweka kalamu chini; na nikatazama juu, "Ee, Mungu unirehemu, lile jambo likawa pale, papo hapo. Hilo ndilo ninalolitafuta." Sasa, kuna jambo fulani yanipasa niyaruke. Tutalifikia baadaye kidogo, Bwana akipenda.

315 Agano la Kale lote lilikuwa mifano inayoelekea kwa Kristo na Kanisa Lake.. Unaamini Adamu na Hawa walielekeza kwa Kristo Na Kanisa Lake? Unaamini Yehova na Mke Wake walielekeza kwa Kristo na Kanisa Lake? Vema, ikiwa wao ni mifano na hili ni kinyume na mfano, lingepasa liwe kama mfano, kwa sababu mfano huchukua toka kwenye-toka kwenye-kinyume cha mfano huchukua toka kwenye mfano. Kristo ni Kichwa, Jiwe halisi la Mungu. Unaamini hilo? Lile Neno la kweli. Bibi Arusi ni ule Mwili.

Mnahitaji Maandiko juu ya haya, ili muweze kuyaangalia? (Nilikuwa niyasome Maandiko, lakini sitafanya hivyo.) 1Petro 2:1-6; Waefeso 5:22; (unaona?) 1Petro 2:1-6; Waefeso 5:23. Soma ile sura, yote mawili katika hilo, unaona.

316 Agano la Kale: Kristo, tazama hapa. Hebu tuchukue hili kama mfano. (Labda kama mke wangu hakuchukua dola yangu. Iko hapa. Nililipia vipande vya mkate vyenye nyama ndani muda mfupi uliopita. Samahani, marafiki, sikupenda kusema hilo, lakini-nina mke mzuri.) Sasa,, upaande wa nyuma wa hii dola - (Kama si kwa sababu ya mke wangu, singekuwa na hii dola, nadhani; rehema za Mungu zilitupa naye ananisaidia.) Sasa, nyuma ya hii, inaonekana kama, kama hiyo ni fedha yetu, chapa ya Kimarekani upande wa kushoto wa dola inapasa iwe chapa kuu katika nchi hii. Sawa hiyo? Vema, kwa nini piramidi inaitwa chapa kuu? Hata fedha yenu yapasa iishuhudie. Ndiyo, wakati wote unapotuma posti kadi au barua yakupasa ushuinashuhudia: mwaka wa Bwana wetu, elfu moja mia tisa sitini na mbili. Kila kitu kinamshuhudia Kristo, unaona?

317 Je, uliwahi kuona kuwa ile chapa kuu ni piramidi? Kuna mtu yeyote aliyejua kuwa piramidi hazikuwahi kuwa na jiwe la kifuniko juu yake? Wangapi wanajua hilo? Hakika. Niliwahi kuwa kule Misri, Cairo; nikaiona. Haikuwahi kuwa na jiwe la kifuniko. Kwa nini?-lilikataliwa, jiwe kuu la pembeni. Lile lilikuwa jiwe kuu la pembeni lililoshikilia hili jengo-ni jiwe la katikati ya safina. Wangapi wanajua jiwe la kiungo ni nini? Wakati jingo la muundo wa piramidi linapojengwa, basi jiwe la kiungo ndilo linaloshikilia pamoja. Lile jiwe kuu la pembeni ndilo linaloshikilia jengo, hiyo ni sawa? Na jiwe kuu la pembeni katika piramidi lilikuwa kifuniko-lilikuwa jiwe la kiungo ya safina lililoishikilia yote pamoja. Sasa, hili jiwe la kiungo ya safina lilikataliwa.

Uliwahi kuona , juu kule, linasimama juu, juu ya piramidi. Sasa, hiyo liliwakilisha nini Henoko alipoijenga?

318 Hiki ndicho kilichotokea: ni kama tu kanisa la Injili likija. Unaona, sasa sehemu ya chini ya piramidi iliyopana iliyo chini, inawakilisha siku za kwanza za matengenezo ya kanisa - za kujiita tu wewe mwenyewe Mkristo na kukataa Kanisa Katoliki, ikimaanisha kuwa ungeuawa kwa ajili hilo. Ndipo kukaja-walihubiri kuhesabiwa haki kwa imani.

Ndipo kukaja-Sasa tazama wale watatu wakirudi tena. Akaja John Wesley , akihubiri utakaso, lile Kanisa likazidi kupungua wakawa wachache zaidi. Unaona, likashuka namna hii.

319 Na ndipo baada ya siku za utakaso za John Wesley, likaja kanisa la Kipentekoste, na Mungu akachukua mabaki kutoka huko; kila mmoja aliyelipokea Neno, unaona. Sasa, ilipokuja kwenye Wapentekoste, ilipunguza kwa karibu zaidi kwa sabubu ilikuwa ni kurejeshwa kwa karama. Likiileta moja kwa moja-Ni kitu gani? Chini hapa ni mbali na muonekano wa kichwa. Chini hapa ni karibu kidogo na kichwa. Juu hapa ni karibu kidogo, lakini hilo lapasa lilingane kabisa na yale mengine. Yapasa linolewe. Katika ile piramidi, unaweza kuchukua wembe na hutaweza kuupitisha kati ya mawe mawili pale saruji ilipo; yamewekwa na kulingana pamoja. Walisema hekalu la Sulemani lilikuwa vivyo hivyo. Unaona?

320 Mungu anawachukua Wateule kutoka kwenye lile kanisa la Kipentekoste (lile lililochanganya mbegu) akiwavuta nje na kumalizia Neno. Na ingefanana sana hadi Neno Lenyewe lichanganyike na hili Neno. Pale linakuja Jiwe la kifuniko, likilia, "Neema, neema, neema ya ajabu"-lile Jiwe la Kifuniko. Uko hapa namna hii unaona, juu ya hili. [Ndugu Brnham anatoa maelezo kwa vitendo kwa mkutano-Mh.] Unaona, jinsi linavyokuja chini hapa? Na linaendelea kukaribia, kukaribia, kukaribia (huduma), baada ya muda mfupi anakuja-huyu hapa Luther: kuhesabiwa haki, wakahesabiwa haki. Hapa akaja Wesley: kundi lililotakaswa. Hapa ikaja Pentekoste: kurejeshwa kwa karama.

321 Sasa, Mungu ananzia pale akichomoza kundi kama pembe lenye kufanya huduma kama tu lile Neno kule nyuma, kwa sababu yapasa kulilingana lile Neno. Huyo ndiye Bibi Arusi; atakayemchukua juu.

Sasa, Kristo alidhihirishwa ili aangamize kazi za shetani. Unaamini hilo? Sasa, siwezi kueleza lote hili; nakwenda tu kulipitia, kwa haraka tu sasa; nigonge mahali pa juu ili msikawie hapa kupita kiasi. Kristo alidhihirishwa ili aangamize kazi za shetani. Hiyo ni sawa? Wote mnaamini hilo? Hiyo ndiyo sababu Yeye-Yeye alikuwa nini?-Neno la Mungu, ambalo linaangamiza kazi za mbegu iliyochanganywa, shetani. Hiyo ni sawa? Yeye alishinda ili afanye hilo; Yeye alizaliwa ili awe hilo, kuangamiza kazi za shetani.

Sasa, Mwili Wake utafanya jambo lile lile kwa sababu Mwili ni-Kichwa naa Mwili viko pamoja. Hiyo ni sawa? Ikiwa Kristo ni Kichwa-alikuwa Neno, Mwili Wake yapasa uwe kitu kile kile kama Kichwa Chake kilivyokuwa. Hiyo ni sawa? Kanisa la Neno, lililozaliwa kwa Neno. Bikira aliyezaliwa toka kwenye Neno, sio la dhehebu sasa. Bikira aliyezaliwa kutokana na Neno.

322 Njia ambayo Mwili unatumia kujiendesha ni kwa kuongozwa na Kichwa. Hiyo ni sawa? Mwili wangu hauwezi kutembea hadi kichwa changu kiuambie utembee. Vema, vipi kama kichwa changu ni nyama na mwili wangu ni zege?siwezi kutembea. Kichwa kinaweza kusema, "Tembea, tembea, tembea, tembea, tembea, tembea," lakini hakuna popote pa kutuma ujumbe. Hiyo ni sawa? Vema, ikiwa Kichwa changu ni Kristo na mwili wangu ni dhehebu, utafanyaje kazi? Usafi na kahaba watafanyaje kazi pamoja?

Ee, nalipenda, ndugu; nawaambia. Ningependa kuhubiri juu ya baadhi ya hili kwa muda kidogo. Njia ambayo Mwili unajiendesha ni kwa kuongozwa na Kichwa, na Kichwa ni Neno. Hiyo ni sawa? Kichwa ni Neno.

323 Linganisha kanisa la kisasa, sasa. Kwa nini hatuna miujiza ndani yake? Kwa nini hatuna Neno ndani yake? Haliwezi kufikiwa naNeno; dhehebu linalizuia. Hakika.

Unasema hapa anakuja mtu mzuri mtakatifu wa Mungu, akihubiri Neno la Mungu moja kwa moja toka kwenye Biblia awezavyo; dhehebu: "Loo! Hapana! Hapana, bwana! Mtoe hapa!" Unaona? Mwili hauwezi kutembea; umewekwa mbali na kichwa unapaswa -.

324 Sasa, Mwili huchukua (matendo huchukua) kazi na hufanya kazi zile ambazo unaamriwa na Kichwa uzifanye. Niambie pale ambapo Yeye alisema "unda shirika la dini"! Niambie ni wapi Kichwa husema, "Ni sawa kwa wanawake kukata nywele zao"! Pataje-hapako. Niambie ni wapi Kichwa kiliwahi kusema, "Hizi kazi ninazifanya lakini ninyi hamtazifanya"! Niambie hilo! Lakini Kichwa alisema hili (kama unataka kuandika hilo Andiko, nitakupa: Yohana 14:12), "Kazi nizifanyazo, nanyi mtazifanya pia." Huo ni Mwili Wake, unaona.

Unaona sasa, kwa nini nimekuwa na moyo wa kujali sana ni aina gani ya mbegu niliyokwishaipanda kwa ajili ya Mwili? Mvua itanyesha hivi punde; namaanisha mvua

halisi. Na inapasa kuwe na mbegu ambazo itazinyeshea. Natumaini nitaishi niione. Mnaelewa sasa? Litakuwa Neno hai kama ilivyokuwa hapo mwanzo-Neno la Mungu lililonenwa, liwe na uwezo Wake; kwani upo ndani Yake katika Mwili Wake Mwenyewe, akitenda kwa njia Yake Mwenyewe. Ukisimamia zile zile ahadi Mungu alizoupa Mwili huu.

325 Sasa, tunakuja kwenye jambo fulani. Tunakuja kwenye Mlima Sayuni sasa. Hebu tutazame kile Yeye alichosema kwa huu Mwili-namaanisha waliozaliwa bikira. [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara saba-Mh.] Sasa tunaona kuigwa kwake. Tunaliona kila siku. Lakini hebu tuje kwenye ule Mwili halisi na tuone kile Yeye alichosema kuhusu huo. Hebu tuangalie. Vema, hili ndilo Yeye alililoliahidi.

Unaamini kuwa Yohana 3:16 ni sahihi? Inanipasa tu nisome hili. Hilo ndilo tu lililopo kwa hilo. Vema. U-naweza-Kila mtu anayeamini Yohana 3:16: "Mungu aliupenda ulimwengu akamtoa Mwana Wake wa Pekee," na kadhalika, sema amina. [Kusanyiko linajibu: "Amina."-Mh.] Muwe wajasiri kuamini hayo mengine yote! Nazungumza kuhusu ule Mwili, sasa.

326 Hebu tuchukue Yohana 20 kwa kuanzia. Vema, chukua Yohana sura ya 20 na tuone. Yohana mlango wa 20 na tunakwenda kuanzia kwenye, ee, ningesema kwenye aya ya 19. Yohana Mtakatifu 20, (Naamini hilo ndilo nililoweka alama chini hapa), na kuanzia aya ya 19. Sasa, sikiliza kwa makini.

Nawapa changamoto katika kuliamini! Ee, nalipenda tu. Ee, kama tu ningeweza-natamani ningeweza tu kumwona Roho Mtakatifu akizungukazunguka juu hapa, namna hiyo; aseme, "Sasa, ni Mimi." Sikiliza:

… ikawa joni, siku ile ya kwanza ya juma, pale walipokuwapo wanafunzi, milango imefungwa …(milango ilikuwa imefungwa pale wanafunzi walipokuwapo) … kwa hofu ya Wayahudi, akaja Yesu, akasimama katikati, akawaambia, Amani iwe kwenu …

… (na alipokwishasema) … Naye akiisha kusema hayo, akawaonyesha mikono yake na ubavu wake … (Na wanafunzi wake-hebu tuone-ubavu wake na wakati) … Basi wale wanafunzi wakafurahi walipomwona Bwana.

Basi Yesu akawaambia tena … Amani iwe kwenu: … (Ee, mko tayari?) …kama Baba yangu alivyonituma mimi, … (Yeye ni Neno, ile Mbegu, Mbegu ya Neno) … mimi nami nawapeleka ninyi. (Mnaliamini? Usisimame; kuna mengine zaidi yanayotokana na hilo.)

Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia, akawaambia, Pokeeni Roho

Mtakatifu.

Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wowote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa.

327 Hiyo ni ile Kweli? Yeye alisema hilo kwa nani?-ile Mbegu, lile Neno. Kwa nini?-wangeweza tu kuzaliwa na Neno. Hiyo ndiyo sababu. Unaamini hilo? Hebu tuchukue Mathayo 16 sasa, kwa dakika tu. Mathayo 16:19. Hebu tusome hili kwa dakika moja tu. Vema.

Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote utakalolifubgua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.

Nawapa changamoto mliamini. Na kama hilo sio Neno, Yohana 3:16 sio Neno. Kwa nini uchukue baadhi na usichukue mengine? Neno lote la Mungu liko sahihi, lakini lapasa lije katika tumbo la uzazi la bikira pale ambapo panakaa Mbegu na sio kitu kingine. Mnaliamini? Vema. Sasa, tazama hili kwa makini hasa.

328 Najua yule kahaba analidai hili, na wao huondoa dhambi kwa nguvu zao za kidhehebu. Lakini waangalie watoto wao: kila ukumbi wa dansi, hukata nywele zao, waliopakwa rangi kama wachekeshaji, mwanaume akiishi na wake za watu wengine, wakifanya mapenzi ovyo ovyo barabarani, kuoga wanaume na wanawake pamoja; kila kitu kingine. Hakika, wao husamehe; wao huondoa dhambi katika njia yao wenyewe, lakini matunda yao huonyesha wao ni kitu gani. Sio sahihi wao wanapofanya hivyo, hapana bwana. Huwa wanafanya nini? - wanavaa nguo fupi, wanakata nywele zao, wanajipodoa. Yesu alisema, "Kwa matunda yao mtawatambua," wao ni mbegu ya aina gani. Hicho ndicho kilichopo.

Mbegu ya kidhehebu hutoa msamaha wa kidhehebu. Hiyo ni sahihi hasa. Mungu

alisema, "Na Neno liwe kwa Jinsi Yake Lenyewe," na ndivyo ilivyo. Hiyo ni sahihi. Ee, Ndugu, Maandiko ni ya kweli. Unayaamini?

329 Na Roho Mtakatifu anashuhudia karama iliyochaguliwa tangu asili ambayo kanisa linaidai kuwa nayo. Nini? Kwa kulinyeshea Neno, kuitikia Neno kwa amina.

Wakati Neno Liliposema, "Tubu ukabatizwe katika Jina la Yesu Kristo""Amina!" Linaposema haya mambo mengine-"Amina!" Hilo ndilo lenyewe: "Amina" kwa kila kitu, unaona. Ililiweka Neno ipasavyo. Na Mungu kwaalichagua tangu asili karama ije, ya kuondoa dhambi, lakini ni Mwili wa Neno uliojazwa Roho Mtakatifu ndio uliopewa hiyo karama, kwa sababu ni Neno tu liwezalo kusamehe dhambi, kwa sababu Neno ni Mungu.

330 Mafarisayo walikwa wakweli jinsi gani. Nilitamka hili asubuhi kuwa tungefikia hili, sasa nimechukua muda mrefu. Lakini Mafarisayo walisema, "Huyu mtu anasamehe dhambi. Tunajua yeye anakufuru. Mungu pekee ndiye anayeweza kusamehe dhambi, na huyu mtu amesamehe dhambi"-bila kujua kuwa yule alikuwa Neno. Neno husamehe dhambi kwa sababu Lenyewe ni Mungu. Na unapokuwa siyo mali yako mwenyewe-Mungu anajua-alijua na alijua kabla kwa ufahamu wa kimbele ni nani angechukua hii Karama na nani angeitumia katika njia sahihi. Wale waliyo nayo wamethibitishwa kwa Neno la Mungu pamoja na Neno lote na Roho. Hilo limeeleweka? Wengine wangewafanya muamini likiwajia kwa kusomea, kupata elimu ya juu, shahada; kama ukienda shule kwa muda mrefu; kama ukiwa askofu, ukijifunza kuwa papa, au unakuwa kadinali au kitu kama hicho (kwamba baadhi wangetufanya tuamini kuwa hapo ndipo inakotoka) wakati mtu kwa kukuwekea mikono hukufanya uwe kitu fulani cha kulifanya hilo. Lakini wako nje ya Neno.

331 Warumi 11: 29 ilisema, "Kwa sababu karama za Mungu hazina majuto." Mungu huzitoa. Na pia Yohana 15:16, kama mnataka kuliandika. Sikilizeni, kwa makini sasa. Jinsi gani Yesu katika siku Zake alikuwa tofauti na madhehebu ya siku Yake! Wangemnyooshea vidole Yeye-Ningependa kukaa juu ya hili kidogo. Loo! Wangemnyooshea vidole juu ya mabega yao, wakirudi nyuma katika nyakati na kusema, "Sisi ni wanafunzi wa Musa. Tunajua kuwa Mungu alimtokea Musa katika kichaka kilichowaka moto, tunajua." Walijua-walijua historia ya Musa, lakini hawakumjua Mungu wa Musa, kwa sababu Yeye alisimama mbele yao katika Yohana 6 na kusema, "Kabla Musa hajakuwako-kabla Abrahamu hajakuwako, Mimi niko"-kichaka kilichowaka moto. Walijua historia ya Musa.

Ndivyo ilivyo leo. Wanajua kuwa Mungu-wanadai kuwa wanajua Neno la Kristo, lakini hawamjui Mungu aliyekuwako katika Kristo. Moto uliochorwanani atapata joto kwa moto wa kuchorwa - ujuzi wa seminari? Walimjua Musa, lakini sio Mungu wake.

332 Yesu angeweza na alisema amina! Sikiliza hili, Ndugu. Loo! Sasa, najisikia kama Daudi, akizungusha lile kombeo sasa. Natumaini siwaudhi sana, marafiki. Sina tatizo ila najisikia tu vizuri. Nazidi kujisikia vizuri tu sasa.

Yesu alisema, "Baba aliyenituma yuko ndani Yangu, na kama Yeye alivyonituma Mimi, nami nawatuma ninyi"-kwa wanafunzi Wake. "Baba aliyenituma yuko ndani Yangu. Kama sizifanyi kazi za Neno lililoahidiwa na Baba Yangu, basi msiniamini, kwa sababu hizo ndizo zinazonishuhudia Mimi." Haleluya! Ee, Kanisa, uko wapi? Yesu alisema-walisema, "Ee, tunajua kuwa Mungu alifanya hili, lakini sio leo." Yesu alisema hilo hilo-"Tunajua Mungu alikuwa na Musa."

"Lakini yule Mungu aliyekuwa na Mimi yuko ndani Yangu, kwa sababu kama hamliamini, tazameni yaliyoandikwa kunihusu Mimi. Angalieni kile Maandiko yalichosema ningefanya na kama silingani na Maandiko, basi msiniamini.

333 Hebu niseme hili siyo la kuudhi, ila hebu niseme kuhusu Ujumbe ninaohubiri. Kama Mungu hathibitishi hili kuwa ile Kweli, basi sio; lakini kama Neno linathibitishwa kuwa nawaambia ile Kweli, basi liaminini Neno! Wao ndio hushuhudia kama nasema ile Kweli au la. Wao ndio huo ushuhuda; wanatoa ushuhuda kwa - wanatoa ushuhuda kwa ajili ya huduma ambayo Yeye Bwana alinipa. Yeye aliahidi hili katika siku za mwisho. Liko hapa! Alisema kile ambacho lingefanya. Kiko hapa; tunakwenda moja kwa moja ndani yake sasa! Uone kama ni ile Kweli au la.

Hebu Mungu atoe ushuhuda. Kama kazi, yale mambo ninayoyahubiri hazirudishi ushuhuda kuwa ni ile Kweli, basi sio ile Kweli; lakini, kama Neno linazungumza kuhusu haya, na liko hapa, basi utakwenda kufanya nini kuhusu hilo?

334 Yesu alisema, "Nawajua ninyi; mnadhani mnamjua Musa. Mnamjuamnaweza kujua … historia ya Musa, lakini hamumjui Mungu wake; kwani nilikuwako kabla ya Musa. Mimi Ndiye niliyenena na Musa. Mimi Ndiye ambaye Niko; Mimi ni Neno." Wasingeweza kuliona kwa sababu wao ni wa baba yao, Ibilisi. Madhehebu yao yasingewaruhusu walione. Hilo halikuzuia Neno lkuendelea kama kawaida Yake. Lilianguka juu ya baadhi, na kutokana na hao akaja Bibi Arusi katika kile kizazi.

335 Vema, ni tofauti ya-moto wa kuchora. Yesu alikuwa akisema, "Baba aliyenituma yuko pamoja Nami na zile kazi ninazozifanya zinashuhudia kwa sababu nakwenda kufanya yale yale mambo ambayo Maandiko yalisema ningefanya." Wayahudi walimjua Mungu wao wa kihistoria. Vivyo hivyo sasa, naam. Kwa nini walimjua Mungu wa kihistoria ni kwa sababu walikuwa na mbegu ya kihistoria! Kwa nini hawakumpokea Yeye?-kwa sababu ilikuwa mbegu mchanganyiko na dhehebu. Yesu alimjua Yeye aliyemtuma kwani Yeye aliyemtuma alikuwa ndani Yake, na hakufungwa na dhehebu lolote. Amina! "Niambieni ipi-Yeye alitoka shule gani?" Walisema, "Yeye alipata wapi hii hekima? Hii elimu ilitoka wapi?" Hawakupata shule Ambayo Yeye aliwahi kwenda, na bado kwenye umri wa miaka kumi na mbili Yeye aliwastaajabisha wale Waandishi na Mafarisayo. Loo jamani! Hilo lililitimiza.

336 Kwa nini hawakusema kitu Naye kama mtoto? Lilikuwa Neno la Mungu. Wasingeweza kushindana na hilo. Hata sio ajabu watu walishangazwa na fundisho Lake. Uliwahi kusoma hilo? Marko 1:22; kama mnataka kuliandika. Watu walishangazwa na fundisho Lake kwa sababu Yeye aliongea kama mtu aliye na mamlaka. Yeye alijua kile alichokuwa anakizungumzia. Unaona? Kanisa sasa lingekuwa na kiasi maradufu cha Roho. Kwani ni kweli, kama vazi la Eliya lililoanguka juu ya Elisha (kiasi maradufu), jambo lile lile linatoka kwa Yesu Kristo.

Sasa unasema, "Ee, Ndugu Branham, unazungumza kuhusu Kanisa Lake." Hiyo ni sahihi. Huo ni Mwili Wake. Je, mke wangu sio sehemu ya mwili wangu? Je, mke wako sio sehemu ya mwili wako? Nyama ya nyama yako na mfupa wa mfupa wako; muungano mtakatifu, hiyo ni sahihi? Hiyo ndiyo sababu Mkristo hapaswi kumwoa kahaba, unaona? Hiyo sio sawa. Hapana bwana, kwa sababu hiyo inavunja mambo yote ya Mungu.

337 Unasema, "Ee, Ndugu Branham, subiri kidogo; unazungumza juu ya Roho wa Kristo akiwa juu-" Biblia ilisema ingekuwa. Hiyo ni sawa? Isaya 9:6 ilisema-ilisema, "Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; Naye ataitwa mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, na ufalme wake hautakuwa na mwisho, na uweza wa kifalme utakuwa juu…" Nini? [Kusanyiko linajibu: "mabegani Mwake"-Mh.] Hiyo ni sehemu ya Mwili Wake. Ufalme uko wapi duniani?-katika Mwili Wake. Watakatifu wataihukumu dunia. Hiyo ni sawa?

Paulo alisema, "Msithubutu kupelekana mahakamani bila kulipeleka mbele ya kanisa." Hiyo ni sahihi. Watakatifu watahukumu dunia. Ufalme utakuwa juu ya nini?-mabegani, Mwili Wake. Ufalme juu ya mabega Yake. Hiyo ni sehemu ya mwili.

Ni kitu gani?-Uwezo Wake wa duniani. Uwezo wa duniani wa Mungu ni Neno Lake lililofanyika mwili katika Mwili Wake hapa duniani, unapolileta.

Musa-

338 Sikiliza, hebu tuyaruke mengine. Wajumbe wa Mungu siku zote wamekataliwa. Unaamini hilo? Musa alikataliwa. Hiyo ni sawa? Yesu alikataliwa. Na Luka alisema, katika 10:16 (kama unataka kuliandika, vema)alikataliwa; (1Samweli 8:7, Ujumbe wa Mungu ulikataliwa. Mungu. Mungu alikuwa na mjumbe, nabii aliyeitwa Samweli. Je unaamini hilo? Walimkataa pamoja na Ujumbe wake. Waliuchukua ulimwengu. Hii ni sheria ya-ya Mungu. Hii itakwenda-sijui kama niliseme hili au la. Hii ni sheria ya Mungu. Sheria ya Mungu ni kupokea mtumishi aliyethibitishwa. Hebu tu-hebu tu tuthibitishe hilo kwa dakika moja. Nataka nichukue moja ya Maandiko hapa: Yohana 13:20. Hebu tuone tu; Nina kitu fulani kimeandikwa hapa. Ni-namna ya-nilikuwa nacho akilini mwangu ndipo tu-Ee, naam, hivyo ndivyo.

Amin, amin nawaambia, Yeye ampokeaye mtu yeyote nimpelekaye, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenipeleka.

Mtumishi aliyethibitishwa. Ee, Ndugu, kuna mahubiri elfu yaliyokaa hapa hapa sasa. Unaona? Hiyo ni sahihi. Loo jamani, ni sheria ya Mungu; ipokee.

339 Samweli alikuja na kusema, "Nataka niwaulize jambo fulani. Je, nimewahi

kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana ambalo halikutokea?"

"Hapana."

"Je, nimewahi kuchukua sadaka zozote ili kujenga majengo makubwa na kufanya mambo mengi makuu, na kujitukuza mimi mwenyewe?"

"Hapana!"

"Je, Mungu amethibitisha na kujibu lile Neno nililolisema?"

"Ndiyo!"

"Vema, kwa nini hamnisikii?"

340 Yesu aliwaambia Mafarisayo … "Tunajua mmezaliwa katika uasherati." Yeye alisema, "Yupi miongoni mwenu anaweza kunihukumu jkuwa nina dhambi? Hebu niwaonyeshe Neno la Mungu na nione kama mnaliamini. Nione kama Mungu analithibitisha ndani yenu. Na hebu niseme juu Yangu Mwenyewe. Ikiwa nanena Mwenyewe, Mimi ni mwongo, lakini kama nanena juu ya Mungu na Mungu ananena kupitia Mimi kwa Neno Lake, basi ni ile Kweli. Basi nani anayeliamini Neno la Mungu: Mimi au ninyi?" Aha! Walikuwa nalo!

Yesu alisema, "Awapokeao wale niliowatuma, anipokea Mimi." Na sasawale Anaowatuma. "Na wale wanipokeao Mimi wanampokea Yeye aliyenituma." Natamani tungekuwa na wakati wa kukaa juu ya hilo.

341 Unaweza tu kumtumikia Mungu kama-unaweza tu kumtumikia Mungu kama ufanyavyo na-na kuwaamini watumishi Mungu anaowatuma. Unaweza tu kumtumikia Mungu duniani (unaona) kama watumishi wa Mungu waliotumwa duniani kwa uvuvio wa Kiungu wanalifasiri Neno kwako.

Unaamini hilo? Unataka kuandika Maandiko kwa ajili ya hilo? 1Wakorintho 14:16. Paulo alisema, "Nifuateni mimi kama ninavyomfuata Kristo." Vile vile, 11:1; Luka 10:16. Uone kile Alichosema; kile Alichosema pale, Luka 10:16. Naamini tumelikaribia hapa. Hebu tuone kile linachosema wakati mmoja hapa. Luka 10:16, wakati wanapoandika hayo mengine. Sasa, hiyo ni 1Wakorintho 14:16, 11:1 pia, na Luka 10:16. Sasa hebu tusome. Nachukua Luka 10:16 hapa, ili kusoma tu wakati ninyi wote mnatazama hayo mengine sasa, kwa muda mfupi tu. Vema, tumefika hapa.

Awasikilizaye ninyi ananisikiliza; naye awakataaye anikataa mimi; naye anikataaye mimi amkataa yeye aliyenituma."

Hilo linathibitisha kuwa Mungu husema Ujumbe Wake kupitia watumishi Wake. Siku zote amefanya hivyo; hiyo ni sahihi.

342 Sasa, uwezo wa kanisa lililoamini: Kristo ana uwezo wote mbinguni na duniani. Unaamini hilo? Basi vipi ikiwa Yeye yu ndani yako? Je, Kristo anao uwezo wote? Mathayo 28:18. Vema.

Yeye ni Neno lililo Mbegu katika Mwili Wake, na Yeye ndani yetu anakuwa Neno lililo Mbegu ndani yetu. Kile-yote yale Mungu aliyokuwa, Yeye aliyamwaga ndani ya Kristo, na yote Kristo aliyokuwa, yalimwagwa ndani ya Kanisa; huo ndio uwezo.

343 Sasa tazama! Kumbuka sheria ya Mungu ya uzazi. Sasa kumbuka, kwa jinsi yake. Hiyo ni sawa? Mbegu ya Kristo, lile Neno, lazima ije kupitia Mwili Wake. (Ee, mnachoka? Vema, kwa dakika moja tu, sasa. Hebu tutulie kimya tu na kuomba.) Nataka kulipata hili vizuri hasa. Nataka hili lisagike kabisa. Ile Mbegu ya Kristo lazima, l-a-z-i-m-a, lazima ije kupitia Mwili Wake-sio kupitia dhehebu, ila kupitia Mbegu ya Neno iliyozaliwa upya-lazima ije kupitia hiyo.

Sasa, kumbuka, ni kitu gani? Mbegu ya Kristo-Mbegu yangu inakujaje?kupitia mwili. Jinsi gani mbegu ya mti wa tofaa inakuja?-kupitia mwili. Mbegu ni kupitia mwili, na Kanisa ni Mwili wa Kristo. Hiyo ni sawa? Lile Kanisa la Biblia. Huu uzazi unamleta (huo ni uzazi mpya) Mwenyewe katika mwili. Kanisa Lake ni Neno Lake, kwa hiyo wale watu wanaweza kuona uthibitisho wa Waebrania 13:8: "Yesu Kristo ni yule jana, leo, na hata milele." Unaliamini? Hizi sio mbegu za kidhehebu zilizochanganywa sasa. Hizi ni zile zilizo katika mzunguko zikisubiri matayarisho ya mwisho kwa ajili ya tukio (mnajua ninachokimaanisha), zikijiandaa kuruka. Utukufu! Hizi sio mbegu za kidhehebu zilizochanganywa, sio hizi zilizosimama ndani hapa, siyo. Hapana, bwana, ni ile Mbegu.

344 Paulo alihofia kuwa wale watu walitazamia namna fulani ya maneno makubwa ambayo yeye angeweza kusema (baadhi ya elimu yake). 1Wakorintho 2:1-8, unataka kuliandika. 1Wakorintho 2:1-8, Paulo alisema, "Sikuja kwenu nikinena maneno (ya kielimu, unajua) ambayo imani yenu ingeweza kuwa katika baadhi ya mambo ya kiseminari, ila nilikuja kwenu na urahisi, katika nguvu na udhihirisho wa Roho Mtakatifu ili maneno yenu-ili imani yenu ikae katika Neno la Mungu. Naam, bwana."

345 Ingawa makanisa ya kidhehebu yatamzidi Bibi Arusi katika uwiano wa elfu moja kwa moja-Unaamini hilo? Unaamini kuwa Biblia inalifundisha hilo? Isaya 54:1. Yeye aliahidi hilo. Kwa ajili-hupe-mnataka nilisome? Vema, hebu tulipate. Kama mnataka kuona pale lilipo pale Yeye alipoliahidi kwamba wangezidi, hebu tupate pale Isaya 54 …53…54:1.

Imba, wewe uliye tasa, wewe usiyezaa; paza sauti yako kwa kuimba, piga kelele, wewe usiyekuwa na utungu; maana watoto wake aliyeachwa ni wengi kuliko watoto wake yeye aliyeolewa, asema Bwana.

Hiyo ni sawa? Watoto wa kahaba ni wengi kuliko wale wa mke aliyeolewa. Hakika, wanazidi mara nyingi. Ingawa watakuwa wengi kwa tarakimu hawana baba wa kweli!

Sasa, aina za kidhehebu zinawakilishwa katika Yuda 8-13. Hilo ni kanisa la kiulimwengu. "Mawingu yasiyo na maji, yakitoa aibu yao yenyewe kama povu." Kanisa la Kipentekoste linawakilisha lile kundi katika 2Timotheo 3:18. "Wenye mfano wa utauwa"-mbegu yao ilizaa jinsi yao.

346 Angalia, yule towashi-Ee hapa, tunakwenda kuingia katika jambo fulani kwa kina sasa. Sasa tazama, hili Kanisa lililo Mbegu, hili Kanisa halisi lenye mbegu ya uzazi halisi. Angalia, yule towashi amekuwa na shahada za juu za elimu ya dini - D.D zote. Sasa kumbuka, Mungu hakuwahi kukabidhi - Mungu hakuwahi kukabidhi kuhubiri Kwake na Injili Yake kwa Malaika. Wangapi mnajua hilo? Wangapi mnajua kuwa Wagalatia 1:8 ilisema, "Kama Malaika akija kutoka mbinguni na kuhubiri kitu kingine tofauti na … wao walichohubiri na alaaniwe"? Kwa hiyo Malaika anakosea, ikiwa yeye anatofautiana na Neno. Mungu alishuka chini, ya Malaika, na kuikabidhi kwa wanadamu, ambao walikuwa wana. Unaamini hilo? Sasa tazama! Sasa Yeye hakuwahi kuikabidhi kwa Malaika. Angalia, Yeye hakufanya hilo.

347 Sasa, Filipo alikuwa kwenye Pentekoste, Yerusalemu, kwa ajili ya kuabudu. Wangapi wanasema, "Amina," kwa hilo? Yule towashi alikuwa tayari ana shahada zote za elimu ya juu ya dini (D.D) na za elimu ya juu ya maarifa ya dini (L.D), na kila kitu. Lakini kwa nini hakupata kitu? Anarudi akijifunza unabii wa Isaya.

Ingawa Malaika alimwelekeza Filipo kwake, lakini mbegu ya Uzima ilipasa ije kupitia mwili-Filipo. Ee, Ndugu, sasa tuko kwenye mstari! Mbegu ilitoka wapi? Kupitia Malaika? Malaika alimwonyesha pa kwenda. Malaika ni mjumbe; hapa yupo mwana. Filipo alikuwa na mbegu ya uzazi, ule Ujumbe, lile Neno. Hivyo ndivyo mtoto anavyoweza kuzaliwa. Filipo aliweka mikono juu yake. Filipo akambatiza katika Jina la Yesu Kristo. Pale akaja Roho wa Mungu. Hakika.

Sasa, ilipasa mbegu ije kutoka kwenye mwili. Mwili gani?-Mwili wa Kristo. Sahihi. Na Filipo alikuwa sehemu ya huo Mwili.

348 Sasa sikiliza, kitu kile kile kilitokea katika Matendo 10:48. Petro alikuwa darini. Malaika alimwelekeza kwenye nyumba ya Kornelio, lakini Neno lilitoka wapi? - ule Mwili. Najisikia vizuri hasa; najisikia kuendelea na safari.

Malaika alikuja na kusema, "Usiogope, usiite chochote najisi, endelea tu; usiwaze lolote." Na Petro aliponena haya maneno-sio Malaika, sio kadinaliPetro aliponena haya maneno. Nini? Yeye alikuwa ule Mwili. Yeye alikuwa na Neno. Neno lilishika hatamu. Loo, Ndugu! Wiu! Umph! Loo jamani! Malaika alilielekeza, lakini Uzima ulikuja kupitia Mwili wa Kristo.

349 Paulo, akielekea Dameski, ono lilimwelekeza; lakini Anania (hiyo ni mbegu) alikuwa na Neno. Amina! Yule nabii, Anania, aliona ono na kusema, "Nenda juu kule na uweke mikono yako juu yake."

Akasema, "Ndugu Sauli, Bwana alikutokea njiani ukija hapa." Alijuaje? Yeye alikuwa na Neno. Neno la Bwana lilikuja kwa nabii. Alitabiri, akaenda juu kule, na kusema, "Alikuja-alinituma hapa ili niweze kukuwekea mikono, na ungepona na kumpokea Roho Mtakatifu - upate kuona!" Na magamba yakaanguka machoni pake, na akasimama,

akabatizwa katika Jina la Yesu na akaenda kujifunza. Malaika alilielekeza. Hiyo ni sahihi. Lakini, Paulo alikuwa na kiini cha Mbegu.

Inamhitaji Roho wa Mungu, Mbegu kutoa Uzima wa Milele Wiu! Jamani!

350 Tayari imefika saa nane? Najua hilo. Nitasoma baadhi basi. Hebu nisome kwa dakika kumi tu, mnakubali?. Nina wazo zuri-ningeweza kukaa hapa, lakini ni bora niendelee kidogo hapa, na tutatoka bila kuchelewa. Ni saa kumi na moja kasoro dakika ishirini na tano. Sijui ni muda gani tutafika Georgia! Natamani ningeweza kumaliza na kueleza juu ya hili kidogo, lakini nitalisoma tu, kwa taratibu hasa.

351 Sasa sikiliza kwa makini. Hapa kuna kile nilichonyanyua kalamu kwa ajili yake, sehemu yake. Mnaona, marafiki, nilicho nacho-jinsi nimesimama nilivyosimama? Mnaona ni kwa nini nashindana - kutoka kwenye madhehebu na kupata Kanisa halisi la Mungu? Mnaona ni kwa nini yapasa litoke kwenye Neno? Haliwezi kuja kwa hekima ya mwanadamu, inapasa lije kwa Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sababu naamini Neno tu kama lilivyoandikwa. Sitaongeza chochote au kupunguza chochote; ila kulihubiri namna hiyo; niendelee tu moja kwa moja.

Sasa, ndugu (ninyi nyote mnaosikiliza kanda), kama hamkubaliani na mimi, nitawaombea; kama niko makosani, mniombee. Nitasoma baadhi tu sasanataka msikilize hili kwa makini hasa. Hapa ndipo Roho aliposema, "Chukua kalamu." Inabidi niyaache baadhi yake, lakini yanipasa kuyaleta baadhi yake kwenu.

352 Vema. Sasa, hili ndilo ninalojaribu kuwaambia: sheria ya uzazi inaleta kila moja kwa jinsi yake (Mwanzo 1:11). Hizi siku za mwisho, Bibi Arusi wa Kanisa wa kweli anakuja kwenye Jiwe la Kifuniko. Litakuwa kanisa bora sana; Jamii bora sana wanapokaribia lile Jiwe la Kifuniko. Watakuwa zaidi kama-zaidi kama Yeye, hata watakuwa wa sura Yake halisi, ili kwamba waungane na Yeye. Watakuwa Mmoja. Watakuwa udhihirisho halisi wa Neno la Mungu Aishiye. Madhehebu kamwe hayawezi kufanyiza hili. Hili litakuwa - watafanyiza maungamo yao ya imani za dini na kanuni za imani yaliyochanganywa na Neno na-na kuleta zao mchanganyiko.

353 Mwana wa kwanza, alikuwa Neno la Mungu lililonenwa lililo Mbegu. Alipewa bibi arusi. (namkariri tu Roho, na nilikuwa nachukua kile nilichosema, unaona) Bibi Arusi atazaa-kumzalia tena huyo mwana. Alianguka-(Unaona, hicho ndicho bibi arusi alichopewa, kuzaa mwana mwingine wa Mungu, lakini al;ianguka kwa kuchanganya mbegu, unaona.) Alimzalia huyo mwana - lakini alianguka; alimsababisha yeye kufa.

Mwana wa pili Neno la Mungu lililonenwa lililo Mbegu alipewa bibi arusi kama Adamu, lakini kabla Yeye hajamuoa, alikuwa ameanguka pia; kwani alipewa uhuru wa kuamua apendavyo kama mke wa Adamu alivyokuwa, aamini Neno la Mungu aishi, au alitilie shaka afe-na alifanya hivyo.

354 Ndipo kutoka kwenye kundi dogo la Mbegu ya kweli ya Neno, Mungu atamletea Kristo Bibi Arusi mpendwa, Bikira-Bikira wa Neno Lake-na kupitia wao na kwa wao yatatimizwa yote yale yaliyoahidiwa kwa ajili ya Neno Lake katika Bikira, ambaye hajui maungamo ya imani za dini na kanuni za imani zilizotungwa na mwanadamu. Neno la ahadi kwa Yeye Mwenyewe, kama ilivyokuwa kwa Mariamu - Mungu Mwenyewe akidhihirishwa. Yeye atatenda, Yeye Mwenyewe, kwa Neno Lake Mwenyewe la ahadi ili kutimiza yote yale yaliyoandikwa juu Yake. Kama Yeye alivyofanya alipotoka kwenye tumbo la uzazi la bikira (mfano wa tumbo la uzazi la roho sasa), vivyo hivyo na Bikira sasa, akipokea Neno Lake: "Na iwe kwangu kama ulivyosema," ingawa lilisemwa na Malaika, hata hivyo lilikuwa Neno lililoandikwa (Isaya 9:6) Watampenda Yeye (Watawapenda - ), na watakuwa na tabia Zake zote, kwani Yeye ni Kichwa chao, nao ni watu Wake, wanategemea Kichwa Chake. Ukuu wa Kristo ulikuwa Wake.

355 Tazama, maelewano ya ajabu. Yesu hakuwahi kufanya lolote hadi aone kutoka kwa Baba au Baba amwonyeshe kwanza. (maelewano kati ya Mungu na Kristo, unaona, Yohana 5:9) Hivyo hivyo na Bibi Arusi, na Yeye anamwonyesha Bibi Arusi Neno Lake la Uzima (Yeye anamwonyesha Bibi Arusi), naye analipokea. Hakuwahi kulishuku.

Hakuna kitakachomdhuru Bibi Arusi, sio hata kifo; kwani kama Mbegu ikipandwa maji yataifufua tena. Amina. (Sasa, nina Haleluya kubwa ajabu!) Siri iko hapa; Neno liko ndani ya Bibi Arusi na nia ya Kristo ili kujua kile Yeye anachotaka kifanyike kuhusu Neno, na Bibi Arusi anakifanya katika Jina Lake. Anayo HIVI ASEMA BWANA.

Ndipo inaoteshwa; kwa hiyo Roho Mtakatifu anainyeshea hadi inakua na kutimiza

kusudi lililokusudiwa. Wanatenda tu yaliyo mapenzi Yake. (Amina! Nitaliamini hilo.) Hakuna yeyote anayeweza kuwashawishi vinginevyo. Wana HIVI ASEMA BWANA, au wanakaa kimya. Basi watafanya kazi za Mungu. Kwani ni Yeye Mwenyewe ndani yao, akiendeleza kulitimiza Neno Lake kama Yeye alivyomaliza katika siku Zake. Vitu vyote-Yeye alipokuwa hapa-Yeye hakumaliza yote alipokuwa hapa, kwani wakati ulikuwa bado.

356 Sasa, hebu tusimame kama Yoshua na Kalebi. (Sasa, tazama kwa makini, hili litakuwa na msingi wa kiroho.) Sasa, hebu tusimame kama Yoshua na Kalebi. Tunapoona ile nchi ya Ahadi inaanza kuonekana. Ili tupewe - Yoshua kwa Kiebrania humaanisha Mwokozi na inawakilisha kiongozi wa wakati wa mwisho aliyeahidiwa kulivusha Kanisa. Kalebi huwakilisha mwamini wa kweli aliyekaa na Yoshua. Mungu alianzisha, Israeli wakiwa bikira, kwa Neno Lake, lakini walitaka kitu tofauti. Hivyo hivyo kanisa la siku za mwisho.

357 Tazama jinsi Mungu hakuwatoa Israeli, hadi wakati Wake Mwenyewe alioupanga. (Sasa sikiliza. Hili linakwenda kumaanisha jambo fulani.) Yoshua alisubiri ule wakati! Ee jinsi-Haidhuru ni watu wangapi wangekuwa wamesema, "Mungu alitupa nchi, ile ahadi, hebu twende sasa na kuimiliki." Wangeweza kusema, "Yoshua, umepoteza utume wako. Wewe umekwisha kabisa. Kwa nini hufanyi chochote? Ulizoea kufanya-kujua HIVI ASEMA BWANA katika muda mfupi na kile kilichokuwa mapenzi ya Mungu." Lakini huyu nabii mwenye hekima aliyetumwa na Mungu alijua ahadi ya Mungu lakini pia alijua kusubiri ile ahadi-uamuzi sahihi toka kwa Mungu kwa ajili yake.

(Hii mifano? Sasa tazama.) Na wakati ulipowadia Mungu alimpa Yoshua, ambaye alikaa na Yeye kwa Neno, kwani Yeye hangeweza kuwaamini wengine; Mungu alimwamini yeye. Kwa hiyo litajirudia.

358 Kama yule nabii mwenye nguvu mpakwa mafuta Musa alijua Mungu angemtumia, kwani Yeye alikuwa amemthibitisha Musa kuwa mtumishi Wake kwa kuzaliwa kwake kulikokuwa kwa kipekee. Kwenye wakati uliofaa ambao kama-ukombozi kwa ajili ya mbegu ya Abrahamu ulikuwa wakati ule. (Mnalielewa?) Musa hakuwahi kukaa Misri na kubishana nao juu ya mambo ya kimaandiko. Hakuwahi kuhangaikia kwa makuhani, lakini alikwenda jangwani na kumsubiri Bwana hadi-hadi watu walipokuwa tayari kumpokea. Alikuja kuwashuhudia, lakini hawakumpokea. Mungu alimwita nabii Wake kule jangwani. Mungu alikuwa ameshuhudia; Alimchagua yeye, lakini kusubiri hakukuwa kwa Musa, ila kwa ajili ya watu kuwa tayari kumpokea Musa. Musa alifikiri kuwa wale wana wangeelewa kuwa yeye alikuwa ametumwa. (Siyo mimi niliyeliandika. Ni Yeye, kwa hiyo ndivyo ilivyo sasa.)

359 Kama Eliya , baada ya yule nabii mkuu aliyethibitishwa ambaye Neno la Mungu lilikuja kwake alipomaliza kuhubiri Ujumbe wake kwa yale makundi ya kisasa ya Kimarekani ya mke wa rais akiwa amenyoa nywele na makundi ya Yezebeli yaliyojipaka rangi - Mungu alimthibitisha nabii Wake; kila wakati alipotabiri; ilikuwa kweli - Mungu ilibidi amwondoe kutoka uwanja wa huduma hata akakipiga kile kizazi kwa mapigo makuu kwa ajili ya kukataa Ujumbe wa nabii Wake na Neno la Mungu ambalo Yeye alikuwa amewatumia.

Mungu alimtuma jangwani akajifiche. Hata mfalme hangeweza kumwita atoke huko. Na wale waliojaribu kumshawishi kinyume na mapenzi ya Mungu walikufa kwa kufanya hivyo! Loo, utukufu! Wiu! Umph! Lakini Mungu aliponena na nabii Wake mwaminifu kwa ono, kule jangwani alikuja na HIVI ASEMA BWANA. Yeye nabii alifanya nini? Moja kwa moja kwenye Neno, alirudi kwenye Neno. Akaleta mawe kumi na mawili na kuyafunga pamoja.

360 Kama Yohana Mbatizaji, mtangulizi mwaminifu, nabii aliyepakwa mafuta, hakwenda shule ya baba yake, hakwenda shule ya Farisayo, hakuna dhehebu lingeweza kumwita atoke nyikani alikotumwa na Mungu hadi asikie Sauti ya Mungu, Mwana-Kondoo wa Masihi!

Mnasikiliza nia ya kiroho? Nitasema yapi zaidi hapa? Naruka mambo fulani hapa sasa.

361 Leo ni tofauti mno! Wengi wanaoitwa wainjilisti wanadai wana jibu toka kwa Mungu kwa ajili ya watu, kama tu Kora alivyofanya - akikana, akishindana na mamlaka ya nabii wa Mungu aliyethibitishwa na kupakwa mafuta, Musa, akidai yeye alikuwa na jibu. Huu ulikuwa mpango wa kutengeneza fedha, pia-ndama wa dhahabu, kama wengi wafanyavyo leomajengo makubwa, shule kubwa, wakiangua kutoka kwenye mashine za

kuangulia mbegu zao zile zile. Na ndipo basi watu-kama sasa, walivutiwa na hilo baada ya kuwa wamesikia Neno la Mungu kupitia nabii aliyepakwa mafuta aliyekuwa amethibitishwa.

Walivutiwa na uongo wa Kora. Nabii wa Mungu aliyethibitishwa, na Mungu alijua-na walijua Mungu alikuwa amewaambia-Israeli walijua Mungu alikuwa amewaambia wazi kuwa Yeye angewathibitisha manabii Wake kwa Neno Lake. Kora hakuwa nabii wa kimaandiko, lakini iliwapendeza sana watu; sawasawa tu kama inavyofanya sasa. Leo-leo ni damu mikononi mwako, vimondo jukwaani, mafuta katika vidole vyako; na jambo lile lile hufanyiza wanawake wahubiri, nywele fupi-zilizokatwa, kujipamba … Una nini? Hugewaza kuwa watu wangevutiwa na hilo, lakini walivutiwa na Kora, na wanafanya kitu kile kile sasa na kugeuka kutoka kwenye Neno la kweli na kwenda kwenye madhehebu. Nguo fupi: hii ni kuonyesha ni aina gani ya mbegu iliyoko ndani yao.

362 Lakini Mungu ashukuriwe sio Israeli wote waliovutiwa na Kora. Baadhi walikaa na Musa, nabii aliyepakwa mafuta kwa Neno la Mungu. Ndivyo ilivyo leo kwa wengi wa Wateule wa Mungu, kwa Neno Lake na Roho Wake.

363 Kumbuka, magugu, majani, yatakusanywa na kufungwa matita matita. Hiyo ni sawa? Hili limekwishatukia. Makanisa yaliyo mashirika yaliyoasi Neno yanafungwa na kukazwa zaidi kuliko yalivyowahi kufungwa. Yanawekwa matita matita pamoja katika shirikisho la makanisa, tayari kwa moto wa hukumu ya Mungu. (Sikuandika hili ili nije kulihubiri, najisikia kuwa ni Yeye Bwana aliyelifanya hili.) Wapentekoste wamejaa kile kinachoitwa-kile kile kama wao. Lile Neno la ngano litakusanywa siku moja baada ya kuondoka kwenda kwa Bwana.

364 Mungu ameahidi (uwe mwangalifu!)-Mungu ameahidi Malaki 4 kwa ajili ya hii siku ya mwisho, na Malaki 4 haijatimizwa bado, lakini lazima itimizwe kwani ni Neno la Mungu lililochipuka, lililonenwa kupitia Malaki, nabii. Yesu alilitaja. Litakuwa kabla tu ya kuja kwa Kristo mara ya pili.

(Sikiliza kwa makini sasa.) Maandiko yote ambayo hayajatimizwa, lazima yatimizwe, kabla ya ule wakati. Biblia itakuwa imetimia - itatimizwa; Majira ya Mataifa yatakwisha pamoja na kipindi cha kanisa. Huyu mjumbe aliyepakwa mafuta atakapowasili, bila shaka, yeye atapanda Mbegu ya Biblia yote, tangu wakati wa yule nyoka wa zamani hadi wakati wa yule mjumbe, katika mvua ya masika. Ndipo yeye atakataliwa na watu wa kidhehebu kama mhenga Yohana na Eliya, kama ilivyonenwa na Bwana wetu-watu-kama Eliya alivyokuwa mara ya kwanza kwenye wakati wa Ahabu. Itatokea hapa katika nchi hii, kwani hii nchi ni mfano wa Israeli.

365 Soma au sikiliza mahubiri ya Dini ya Yezebeli. Kama nchi hii - Wahenga wetu … waliabudu walivyotaka, walikuja katika nchi hii na kuwafukuza wenyeji na kujichukulia nchi; vivyo hivyo Israeli walijichukulia nchi walipokuja kutoka Misri. Tulikuwa na watu wacha Mungu kama Washington, Lincoln. Walikuwa na mtu mkuu mcha Mungu kama Daudi na kadhalika. Ndipo wakampata Ahabu kwenye kiti cha enzi akiwa na Yezebeli nyuma yake kumwongoza-nasi tunaye! Kwa hiyo ni wakati huu, katika nchi hii kwamba yule mtu atatokea. Kwa kuwa liko katika Maandiko, na ni HIVI ASEMA BWANA.

366 Ndipo katika mvua ya vuli kutakujaMlima Karmeli, onyesho la kupeana ukweli - Biblia ikitimizwa kwa makini kabisa bila ya lolote kusalia. Yohana Mbatizaji, mjumbe Wake aliyetangulia mbele Zake katikaMalaki 3 alipanda mvua ya awali na alikataliwa na yale makanisa (madhehebu-Mafarisayo na Masadukayo) katika siku yake. Yesu alikuja na alikuwa na na onyesho la ukweli alipogeuka sura Yake kule Mlimani. Huyu mtangulizi wa siku za mwisho atasia mbegu kwa ajili ya mvua ya masika. Yesu atakuwa onyesho la kupeana ukweli kati ya madhehebu na maungamo ya imani (ambao ni Neno Lake). Yeye atakapokuja, lile onyesho la kupeana ukweli - Unyakuo wa Bibi Arusi Wake! Wa kwanza ulikuwa Mlima Karmeli; wa pili ulikuwa Mlima wa Kugeuzwa; wa tatu utakuwa Mlima Sayuni! Utukufu!

367 Tabia ya Eliya, tabia ya Musa, tabia ya Yohana, wakiondoka kwenye uwanja wao wa huduma-watu wengi hawakuwaelewa. Ilikuwa kwa sababu walikataliwa pamoja na Ujumbe wao. Mbegu ilikwishapandwa; hukumu ilikuwa ifuate, na kulikuweko na ishara kwa watu kutoka kwa Mungu kuwa hukumu ilikuwa imekaribia. Wakati wa kusia mbegu ulikuwa umekwisha.

368 Naamini siku moja Bibi Arusi halisi wa Kristo atalazimishwa kuacha kuhubiri Neno la Mungu. Biblia inatabiri juu yake katika Ufunuo 13:16 (kama unataka kuliandika).

Madhehebu yatalazimisha kusitisha, au wachukue "alama" yake. Basi Mwana-Kondoo atamchukua Bibi Arusi Wake na kumhukumu kahaba kwa ajili ya hili.

369 Kumbuka Musa, alizaliwa kwa ajili ya hiyo kazi, ilimpasa amsubiri Mungu kwa ajili ya karama ya ziada kwa ajili ya ile kazi. Ilimpasa arudi na kusubiri.) Na kwa wakati uliokusudiwa na Mungu Farao fulani ilipasa awe kwenye kiti cha enzi. Na ilibidi wawe wanautaka Mkate wa Uzima kabla Mungu hajamrudisha. Sasa, pamoja na maelfu ya watenda ishara katika hii siku ya mwisho imefanya kizazi cha watafuta ishara, ambao hawajui tena - lolote kuhusu utendaji wa kweli wa Mungu katika Neno Lake katika hizi siku za mwisho.

Kama nilivyokwishasema, "Wape damu na mafuta na maonyesho ya kimwili kwenye jukwaa, na wataliunga mkono iwe ni Neno la Mungu au hapana, kama ni la kimaandiko au la." Yesu ametuonya juu ya vitu kama hivi kwenye wakati wa mwisho. Kama nilivyosema, katika Mathayo 24, roho mbili, zinafanana sana, zingewadanganya hata walio Wateule kama ingaliwezekana. Utawezaje kuwaambia? Wape jaribio la Neno. Utawezaje kujua hilo? Nena Neno; angalia watakavyosema juu Yake. Kama hawaliamini Neno hawana uzima wa Mbegu ndani yao. Wao ni wa yule mwovu na wanakudanganya. Kama vile yule bibi arusi wa kwanza alivyodanganywa ndipo na bibi arusi wa pili alidanganywa. Wao ni wadanganyaji wa bibi arusi wa tatu kwa kuchanganya Neno, au kujaribu kulichanganya.

370 Mungu hakuwahi kuweka ishara zitangulie Neno Lake. (Amina! Hilo ni la kuchoma.) Mungu hakuwahi kuweka ishara zitangulie Neno Lake. Ziliongezwa kwa ajili ya kuthibitisha Neno,, lakini Neno ni la kwanza.

Kulithibitisha, Eliya alimwambia yule mwanamke, "Nitengenezee mkate kwanza." Basi angalia muujiza ukitokea. Njoo kwenye Neno kwanza ndipo uone muujiza. Neno la Mbegu lenyewe ndilo linalopewa nguvu na Roho Mtakatifu. Sasa mjumbe aliyetumwa toka kwa Mungu anaweza tu kuamini baadhi ya Maandiko na sio Neno lote?-akatae sehemu yake.

371 Nabii wa kweli wa Mungu atapiga mbiu ya Neno katika siku za mwisho; madhehebu yatamchukia. Hatapunguza mashambulizi yoyote juu yao. Atakuwa kama alivyokuwa alipokuja kwenye kuja kwa kwanza kwa Kristo. "Enyi kizazi cha nyoka!" Lakini wale waliochaguliwa tangu asili watasikia na watakuwa tayari kwa matayarisho ya mwisho kwa ajili ya tukio. Ila Mbegu ya kifalme ya imani ya Abrahamu (kama yeye) ikishikilia kwenye Neno la Mungu hata iwe nini, kwani yeye alikuwa amechaguliwa tangu asili. Mjumbe wa Malaki 4 atatokea kwenye wakati wa Mungu alioukusudia. Sote tunamtafuta. Tunaamini atakuja. Hiyo ni kufuatana na Neno Lake; itakuwa kwenye wakati wa mwisho, ambapo wakati wa kuona hilo ni sasa.

372 Atakuwa sa-atakuwa amewekwa wakfu kwa usahihi kwa Neno kama ambavyo wamekuwa siku zote; kwa kuonyeshwa na Neno la Mungu-na kuthibitishwa. Mungu atathibitisha kile yeye anachohubiri kuwa ni ile Kweli kama alivyofanya juu ya Eliya; kwani ni Eliya anayekuja, akitayarisha Unyakuo wa Mlima Sayuni. Yesu alisema katika siku za mwisho itakuwa kama wakati wa Lutu. Kuhubiri kwake kutakuwa pamoja naye Roho na mstari ulionyooka wa Neno la Mungu. Kwa sababu mengi yameitwa Kweli ya Mungu, wengi watamwelewa vibaya huyu mjumbe wa kweli. (Nimeandika hapa u-n-ab-I-I ), unabii. Kwa sababu-kwa sababu mengi mno yameitwa Kweli ya Mungu na waigizaji, wahudumu wengi wa kweli watamwelewa vibaya yule mjumbe.

373 Kama ambavyo unabii wa wakati wa mwisho utajirudia, naamini, kama vile mtangulizi wa kwanza alivyokuja toka nyikani na kupiga kelele, "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu", mtangulizi wa pili inaelekea atafanya kile kile akiwaelekeza watu kwenye Neno-Bibi Arusi aliyezaliwa. Bibi Arusi wa Kristo ataelekezwa mawinguni kwenye kuja kwa Yesu, akipiga kelele, "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu!" litatoka midomoni mwake. Mungu tusaidie kuwa tayari kwa hili tukio lililo karibu.

374 Sasa, ni bora nikaliachia hapa hapa.

Unaamini? Kwa nini hili limekuwa? Unao ufahamu mzuri zaidi sasa? Ni Neno marafiki. Hili limekuwa kwenye masaa sita (inakaribia kabisa), matano na nusu au masaa sita. Kuna mengi zaidi ya kusema, lakini hakika Roho Mtakatifu kwa wakati huu ame-amelizamisha kwa kina zaidi ndani yenu, kwamba mnajua kile ninachozungumzia. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Mbegu zimekwishapandwa sasa; mvua ya vuli inajiandaa kuja.

Kumbuka, kutakuwa na mkusanyiko wa kidhehebu karibuni sana; kiasi kwamba utakuwa wa kutisha. Na watajikusanya pamoja katika hili shirikisho la makanisa, na ndipo aina hii ya kanisa itatolewa kwenye utendaji (jinsi wanavyojua). Ni kwenye huo wakati ambao Yesu atatokea, na Yeye ataonyesha ni yupi Bibi Arusi na yupi sio.

375 Na kumbuka,, marafiki Wakristo, mimi ni mwanadamu; naweza kukosea, lakini Mungu, akiwa Yeye ndiye Mungu hawezi kukosea. Maneno yote yaliyoandikwa sharti yatimizwe, Yesu alisema hivyo. Kwa hiyo tuna mambo hapa katika Maandiko ambayo ni lazima yatimizwe, na hilo ni mojawapo ya hayo mambo - huu ususiaji unaokuja. Lakini kabla ya kuweza kuja kwa huu ususiaji (wa kuweka alama ya mnyama), kutakuwa na Mbegu iliyopandwa kwa ajili ya Mungu kulichukua Kanisa kutoka kwake. Mnaelewa sasa? Inapasa Mbegu ipandwe. Mbegu ya kidhehebu na pale-kufanya sura au sanamu ya mnyama (kanisa la Rumi); na yapasa kuwe na Bibi Arusi wa Kweli.

376 Na tunaelewa kuwa yule aitwaye bibi arusi amekataliwa-bibi arusi wa Adamu alikataa kuleta Uzima. Alileta kifo; sisi ni zao lake (mwili wetu); sote tunakufa. Tutazame, unaweza kuona.

Bibi arusi wa Yehova alikufa; Yeye alimpa talaka na kuchukua watu kutoka Mataifa kwa ajili ya Jina Lake. Hiyo ni sawa? Jina Lake-kama mwanamke huchukua jina la mwanamume, bibi arusi. Sasa bibi arusi amefanya nini? Kitu kile kile walichofanya ule wakati mwingine, alijifanya dhehebu mwenyewe; akajichafua. Lakini katika kila kizazi, kila uamsho huleta manabii wa Mungu (nabii ni muhubiri, muhubiri wa kweli wa Neno ambaye hukaa na Neno), na wanaleta uamsho ambao hukusanya wateule kutoka katika kile kizazi. Ndipo bibi arusi anakwenda kuwa mbegu. Basi Mungu hataitumia tena. Nauliza mwanathiologia yeyote, mwanahistoria yeyote aniambie wakati mmoja ambao dhehebu liliwahi kuinuka; halijawahi. Alikufa alipofanyika dhehebu, na pale ndipo anapolala.

377 Nawaza juu ya Dwight Moody, ile Biblia ya Moody-iliyokufa kama usiku wa manane. Nawaza juu ya wamethodisti, Wapentekoste, Wapresbiteri, Walutheri, Wanazareti, na Pilgrim Holiness; watu wacha Mungu walioinuka, Buddy, Robinson na George Whitefield na wote hao watu wakuu wacha Mungu wote waliohubiri Injili, na kile kizazi kilichopokea ile mbegu iliyopandwa kwa ajili ya sehemu yao. Kama nafaka-ikiwa ni bua, kama ilikuwa jani, kama ilikuwa kishada, kama ilikuwa punje, chochote kile, yule mhudumu alileta Neno la Mungu la siku ile. Liliita toka pande nne za dunia na kuchukua wateule wa kile kizazi. Kupitia wale Wateule kumejengwa Nyumba ya Mungu aliye hai.

378 Sasa, hii huduma hapa yapasa inolewe na kuchongeka hadi ifike mahali ambapo zile zile kazi alizofanya Yesu-kwa sababu Yeye atakapokuja, Jiwe la Kifuniko litaingia moja kwa moja ndani yake, kwa sababu hawata-kutakuja Unyakuo, nao watachukuliwa, na wale wengine walio sehemu ya ule Mwili watakuja nao; na Bibi arusi atakuwa amekwenda Mbinguni. Sio dhehebu, marafiki; Kanisa la Neno la Mungu. Mnaliamini? Hapa kuna baadhi ya leso, hapa.

379 Sasa, nakwenda-sijui ninakokwenda. Natafuta, mapenzi ya Mungu, kama wewe. Natamani ningekaa kwenye hili hekalu; siwezi kufanya hilo. Kuna maelfu-nasikia kilio-roho mchafu akiwararua. Nalala kwa shida. Nasikia watoto wadogo wakilia na kuona akina mama wakiwasukumia watoto wao kwenye mstari wa maombi, namwona mama uani akimpepea mtoto, akiwa ameshika shuka juu yake kumkinga na mvua. Nawaonea huruma nyingi.

380 Nilipojenga hili hekalu, siku nilipoweka jiwe la pembeni pale, nakumbuka lile ono asubuhi ile. Nililiandika pale pale ndani ya jiwe la pembe; akasema, "Hili sio hekalu lako. Fanya kazi ya mwinjilisti; hakikisha huduma yako." Nalipenda hili; nawapenda watoto wa Mungu kila mahali. Sijui Yeye atakakoniongoza. Sijui; nasubiri. Nimesubiri kwa mwaka. Naweza kusubiri kwa miaka miwili; naweza kusubiri kwa miaka mitatu, sijui. Sijui litakalofuata. Nalisubiri. Lakini, nawaza kufuatana na Maandiko, Neno limekwishapandwa. Jambo linalofuata ni kuja kwa Roho.

381 Billy Graham anaweza kuhubiri kila mahali; Oral Roberts, wale watu wacha Mungu wanaweza kuhubiri kila mahali. Bwana anaweza kunituma kusia mbegu mahali pengine (shamba fulani), lakini naamini taifa letu limepandwa mbegu, na naamini liko tayari kwa kuvunwa sasa.

Wakati Roho anaposhuka na kunatokea msukumo wa utendaji miongoni mwa watu, madhehebu yataungana katika hilo na kwenda pamoja kwa dhahiri tu kama

nilivyosimama mimbarani. Na Kanisa la Mungu litafukuzwa, na watafanya hii kuwa ghasia kubwa hata watafanya hili kuwa Shirikisho na kuweka ususiaji juu ya yeyote ambaye si wa kwao. Rumi, itatawala ulimwengu kwa saa moja tu. Itatawala kwa kipande kidogo. Sio UkomunistiUromani, utatawala ulimwengu wakiwa katika ushirika na Uprotestanti, katika muundo wa kanisa la kidhehebu, ambalo Mungu amelikataa. Hilo liko karibu kama nijuavyo Neno la Mungu.

382 Nawapenda. Nawafurahia ninyi. Labda nitarudi kwenye Jumapili ijayo. Nakwenda Florida sasa, Bwana akipenda, kule Georgia kwa kesho usiku.

Ninayo mikutano michache iliyosambaa huko na huko. Kama Bwana akiongoza, nina kitabu kilichojaa hayo - hayo mambo akina Ndugu Robersonau Bordres alinitumia siku ile nyingine. Nadhani kuna-kulikuwa na sehemu ambapo kuna makanisa thelathini na arobaini yaliyo tayari kushirikiana, lakini Roho anaonekana kunizuia. Sijui kwa nini. Sijui kwa nini. Kwa hiyo mniombee, nami nitawaombea. Tusimame pamoja. Na Bwana atusaidie. Kusiwe na hata mmoja wenu hapa ambaye atashindwa na kuukosa ule wakati mkuu unaokuja.

383 Sasa, nimeshutumiwa mambo mengi, marafiki, na nina hatia katika mambo mengi. Mimi ni msahaulifu; hiyo ni kweli. Sijui ni kwa nini imekuwa hivyo. Inabidi mtu fulani anisukume hadi pembeni na kunifanya nipigane. Sijui; hiyo ni asili. Nimefanya mambo ambayo yasingepasa kufanya, sio kwa kukusudia, lakini nimeteka nyara katika hilo. Na hilo ndilo (kwa hiyo) hunifanya kuogopa mno, kwa kuona siku hii (ile siku tunayoishi)-na unaona sasa kile ninachoamini. Nataka niskie kutoka kwa Mungu kama inawezekana, kabla sijafanya kitu, unaona, kwa sababu sitaki kumkosea Yeye. Nataka niwe na Yeye kila mahali. Na nataka ninyi mniombee.

384 Na kumbukeni, nimewaambia ile Kweli. Sasa, nawashukuru kwa kuketi hapa siku yote hii (tangu mapema asubuhi hii); wengi wenu mkiwa mmesimama kuzunguka kuta na ukumbi wote, nyayo na miguu ikikakamaa kwa baridi na uchovu, mkiwa mmeketi ndani ya magari; betri zenu zikiisha nguvu kutokana zaidi na kusikiliza, na ndilo hili hapa; lote liko kwenye kanda. Vijana wamelinasa pale, na unaweza kulipata.

Na ikiwa utalipata, lichukue nyumbani na ujifunze kwa makini hasa na kwa hekima, na uone kile Bwana atakachokufunulia. Unampenda? Teddy yuko wapi? Kabla tu ya kuomba kwa ajili ya hizi leso na watu, nataka nimwombee kila mmoja wenu. Nataka kuimba huu wimbo sasa, na ndipo Ndugu Neville atatoa tangazo lake kwa ajili ya huduma nyingine.

Nampenda, Nampenda (Je, unalipenda Neno Lake? Basi unampenda.)

Sababu alinipenda kwanza

Na akanunua wokovu wangu mtini Kalvari.

385 …nafikiri, Mungu, Yeye Mwenyewe, hutoa tafsiri ya Kiungu; na nina hakika, Bwana, ikiwa nimeleta Neno litaanguka juu ya wale waliochaguliwa tangu asili lianguke juu yao. Neno Lako ni Kweli. Baba, nasikitika kwamba nilikukosea mara nyingi. Nakuomba unisamehe. Naomba usamehe mkutano wangu, waliopo hapa na wasiokuwepo hapa, dhambi zao zote; kwamba Bwana Mungu, tunatambua kuwa tuko mwishoni mwa njia. Kila ishara iko hapa hapa mbele yetu. Nina hakika akili ya kiroho, Bwana, hushika kile nilichosema dakika chache tu zilizopita. Naomba kwamba wataelewa, Bwana, kuwa kile tuna-pale tulipo. Tuko hapa …

386 missing text

387 missing text

MESSAGE online hub

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

*"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7*